

Uhakiki Wa Mtindo Katika Tamthilia Za Arege

Fridah Gesare Oiko

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI
ZA KIJAMII ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA
UZAMILI KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA**

CHUO KIKUU CHA MAASAI MARA

2017

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi..... Tarehe.....

Oiko, Fridah G.

AM01/6006/2012

IDHINI

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Maasai Mara kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili.

Sahihi..... Tarehe.....

Dkt. James Omari Ontieri

Idara ya Lugha, Isimu, Mawasiliano na Uanahabari

Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Sahihi Tarehe.....

Dkt. Emmanuel Simiyu Kisurulia

Idara ya Lugha, Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Kabianga.

HATIMILIKI

Fridah Gesare Oiko © 2017

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kupiga chapa, kutafsiri au kuitoa kazi hii kwa njia yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

TABARUKU

Kwa Lameck China (mume wangu) na watoto wetu, Caleb Omwenga, Calvin Ababu, Alicia Kerubo na Anne Moraa. Pokeeni kwa mapenzi ya mama.

SHUKRANI

Safari hii imekuwa ndefu tu. Tulipofika ni kipumuo tu wala si kituo. Safari ya mbali huanza kwa hatua moja, na hili limetupa ari ya kuendelea hadi tulipofika sasa. Tujuavyo, safari huwa na vikwazo ambavyo humhitaji msafiri kuvumilia na kuwa na matumaini ya kufika mwisho mwema. Haya ndiyo niliyapata kwa wengi wahisani alonipa Maulana kama zawadi.

Kwanza kabisa, shukrani zangu ni kwake Maulana kwa baraka zake za kuniwezesha tangu nilipong'oa nanga hadi kufikisha chombo changu masafa haya. Yeye amezidhibiti dhoruba na mawimbi yalokumba meli yangu kwa kuyawinga na neema zake. Asante Maulana.

Dkt. James Omari Ontieri na Dkt. Emmanuel Simiyu Kisurulia, kwangu mmekuwa si wasimamizi tu bali masahibu waliokeshwa nami ili kuona kwamba kazi hii imeonekana ilivyo na kufikia ukamilifu ilioupata. Asante kwa ushauri, subira na uelekezi wenu wenye hekima mlionisusia nao. Nyinyi mlinihimiza hasa nilipoelekea kukata tamaa kwa kupanda meli yangu na kuchukua usukani na kuisukuma mbele ya safari hii. Fahamu kuwa nyinyi ni injini ya utafiti huu. Mbarikiwe kifu ya Mungu.

Wahadhiri wangu wote wa Kiswahili; Prof. Ernest Sangai Mohochi, Dkt. Samuel Obuchi na Dkt. Nancy Ayodi Mokaya, shukrani zangu ni nyingi mno kwenu. Kwa mchango wenu, nawashukuru sana. Mafunzo mliyoni na ushauri vimenifaa sana katika utafiti huu. Maarifa mliyolijaza bongo langu yameniondolea kiwi kwenye macho yangu na kunipa werevu wa kina. Kusema ukweli usiotiliwa chumvi, mlininoa nami sikuwa butu wa kunoleka. Aidha, maarifa haya ndiyo yaliyoniwezesha kupasi katika mitihani yote niliyoifanya. Msichoke kuwafaa wasomi wengine maana mwahitajika zaidi kuliko yanavyoweza kueleza maneno ya shukrani zangu. Jua na mfahamu kuwa bila msaada wenu na maelekezo labda nisingeweza kufikia hapa nilipo. Mliuwekea utafiti huu msingi thabiti ambao ndio mwongozo niliufuata.

Mwisho na muhimu kwa utafiti huu, ni mume wangu Lameck na watoto wetu Caleb, Calvin, Alicia na Anne kwa kuwa wahisani wa karibu wa kunitia moyo kwa kila hatua ya

utafiti huu. Kila nilipowatazama nilipata ilhamu ya kuukamilisha. Kwa hakika mlinifanya kuwa na ilhamu ya kuikamilisha tasnifu hii. Mungu awavuvie neema zake.

Kuna wengi walioutakia heri utafiti huu kwa njia moja ama nyingine, fahamuni kuwa nawahisi ingawa sijawataja. Furaha inanikosesha msamiati mwafaka wa kuwashukuru. Namuomba Mungu awabariki wote kwa mkupuo huo.

ORODHA YA VIFUPISHO

n.k.	–	na kadhalika
uk.	–	ukurasa
n.w.	–	na wenzake
k.v.	–	kama vile
Prof.	–	Profesa
Dkt.	–	Daktari
Bw.	–	Bwana
TY	–	Tafsiri Yetu
TUKI	–	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

IKISIRI

Matini yoyote ya fasihi huhitaji kusomwa na kueleweka ili ipate kuwa na maana. Hata hivyo, maana ya matini hujitokeza ikiwa msomaji ataelewa mtindo uliotumika kuisuka. Japo huu ndio ukweli, mapitio tangulizi ya maandishi yameonyesha kuwa kuna tafiti chache zilizofanywa kwa kina katika kubainisha mtindo katika fasihi kama kipengele muhimu na kinachojisimamia kufafanua maana na hasa katika tamthilia za Arege. Hivyo basi utafiti huu umehakiki mtindo uliotumika katika tamthilia tatu za Arege ili kutoa mchango katika kuzielewa tamthilia hizi kwa kina. Ili kufikia lengo kuu, tumechanganua, vipengele mbalimbali vya kimtindo ili kuonyesha umaarufu wao katika uwasilishaji wa maudhui tukiongozwa na maswali matatu ambayo ni: i) Arege ametumia mbinu gani za usimulizi kuwasilisha maudhui katika tamthilia teule? ii) Mbinu za usimulizi alizotumia zimesaidia vipi uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia teule? iii) Je, tamathali zilizotumika zimesaidia vipi kuwasilisha ujumbe katika tamthilia teule? Utafiti umeongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo iliyoasisiwa na Leech. Kimsingi, nadharia hii hujihusisha na uchunguzi wa jinsi lugha inavyotumika ili kuleta ujumi katika matini za fasihi. Katika kuchunguza mtindo, ndipo usanii wa kazi ya fasihi hutambulika na kuelezea nafasi ya mwandishi katika kuimulika jamii katika uhalisia wake. Matini za Arege zilizohakikiwa kimtindo ni tamthilia tatu ambazo ni: *Kijiba cha Moyo*, *Mstahiki Meyu* na *Chamchela*. Mbinu ya kimaksudi ya kuteua sampuli ndiyo ilitumika katika kuchagua tamthilia teule tatu ili kuwakilisha uandishi wa Arege katika kipengele cha mtindo. Data ya utafiti ilipatikana maktabani kutokana na usomaji wa maandishi yaliyohusiana na malengo na maswali ya utafiti. Uchanganuzi wa data uliongozwa na mbinu ya uhakiki matini ambapo data iliyokusanywa ilipangwa kwa kuegemea maswali ya utafiti ambapo vipengele vya kisintaksia na kisemantiki katika tamthilia zilizoteuliwa vilibainiswa na kuchambuliwa. Data iliyopatikana ilipangwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinathari. Utafiti huu umebaini kwamba mtindo ndio huamua jinsi ujumbe unavyopokelewa na unavyoeleweka. Vilevile, imegunduliwa kwamba Arege ametumia lugha kwa ubunifu na hivyo kuleta ujumi katika maudhui anayosuka katika tamthilia zilizoteuliwa. Aidha, utafiti umebaini kuwa Arege ametumia mtindo wa kinaya ili kuwakejeli Waafrika waliouandama ukoloni mamboleo kikasuku. Mtindo huu umetawala katika tamthilia zote ili kuonyesha kuwa lengo la Arege ni kuwaonyesha Waafrika kuwa wao ndio chanzo cha shida wanazokumbana nazo. Utafiti huu ni wa manufaa kwa wasomi na wapenzi wa fasihi kwa kuwa umetoa mwanga wa kuzielewa na kuzielezea tamthilia tatu zilizoteuliwa kimtindo. Kwa maandishi wa fasihi, utafiti unawafaa kwani utawawezesha kuelewa mbinu mbalimbali za kuandika matini zenye mvuto wa kisanaa ili kuwasilishia jamii ujumbe kwa ubunifu mkubwa. Aidha, utafiti ni wa manufaa kwa watafiti kwani watakapousoma watakuwa katika nafasi bora ya kuuwekea wao msingi.

ABSTRACT

Stylistic studies as a field of study is not only bound to describing literary works but also to offer the most significant function of interpreting them. This in turn enables scholars to decode the meaning or meanings conveyed in the texts. Though not the only way of rendering literary works more meaningful, style contributes greatly to their appreciation and relevance. As much as this is the fact, literature review has revealed that few researches do recognise style as the determinant of interpreting meaning in literary works. As such, this research aimed at analyzing style in Arege's three plays with an aim of enhancing their appreciation. The study was guided by three research questions namely: i) What are the salient stylistic features employed by Arege in the three plays? ii) What is the significance of the stylistic features on the themes in the plays? iii) How do the figures of speech impact on the message conveyed in the three plays. The literary works of Arege used in this study are his three plays namely: *Chamchela*, *Mstahiki Meya* and *Kijiba cha Moyo*. The study employed purposeful sampling in selecting the three plays to represent Arege's literary world. The study relied on the stylistic theory advanced by Leech (1969) and its tenets enabled the researcher to answer the three research questions effectively. Basically, this theory aims at exploring the way language is used to bring up aesthetic value in literary texts. The study was library based where close reading of texts and other resourceful materials was done based on the research questions to obtain data for analysis. Data collected was based on two levels of style: the syntactical and the semantic. Content analysis technique was used in analyzing data collected and research findings were presented descriptively in accordance with the research questions. Data analysis reveals that style impacts heavily on the message conveyed by the author. It was discovered that Arege relies heavily on irony in explaining the plight of African people under neo-colonialism. Arege uses irony to rebuke African leaders with the intention of awakening them from their ignorance which is the greatest undoing in the development yearned for, in African states. The study is of great significance to scholars who have interest in Kiswahili literature and more so to those with special interest on stylistics for they will be able to understand and appreciate the plays in context. It will also be an inspiration to new researchers to embark on studying style in other literary works with an aim of understanding them. The study is also an inspiration to the upcoming writers since it will enable them understand the various stylistic devices they can use to weave their works and hence come up with better works in the literary world.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI.....	ii
HATIMILIKI.....	iii
TABARUKU.....	iv
SHUKRANI.....	v
ORODHA YA VIFUPISHO.....	vii
IKISIRI.....	viii
ABSTRACT.....	ix
YALIYOMO.....	x
SURA YA KWANZA.....	1
MISINGI YA UTAFITI.....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Usuli wa Mada.....	1
1.3 Suala la Utafiti	3
1.4 Malengo ya Utafiti.....	4
1.5 Maswali ya Utafiti.....	4
1.6 Upeo na mipaka ya Utafiti	4
1.7 Sababu za Kuchagua Mada.....	5
1.8 Umuhimu wa Utafiti	6
1.9 Msingi wa Kinadharia	6
1.10 Mapitio ya Maandishi.....	10
1.11 Mbinu za Utafiti	20
1.11.1 Muundo wa Utafiti	20

1.11.2 Eneo la Utafiti.....	21
1.11.3 Idadi Lengwa.....	21
1.11.4 Uteuzi wa Sampuli.....	22
1.11.5 Ukusanyaji wa Data.....	22
1.11.6 Uchanganuzi wa Data	22
1.12 Hitimisho.....	23
SURA YA PILI.....	24
MTINDO WA UWASILISHAJI WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA	
TEULE	24
2.1 Utangulizi	24
2.2 Arege na Uandishi wake.....	24
2.3 Mtindo wa Uwasilishaji wa Maudhui.....	24
2.3.1 Uwasilishaji Maudhui katika tamthilia ya <i>Chamchela</i>	26
2.3.2 Uwasilishaji Maudhui katika tamthilia ya <i>Mstahiki Meya</i>	29
2.3.3 Uwasilishaji Maudhui katika tamthilia ya <i>Kijiba cha Moyo</i>	36
2.3.4 Wazo Kuu la Mwandishi katika tamthilia zilizoteuliwa.....	40
2.4 Hitimisho	41
SURA YA TATU.....	42
MBINU ZA USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA ZA AREGE.....	42
3.1 Utangulizi.....	42
3.2 Sintaksia.....	42
3.2.1 Mdokezo.....	43

3.2.2 Maswali ya Balagha.....	46
3.2.3 Kuchanganya Ndimi.....	54
3.2.4 Uzungumzi Nafsia.....	56
3.2.5 Usambamba.....	62
3.2.6 Nyimbo, Ushairi na Sauti.....	69
3.3 Hitimisho.....	71
SURA YA NNE.....	73
TAMATHALI ZA USEMI KATIKA TAMTHILIA ZA AREGE.....	73
4.1 Utangulizi.....	73
4.2 Tamathali za Usemi.....	73
4.2.1 Tashbihi	75
4.2.2 Tashhisi	81
4.2.3 Methali	90
4.2.4 Tabaini.....	100
4.2.5 Kweli kinzani.....	104
4.2.6 Taswira.....	108
4.2.7 Takriri	113
4.2.8 Nahau	116
4.3 Hitimisho.....	120
SURA YA TANO.....	122
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	122
5.1 Utangulizi	122
5.2 Muhtasari wa Utafiti	122

5.3 Matokeo ya Utafiti	123
5.4 Mahitimisho.....	126
5.5 Mapendekezo	126
Marejeleo.....	128
KIAMBATISHO A: BARUA YA NACOSTI.....	134
KIAMBATISHO B: KIBALI CHA UTAFITI.....	135

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.1 Utangulizi

Sura hii ni tangulizi na ambayo imetoa mwongozo wa utafiti huu. Ni katika sura hii ambapo vipengele mbalimbali vimejadiliwa ili kuibua na kuweka wazi suala la utafiti. Vipengele vilivyojadiliwa ni usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Vilevile, tumejadili sababu za kuchagua mada, umuhimu wake, upeo na mipaka ya utafiti. Aidha, nadharia iliyouongoza utafiti wetu na mapitio ya maandishi mbalimbali kuhusu mada hii yamechanganuliwa ili kuonyesha pengo tulilolenga kuziba. Mbinu zilizotumika kupata data tuliyochanganua zimeshughulikiwa pia katika sura hii.

1.2 Usuli wa Mada

Mtindo kama kipengele cha fani hutumiwa kukuza maudhui pamoja na dhamira katika kazi ya fasihi. Mtindo hutekeleza haya kwa kutumia lugha kwa njia ya ubunifu. Tamthilia ya Kiswahili kama utanzu mojawapo wa fasihi imepitia awamu mbalimbali kimtindo na vilevile kimaudhui kwa nia ya kuleta ujumi na pia ukubalifu. Hali hii huenda sambamba na mabadiliko ya kijamii. Mabadiliko ya kimaudhui ndiyo hasa yameshurutisha matumizi ya mitindo tofautitofauti ili kuyafafanua na kuamua uelewekaji wake (Ntarangwi, 2004). Utafiti huu ulilenga kuhakiki vipengele vya kimtindo katika tamthila teule na nafasi yao katika kuendeleza maudhui.

Wamitila (2002) anasema kuwa uhakiki ni uchunguzi wa kazi za kifasihi kwa makini na kwa utaalumu. Uchunguzi wa aina hii unahusisha mambo kadha kama: uchanganuzi fasiri, uelezaji, ufafanuzi tathmini na utoaji wa kauli ya kijumla au hukumu. Mambo haya yote huwezesha kazi ya kifasihi kueleweka vyema zaidi na hivyo kufaidi kutokana na thamani zake za kiumbuji wa kisanaa. Hii ina maana kwamba dhana ya uhakiki inahusu uchanganuzi wa sehemu mbalimbali za matini za kifasihi na kuzitolea maelezo ya jinsi sehemu hizo zinavyoingiliana na kukamilishana. Nayo fasiri kwa upande mwingine inarejelea kuchunguza na kutathmini wasifu wa kazi husika pamoja na yaliyomo (usanii

na dhamira au maudhui). Na hivi vyote huchangia katika kufafanua mtindo katika fasihi. Hili ndilo lengo mojawapo la utafiti huu.

Dhana ya mtindo imeshughulikiwa na wahakiki wengi hasa katika karne hii. Hii inatokana na ukweli kwamba mtindo ndiyo njia kuu inayosaidia uelewaji wa maudhui yanayoshughulikiwa katika matini husika. Madai haya yanashikiliwa na mtaalamu Simpson (2004) anaposema kuwa uchanganuzi wa kina wa mtindo huifanya kazi ya fasihi kueleweka vyema na kwa kina. Licha ya kushughulikiwa kwa mapana na marefu kuna tofauti kubwa sana kutegemea mtazamo na nia ya mhakiki. Dhana ya mtindo ina mawanda mapana na hufafanuliwa na wataalamu mbalimbali kwa njia zinazotofautiana. Maana kuhusu dhana ya mtindo hutegemea zaidi uelewa na mtazamo wa mhakiki wa vipengele anavyochagua kuvishughulikia. Mtindo huweza kufafanuliwa kwa kutumia wahusika, msuko, maudhui, na lugha (Ngara, 1982). Hata hivyo mtafiti alilenga kuhakiki mtindo kwa upande wa lugha na jinsi inavyosaidia ukuzaji na uelewaji wa maudhui.

Tamthilia ni mojawapo ya tungo za fasihi zinazotumia lugha kwa ufundi mkubwa. Ni kwa muktadha huu ambapo tamthilia inafafanuliwa kama utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo. Usanii huu ndio unaobainisha mtindo wa tamthilia kwa kutumia lugha (TUKI, 2004).

Ingawa dhana ya mtindo inaweza kuwa na mitizamo mbalimbali, kwa mujibu wa Holman (1976) mtindo una vitengo viwili: jinsi wazo linavyodokezwa na ubinafsi wa mwandishi. Hii ni ishara kuwa mtindo hulenga kudhihirisha ubinafsi wa mtunzi katika matini za fasihi, mawazo na lengo la fikra za mtunzi mwenyewe. Kwa muktadha huu basi mtindo unaweza kurejelewa kama mtu au usanii wa kazi husika. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa tuna mtindo-mtu na mtindo usanii. Mtindo-mtu ni aina ya mtindo unaomtofausha mtunzi mmoja na wengine. Senkoro (2011:25) katika kuweka wazi maana ya mtindo-mtu, anasema hivi:

Mtindo ni ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya kifasihi sura ya kifani na kimaudhui kwa njia ambayo msanii mwingine asingeweza kuipa hivyo hata kama jambo linaloongelewa na wasanii hawa wawili ni lile lile moja.

Wamitila (2003) anatoa mfano ili kufafanua mtindo- mtu kwa uwazi. Anaeleza kuwa kazi za Mohamed S. Mohamed hujumuisha matumizi mapana ya jazanda na isitiari pamoja na unyumbufu wa kisintaksia ilhali kazi za Adam Shafi zimejaa lugha nyepesi na zina tamathali chache. Na hii ndiyo tofauti ya watunzi hawa.

Kwa upande mwingine mtindo-usanii ni mtindo unaochukulia matini ya fasihi kama zao linalojisimamia katika muktadha fulani mahususi. Kwa mujibu wa mkabala huu basi matini huchanganuliwa na kuhukumiwa katika kiwango cha ubunifu bila kuihusisha na mwandishi kwa kiasi kikubwa kama ilivyo katika mkabala wa mtindo-mtu. Uhakiki huu umeegemea kitengo cha pili kwa kiasi kikubwa katika kuchanganua mtindo wa tamthilia teule za Arege.

Leech (2008) anafafanua mtindo kama jumla ya vipengele vyote vya lugha ambavyo vinajitokeza katika kazi ya kifasihi. Vipengele hivi hujumlisha urudiaji, maumbo ya lugha na tamathali za usemi. Maelezo haya yanaashiria kuwa mtindo huchunguzwa kupitia kwa vipengele vya lugha. Ndio maana Leech (1969) anaeleza kuwa kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri pasina maarifa ya lugha ambayo ndiyo njia ya kujieleza. Hili ni lengo mojawapo katika utafiti huu.

Mtindo wowote ule anaoutumia mwandishi ni kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe wake kwa ufaafu kwa hadhira lengwa. Kwa hivyo, uteuzi wa mtindo hutegemea falsafa yake, mazingira, nyakati na aina ya ujumbe anaonua kuwasilisha. Mtindo unahusu namna ya kuitumia lugha ili kufikia ujumbe unaotaka kutolewa, na mara nyingine kuifikia maana au ujumbe huo pamoja na taathira fulani kama kipengele cha ziada katika matumizi ya lugha. Utafiti wetu umeegemea maelezo ya waandishi hawa katika kuufafanua mtindo wa tamthilia teule za Arege kwa kuwa tunalenga kuonyesha kuwa mbinu zinazomwezesha mtunzi wa fasihi kuwasilisha ujumbe wake kwa mantiki ndizo bora zaidi.

1.3 Suala la Utafiti

Matini yoyote ya fasihi huhitaji kusomwa na kueleweka ili ipate kuwa na maana. Hata hivyo kueleweka kwa matini hujitokeza ikiwa msomaji ataelewa mtindo uliotumika. Japo

huu ndio ukweli, tafiti nyingi zilizofanywa hazijazama kuangalia mtindo kama kipengele kinachojisimamia na tena maarufu katika kufafanua maudhui. Mapitio tangulizi ya maandishi yameonyesha kuwa hakuna utafiti uliofanywa kwa kina katika kubainisha mtindo kwenye tamthilia za Arege. Hivyo basi utafiti huu umelenga kuziba pengo hilo kwa kuhakiki mtindo katika tamthilia tatu za Arege ili kutoa mchango katika kuzielewa tamthilia hizi kwa kina.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti ulilenga kuhakiki mtindo katika tamthilia tatu za Arege. Ili kufikia lengo letu tumeshughulikia yafuatayo:

- i) Kuchanganua mbinu mbalimbali za usimulizi zilizotumika katika tamthilia za Arege.
- ii) Kupambanua mchango wa mbinu za usimulizi zilizotumika katika uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia tatu zilizoteuliwa.
- ii) Kuchambua tamathali za usemi katika tamthilia zilizoteuliwa na ufaafu wao katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi.

1.5 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti huu yalikuwa:

- i) Arege ametumia mbinu gani za usimulizi kuwasilisha maudhui katika tamthilia teule?
- ii) Mbinu za usimulizi zilizotumiwa na Arege zimesaidia vipi uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia teule?
- iii) Je, tamathali zilizotumika zimesaidia vipi kuwasilisha ujumbe katika tamthilia teule?

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulihakiki mtindo katika tamthilia tatu za Arege ambazo ni: *Kijiba cha Moyo* (2009), *Mstahiki Meya* (2009) na *Chamchela* (2007). Tamthilia hizi ni jumla ya kazi alizochapisha mwandishi huyu katika kipera cha tamthilia na zimetusaidia kueleza mtindo kwa sababu zina vipengele vilivyoweza kufafanulia ili kuuweka wazi mtindo wa tamthilia teule. Mtindo katika kipengele cha lugha una kategoria nyingi. Utafiti ulijikita katika kategoria tatu ambazo ni: uwasilishaji wa mawazo, sintaksia na semantiki.

1.7 Sababu za Kuchagua Mada

Kushughulikiwa kwa mada hii kulichochea na sababu nyingi. Kwanza, Arege ni mwandishi chipukizi ambaye ameanza uandishi wa tamthilia katika miaka ya hivi karibuni (2009) hivyo basi hajatafitiwa sana kama waandishi wengine mashuhuri. Hii inaonyesha kuwa pana haja ya kuchunguza jinsi anavyoilezea na kuisawiri jamii yake na vilevile kubainisha iwapo ana uwezo wa kutumia lugha ili kuelezea ujumbe wake ipasavyo. Mwandishi huyu ni wa karne ya ishirini na moja na hivyo kazi zake zimeshughulikia mitindo mahususi katika kuwasilisha maswala yanayoikumba jamii finyu na ile pana. Kwa sababu hii kazi zake zinakuwa na umuhimu ambao huwezi kupuuzwa. Tamthilia hizi ziliteuliwa madhali zimetungwa na mtunzi mmoja kwa vipindi tofautitofauti hivyo basi zilitupa data iliyotuwezesha kubainisha mtindo wa mtunzi katika kazi zake. Aidha, tamthilia hizi zimegusia mambo muhimu yanayoiathiri jamii ya leo.

Pili, mojawapo ya tamthilia alizoziandika (*Mstahiki Meya*) ilipata nafasi ya kuteuliwa kwa mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne (2013). Pia mwandishi huyu aliandika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* iliyompelekea kujishindia tuzo la Jomo Kenyatta Foundation (2011). Kuteuliwa kwa tamthilia za mwandishi huyu katika ulingo wa uandishi na ushindi wa tuzo ni vitu vilivyoibua taharuki ya kutaka kujua mtindo uliomfaulisha hadi kiwango hiki. Pia, kwa kufanya huu utafiti tulionyesha jinsi nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo inavyoweza kuhakiki kazi zingine za tamthilia.

Tatu, kazi yoyote ya fasihi hulenga katika kupitisha ujumbe kwa hadhira. Tulichagua mada hii kwa sababu mtindo ni uti wa mgongo katika uelewekaji wa kazi ya fasihi kwa kuwa ni kigezo muhimu kinachosaidia katika kubeba ujumbe wa mtunzi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kazi ya fasihi hueleweka kwa kuchunguza lugha (Leech, 1969). Uchunguzi wa mtindo ni muhimu katika kuelezea kazi ya fasihi na ndiposa Mbatiah (2000) anasema kuwa tangu mwanzoni mwa karne hii (karne ya ishirini na moja) watunzi wa Kimagharibi na hasa Marekani wanatukuza mtindo katika kazi za fasihi na kuiweka dhamira daraja ya pili. Hii inafanya mtindo kuwa na umuhimu wa kushughulikiwa kwa kina.

1.8 Umuhimu wa Utafiti

Fasihi ni kioo cha jamii na ina dhima ya kuimulika na kuifafanua jamii katika mazingira yake ambapo msanii huandika kupitia kwa tajriba iliyopokezwa kwake katika jamii (Ndungo, 1983). Hii huwa na uwezekano tu iwapo kuna mtindo maalum uliotumika kutekeleza dhima ya kukuza maudhui yanayoigusa jamii finyu na ile pana kwa kutumia lugha kwa njia ya kipekee. Kwanza, msamiati wa fasihi ya Kiswahili unapokuzwa na kuhifadhiwa, lugha ya Kiswahili huimarika kwa kutoa misamiati mipya ambayo huboresha ukwasi wa lugha.

Pili, mtindo licha ya kubainisha kinachowasilishwa (ujumbe) pia hutekeleza jukumu la kuchunguza kinavyowasilishwa (lugha). Hii husaidia kueleza na kuweka wazi ujumbe wa mwandishi kwa njia mwafaka. Hili ndilo mtafiti amelitekeleza katika utafiti huu. Kwa kufanya hivi, utafiti huu unakuwa wa manufaa kwa kuwa umefungua njia ya kumwelewa mwandishi huyu haswa kwa wasomi wa matini za fasihi za mwandishi huyu.

Tatu, wasomi watafanikiwa katika usomi wao ikiwa wataelewa mtindo wa mwandishi huyu kwa kuwa mtindo ni uti wa mgongo katika ufunzaji na uelewekaji wa tamthilia. Vipengele vya mtindo vinapoeleweka inakuwa rahisi kuelewa dhamira na maudhui ya mwandishi kwa kuwa vinatekeleza dhima ya ujenzi wa dhamira na maudhui hayo (Njogu na Chimera, 1999).

Mwisho, katika utafiti huu tumeonyesha kuwa mbinu zinazomfaulisha mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake ndizo bora zaidi katika kazi ya fasihi. Hii inatokana na ukweli kuwa mbinu hizi husaidia katika kuelezea ujumbe wa mwandishi kwa mantiki. Kwa wale wanaotaka kuwa waandishi, utafiti huu ni wa manufaa kwani utawasaidia kuelewa umuhimu wa vipengele vya mtindo ambavyo vimechangia ari ya kuzisoma tamthilia hizi ili waweze kutunga zao kwa njia bora zaidi. Pia kwa wahakiki wa fasihi, utafiti huu utawafaa katika kuandika tafiti zao kwa ubora zaidi kwani utafiti wa leo ni msingi wa ule utakaofanywa kesho (Wafula, 1999).

1.9 Msingi wa Kinadharia

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ile ya Uhakiki wa Kimtindo. Nadharia ya Uhakiki wa

Kimtindo iliasisiwa na Buffon (1930). Kulingana na Buffon mtindo ni mtu mwenyewe. Hivi ni kusema kuwa ni ule upekee wa mtu katika matumizi yake ya lugha ili kuwasilisha ujumbe wake.

Mtindo ni dhana yenye utata kuieleza. Msokile (1993) kwa mfano anaifafanua kwa njia mbili. Kwanza, anasema ni namna ambavyo mwandishi ameipa sura kazi yake kifani na kimaudhui na kuitofautisha na nyingine inayoundwa na mtu mwingine. Aidha, anadai kwamba kile kinachoelezwa kinaweza pia kuitwa mtindo. Madai haya yanatiwa nguvu na Ngara (1982) aneyeelezea mtindo kuwa ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha; yaani ni jinsi msemaji awasilishavyo ujumbe wake.

Miongoni mwa waasisi muhimu wa nadharia hii ni Coombes (1953:10) akinukuliwa na Wambua (2001) aliyesema kwamba:

Mhakiki ni lazima azingatie vipengele vinavyofanya kazi fulani iwe ya kuvutia. Nia ya mtindo ni kuchunguza na kuchanganua lugha na kaida zake kwa nia ya kutambua mbinu zilizotengwa kwa kazi fulani ya kijamii, kufafanua sababu ya vipengele fulani kutumiwa na vingine kuachwa.

Kwa mujibu wa maelezo haya ni wazi kuwa nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo hujishughulisha na namna msanii alivyotumia lugha katika kuwasilisha ujumbe wake. Madai haya yanaungwa mkono na wataalamu wengi katika fasihi wakiwemo (Senkoro, 1982; Wamitila, 2013; na Mosha, 2002). Wataalamu hawa wanakubali kuwa maana ya kazi ya fasihi hujikita katika mtindo aliotumia mwandishi katika matini husika.

Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo huhusisha maelezo ya kiisimu ili kuweza kufafanua dhana zake za kimsingi katika fasihi. Maelezo ya Leech (1969) kuhusu uhusiano uliopo baina ya fasihi na isimu yanaonyesha kuwa dhana hizi zinakamilishana katika utendaji kazi. Anasema hivi:

Uhakiki wa Kimtindo hauhusiani tu na ufasiri wa maana za matini kwa mtazamo wa kiisimu. Nadharia hii kama taaluma haijisisimamii pweke bali huhusisha vipengele vya kifasihi na vile vya kiisimu katika uhakiki. Hii ni kwa sababu ya ugumu uliopo katika kuufafanua msamiati mpana wa kimsingi wa ki-

hakiki katika fasihi k.v. sitiari, taswira, kijembe, kinaya, usambamba na jazanda bila kurejelea dhana za kiisimu. Hivyo basi kwa kuziunganisha taaluma hizi mbili- ya fasihi na isimu kiutendaji, nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo inakuwa jukwaa la kushughulikia dhana za fasihi na isimu kwa pamoja. (uk. 2) (TY)

Kimsingi, Leech anaashiria kuwa uhakiki wa mtindo huhusu kuchanganua vipengele vya fasihi na pia vile vya isimu. Hakuna kipengele mojawapo kati ya fasihi na isimu ambacho kinaweza kusimama pweke na kujifafanua kikamilifu. Hii ni ishara kwamba nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo hutumia maelezo ya isimu na fasihi katika kufafanua matini mbalimbali. Hii ina maana kuwa kila tunapohakiki mtindo katika mkabala wa kifasihi hatuwezi kupuuza matumizi ya vipengele vya kiisimu pia. Nadharia hii basi hujihusisha na uchunguzi wa kinachosemwa (ujumbe) na kinavyosemwa (mtindo). Indangasi (1988) anaunga mkono maelezo ya Leech anaposema kuwa nadharia hii hujihusisha na jinsi lugha ilivyotumika kuleta mvuto kisanaa. Mhimili huu ulitufaa katika kuchanganua mbinu za usimulizi na kuonyesha mchango wao kwenye tamthilia zilizoteuliwa.

Leech, anaeleza kuwa lengo la nadharia ya mtindo ni kuchunguza lugha na kanuni zake ili kubainisha mbinu zilizotengewa kazi fulani ya kijamii. Leech anaonekana kusesitiza kuwa nadharia ya mtindo hudhamiria kufanikisha uchunguzi wa kina wa matumizi ya lugha katika fasihi. Mhimili ya nadharia hii ni pamoja na; kwanza mtindo wa kazi ya fasihi ndio hutumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe wake. Mhimili huu ulitumiwa kufafanulia mitindo ya uandishi katika tamthilia teule.

Pili, upo uwiano baina ya ujumbe na lugha katika kazi ya kifasihi na vipengele hivi viwili haviwezi kutenganishwa. Tatu, Lugha ndicho chombo tekelezi kinachosaidia kuelewa ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi. Maoni haya yanaungwa mkono na Tunner (1973) anaposema kuwa uteuzi wa maneno si huru na msanii hulazimika kuwa makini ili kazi yake ikubalike na walengwa au hadhira yake. Mhimili hii miwili ilitusaidia kuangalia namna vipengele vya mtindo vinavyosaidia na kuathiri uelewekaji wa maudhui. Nne, mwandishi hutumia lugha kiufundi na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya kisanaa katika kazi yake. Maoni ambayo yanaungwa mkono na Simpson (2004) anayedai kuwa nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo husisitiza wazo kuwa kila kazi ya fasihi ina ubunifu fulani ambao unapochanganuliwa kwa undani husaidia uelewekaji

wa undani wa matini za fasihi. Pamoja na maoni haya, ni yale ya Chapman (1982) anayeelekea kuafikiana na Leech kuhusu jambo hili anapodai kuwa fasihi haiwezi kujadiliwa pasipo kuzingatia kwamba ina matumizi maalum ya lugha. Mhimili huu uliwezesha utafiti huu kuchanganua tamathali za usemi zilizotumika katika tamthilia teule.

Leech na Short (1981) wameainisha viwango vya kushughulikiwa katika mtazamo wa kifasihi na ambao mtafiti ameegemea katika utafiti huu. Hivi ndivyo viwango ambavyo mhakiki anayechukua mkabala wa kifasihi huweza kushughulikia. Kwanza, ni kiwango cha kileksika ambapo aina mbalimbali za maneno huchunguzwa k.v. nomino, vivumishi, vitenzi, vielezi n.k. Pili, ni kiwango cha kisarufi ambapo aina za sentensi, uchangamano wa sentensi, aina za virai kama virai nomino, virai vitenzi n.k. hushughulikiwa. Tatu, ni kiwango cha semantiki ambapo tamathali za usemi k.v. jazanda, chuku, takriri, tashbihi n.k. hushughulikiwa. Leech (1969) anatumia anatumia istilahi *tropes* kurejelea kiwango hiki. Nne, ni mshikamano na mwingiliano wa kimuktadha ambamo dhana za kimtindo huchunguzwa katika mwingiliano wao. Mtafiti alihusisha kiwango cha pili, tatu na nne katika utafiti huu. Kiwango cha pili na tatu vilimsaidia mtafiti kuhakiki mbinu za usimulizi na vilevile kuonyesha mchango wa tamathali za usemi kwenye ufahamu wa ujumbe katika tamthilia tatu za Arege. Kiwango cha nne kilimwongoza mtafiti kuchunguza jinsi vipengele mbalimbali vya mtindo vinavyoingiliana ili kujenga mtindo katika tamthilia zilizoteuliwa.

Wamitila (2008) akijalizia maelezo ya Leech na Short (keshatajwa) anafafanua vipengele vya kimsingi ambavyo huchunguzwa katika kazi ya fasihi kwa mwelekeo wa nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Vipengele anavyotaja ni: tamathali, uteuzi, sarufi, muwala, mshikamano, mazungumzo na mbinu za uwasilishaji mawazo huku akivihusisha vyote na mtindo. Vipengele vilivyofaidi utafiti huu ni: tamathali, sarufi na mbinu za uwasilishaji usemi (maudhui).

Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na mwanamitindo Leech (1969), mihimili ya nadharia hii ilitusaidia kuchunguza mtindo wa tamthilia teule za Arege pamoja na kufikia malengo ya utafiti huu. Kwa jumla, utafiti huu ulitumia vipengele vilivyofafanuliwa na

wanamitindo tuliowataja hapo juu kwa kuwa wametoa mchango ulioimarisha uelewaji wa nadharia ya utafiti huu. Vipengele hivyo viliusaidia utafiti wetu kwa kuuwekea msingi madhubuti na kuupa mwelekeo uliouchukua katika kufikia lengo kuu la kuelezea na kufafanua mtindo katika tamthilia teule.

1.10 Mapitio ya Maandishi

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu fasihi ya Kiswahili. Suala la mtindo limeshughulikiwa kwa wingi japo kwa namna tofautitofauti. Chacha (1980) amehakiki ushairi wa Abdilatif katika kiwango cha maudhui, akizingatia *Sauti ya Dhiki* na *utenzi wa Adamu na Hawa*. Chacha (1980) alitumia mtazamo wa kimaksi katika kazi yake. Utafiti wake ulilenga kuibua maudhui, hata hivyo aliishilia kuhakiki vipengele mbalimbali vya mtindo kwa sababu ni vigumu kutenganisha mtindo na maudhui (Masinde, 1992). Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa umeshughulikia mtindo katika tamthilia teule. Hata hivyo utafiti wake ulitufaa katika maelezo ya mtindo na vipengele vyake.

Utafiti mwingine unaokaribiana na wa Chacha ni wake Kitsao (1982) ambaye alijadili maudhui mbalimbali yapatikanayo katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Alizihakiki riwaya fulani akitumia uchambuzi wa kitarakimu. Kitsao alionyesha kuwa kila mwandishi huwa na mtindo ambao anaweza kunasibishwa nao. Utafiti wake unatofautiana na huu wetu kwa kuwa ulishughulikia maudhui katika riwaya ilhali huu umeshughulikia mtindo katika tamthilia. Hata hivyo, utafiti wa Chacha ulitufaidi kwa maelezo ya mtindo na vilevile kubainisha ubingwa wa mtindo katika kupitisha ujumbe wa mwandishi.

Senkoro (1988) kwa upande mwingine alihakiki maudhui na mtindo katika mashairi ya watunzi mbalimbali akiongozwa na nadharia ya Umaksi. Katika utafiti wake, Senkoro (keshatajwa) ameshughulikia maudhui tofautitofauti pamoja na vipengele mbalimbali vya kimtindo na kuonyesha jinsi mtindo unavyosaidia kuwasilisha mawazo ya msanii. Aidha, kupitia utafiti wake ameonyesha kuwa mtindo ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha kwa ubunifu. Utafiti wake japo umeshughulikia kipera tofauti umetusaidia kuelewa vipengele vya lugha kwani ndivyo tunalenga kuvichambua. Tofauti ni kuwa huu umejikita katika tamthilia tatu teule za mwandishi mmoja na pia ametumia nadharia ya Umaksi kinyume na wetu ambao umetumia ile ya Uhakiki wa Kimtindo.

Utafiti kuhusu ufundi katika riwaya za Mohamed Said Abdullah ulifanywa na Kamau (1992). Baadhi ya mbinu alizochunguza ni: takriri, mazungumzo, tashbihi, na tanakali za sauti. Kamau ameonyesha kuwa mbinu za kimtindo ndizo zilizomsaidia mtunzi huyu kutoa ujumbe wake kwa nguvu na hivyo kumtambulisha. Utafiti huu unakaribiana na wake kwa kuwa unahusu pia mbinu za kimtindo na tena zile tu zinazojitokeza kwa uwazi katika tamthilia zote. Tofauti ni kuwa utafiti huu unahusu utanzu wa tamthilia wala si riwaya na vilevile utafiti wetu umeshughulikia vipengele hivi kwa mkabala wa kukuza maudhui. Hata hivyo utafiti huu ulifaidi kutoka kwa utafiti wake kwa maelezo kuhusu maana ya nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo na vipengele vya kimtindo alivyovishughulikia kwani tumehusisha baadhi yavyo.

Kwa upande mwingine Masinde (1992) alihakiki dhamira na mtindo katika mashairi huru ya watunzi kutoka Tanzania akiongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Kwa kuhakiki mashairi mbalimbali amethibitisha wazo kuwa mtindo hufanya hadhira ihisi tajriba, mtazamo, na mwelekeo wa mtunzi kuhusu swala analolishughulikia. Utafiti wake ulithibitisha kuwa mtindo anaoutumia mtunzi katika kutoa ujumbe ni vipengele vinavyotegemeana. Utafiti wake ulikuwa muhimu kwa huu kwa kuwa ulituelekeza kuhusu matumizi ya nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo na vipengele vya kimtindo. Hata hivyo utafiti huu ni tofauti na wake kwa njia mbili. Kwanza, utafiti huu ulijikita katika tamthilia tatu za mwandishi mmoja kutoka Kenya ilhali wake ulijikita katika mashairi ya watunzi watatu kutoka Tanzania (Kezilahabi, Kahigi na Mulokozi). Pili, utafiti wake ulishughulikia dhamira na mtindo ilhali huu umeshughulikia vipengele vya mtindo na kuvihakiki kwa namna vinavyoathiri uelewakaji wa maudhui.

Utafiti wa Ntiba (2011) ulishughulikia athari ya dhamira katika uteuzi wa mtindo katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Ntiba amejadili maswala wanayoyashughulikia waandishi katika hadithi fupi zilizoandikwa mwaka wa 2007. Amechunguza dhamira za hizi hadithi fupi na namna zinavyoathiri uteuzi wa mitindo wanayotumia kuziwasilisha na mwisho aliangazia jinsi mazingira huathiri utunzi. Ntiba aliongozwa na nadharia mseto: ya Saikolojia na ile ya Mtindo. Utafiti wake umeonyesha kuwa dhamira huathiri mtindo wa mwandishi. Utafiti wake ni wa manufaa kwa kuwa uliupa utafiti huu msingi wa kuelewa maana ya mtindo na vijenzi vyake. Aidha ulitusaidia kujua athari ya mtindo kwa dhamira

kwa kuwa tuligusia dhamira tulipokuwa tukijadili maudhui yanayojitokeza katika tamthilia teule za Arege. Hata hivyo, unatofautiana na wetu kwa njia kadha. Kwanza, utafiti wetu ulijihusisha na mtindo unaojitokeza katika tamthilia teule na jinsi unavyoathiri maudhui yanayosukwa na mwandishi mmoja ilhali yeye alishughulikia namna dhamira huathiri mtindo unaotumika katika hadithi fupi za waandishi tofauti. Utafiti huu umejikita katika nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo ilhali wake umejikita katika nadharia mseto, ya Saikolojia na Kimtindo. Utafiti umelenga kuonyesha kuwa mtindo ndio unaoamua ujumbe ilhali Ntiba ameonyesha kuwa dhamira ndiyo huamua mtindo.

Mtindo katika hadithi fupi na riwaya za Clara Momanyi ni utafiti ulioshughulikiwa na Onchangu (2013). Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Elimu-Mitindo. Yeye alihakiki mtindo katika mkabala ukiushi wa kisintaksia na rejesta ambapo ameonyesha athari ya ukiushi wa maneno kwenye maudhui anayokuza mwandishi katika kazi yake. Pia ameshughulikia vipengele vya kimtindo na kuonyesha jinsi vipengele hivi huleta ujumi katika kazi nzima. Utafiti wake umetufaa sana kwani umeshughulikia kazi zilizoandikwa na mwandishi mmoja sawia na huu wetu. Tofauti ni kuwa utafiti wake umeshughulikia mawanda mawili ya fasihi: hadithi fupi na riwaya ilhali huu umejikita katika tamthilia pekee. Pia utafiti wake umezama katika kitengo cha sintaksia kwa upande wa ukiushi wa maneno ilhali wetu umezama katika kategoria za uwasilishaji wa mawazo, kisarufi na tamathali (semantiki).

Utafiti wa Kilanga (2014) ulijihusisha na uchunguzi wa ishara katika tamthilia za *Kaptula la Marx* ya Kezilahabi na *Kijiba cha Moyo* ya Arege akiongozwa na nadharia ya Semiotiki. Mtafiti alionyesha umuhimu wa nadharia ya Semiotiki katika kuondoa utata na kusaidia ufahamu wa ishara mbalimbali katika tamthilia zilizoteuliwa. Pia amegusia maelezo ya tamathali za usemi ambayo ni muhimu kwa utafiti huu. Utafiti wake ni muhimu kwa utafiti huu kwani *Kijiba cha Moyo* ni mojawapo wa tamthilia ambazo tumezishughulikia. Tofauti ni kwamba Kilanga (keshatajwa) ameshughulikia tamthilia mbili za waandishi tofauti ilhali huu umetumia tamthilia tatu za mwandishi mmoja. Tena, utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Semiotiki kwa kipengele cha ishara huku wetu ukiongozwa na ile ya Uihakiki wa Kimtindo kwa kipengele cha lugha. Utafiti wake

umeshughulikia kipengele kimoja cha mtindo ilhali wetu umehusisha vipengele vingi vya kimtindo.

Utafiti wa uhalisia wa mtindo wa mwandishi Ken Walibora katika fasihi ya watoto ni wake (Kairu, 2011). Kairu ameshughulikia ufaafu wa mtindo wa mwandishi huyo katika fasihi ya watoto akiongozwa na nadharia mseto ya Mtindo, Maadili na Uhalisia. Katika utafiti wake ameonyesha kuwa pana uhusiano mkubwa kati ya kinachowasilishwa (ujumbe) na namna kinavyowasilishwa (mtindo) na wapokezi wake. Yeye ameonyesha kuwa hadhira inayoandikiwa kazi huathiri mtindo anaoutumia mwandishi. Utafiti wake ulitufaa kwa kutufafanulia dhana ya mtindo na vijenzi vyake. Tofauti ni kwamba, katika utafiti huu tulidhamiria kudhihirisha mtindo unaojitokeza katika tamthilia za mwandishi Timothy Arege. Hata hivyo, maelezo yake kuhusu mtindo yameupa msingi utafiti huu.

Naye Ileri (2011) amechunguza tamthilia kama utendi kwa kurejelea tamthilia ya *Kinjeketile* ya Ebrahim Hussein na *Mzalendo Kimathi* iliyotungwa na Ngugi wa Thiong'o na Micere Mugo. Alichunguza jinsi utendi unavyotumika kuchanganulia tamthilia za Kiswahili. Aidha, amedhihirisha jinsi utendi unavyotumiwa kusawiri wahusika, ujumbe, na lugha na hatimaye kuonyesha kwamba watunzi wa tamthilia wanatumia utendi kama mtindo. Utafiti wetu ni tofauti kwa kuwa umechunguza mtindo katika tamthilia za mtunzi mmoja. Aidha, unahusu vipengele vingi vya kimtindo tofauti na wa Ileri (keshatajwa) ambao ulijikita katika utendi pekee. Pili, utafiti wa Ileri (2011) uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini ilhali huu umeongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Hata hivyo, madhali ushairi ni mojawapo ya mbinu za kimtindo, utafiti wake uliwekea msingi utafiti huu.

Utafiti wa Wakesho (2011) umejadili matumizi ya masimulizi na malumbano katika tamthilia za *Wingu Jeusi* (1987) na *Pango* (2003) ukiongozwa na nadharia mseto za Uhakiki wa Kimtindo na Mwingilianomatini. Anaeleza jinsi fasihi simulizi inavyoathiri tamthilia ya Kiswahili katika kutumia masimulizi na malumbano kama mtindo. Utafiti wa Wakesho ulituwezesha kuelewa baadhi ya vijenzi vya mtindo, matumizi ya lugha na maudhui maadamu haya ni baadhi ya mambo ambayo tuliyashughulikia katika utafiti wetu. Licha ya hayo, utafiti huu unatofautiana na utafiti wake kwa kuwa alichunguza

vijisehemu vya mtindo kutoka tamthilia za waandishi ilhali huu ulitumia vijisehemu hivyo na vingine kuelezea mtindo kama unavyokuza ujumbe wa mwandishi katika tamthilia za Arege. Pia utafiti wake uliongozwa na nadharia mseto za Mwingilianomatini tofauti na huu ambao umeongozwa na nadharia moja ya Uhakiki wa Kimtindo pekee.

Mabadiliko ya kimtindo katika mashairi ya S. A. Mohamed yameshughulikiwa na Ngolo (2011) akirejelea diwani tatu za mwandishi huyu. Ngolo alichunguza mtindo katika diwani hizi: *Sikate Tamaa* (1980), *Kina cha Maisha* (1984) na *Jicho la Ndani* (2002) akiongozwa na nadharia ya Utanzu. Ili kuainisha haya mabadiliko kimtindo, ametumia vigezo vya maudhui, muundo na matumizi ya lugha. Ngolo amebaini kuwa mabadiliko ya kimtindo katika mashairi yamechangiwa na mazingira yaliyomkuza mwandishi huyu. Utafiti wa Ngolo (keshatajwa) umekuwa wa manufaa kwetu kwani umetuongoza kwa upande wa vipengele vya kimtindo. Aidha, ameshughulikia diwani tatu za ushairi zilizoandikwa na mwandishi mmoja sawia na idadi ya tamthilia tulizohusisha katika utafiti wetu. Isitoshe, inasadifu kuwa zimeandikwa na mwandishi mmoja (S.A. Mohamed) sawa na zetu zilizoandikwa na Arege. Kazi hii imetufaa basi kwa upande wa mwelekeo au mtazamo wa uhakiki wetu. Hata hivyo kuna tofauti kati ya utafiti wa Ngolo na wetu. Kwanza, yeye ameshughulikia ushairi akitumia nadharia ya Utanzu ilhali sisi tumeshughulikia tamthilia tukiongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Pili, Ngolo amechunguza mabadiliko ya kimtindo ilhali utafiti huu umechanganua mtindo kama unavyojitokeza katika tamthilia za Arege kwa madhumuni ya kuonyesha ubingwa wake katika kufafanua maudhui.

Utafiti mwingine unaokaribiana na wa Ngolo ni wa Bakari (2011) ambaye ametafitia usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-Adamu* (2002) na mkusanyiko wa hadithi fupi wa *Sadiki Ukipenda* (2002) akiongozwa na nadharia ya Usemezano. Amejadili historia fupi ya uandishi wa waandishi S. A. Mohamed na Wamitila na kuonyesha jinsi walivyobadilisha mtindo wa uandishi kutoka uhalisia hadi uhalisia ajabu. Utafiti wake ulidhihirisha kwamba waandishi hawa walilazimika kubadili uandishi wao ili kuelezea hoja zao kwa uwazi zaidi katika hali zinazobadilikabadilika. Ngolo alirejelea vipengele mbalimbali vya kimtindo katika kufikia kuelezea mabadiliko haya. Utafiti wake ulitufaa kwa kutuelekeza kutambua

vijenzi mbalimbali vya mtindo. Utafiti wake unatofautiana na huu kwa kuwa sisi tumeongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo kuhakiki kazi za Arege kwa lengo la kubainisha umaarufu wa mtindo ilhali utafiti wa Bakari (keshatajwa) uliongozwa na nadharia ya Usemezano katika kubainisha mabadiliko ya mtindo wa uandishi. Pia utafiti wake ulihusisha riwaya na hadithi fupi za waandishi tofauti ilhali huu umehusisha tamthilia tatu za mwandishi mmoja.

Too (2011) alichunguza baadhi ya fani katika tamthilia ya *Nguzo Mama* ya Penina Muhando. Utafiti wake uliongozwa na nadharia mseto ambazo ni Umuundo na ile ya Semiotiki. Katika utafiti wake, Too amechanganua mbinu anuwai za lugha kama zilivyojitokeza katika tamthilia teule. Mbinu alizochanganua ni pamoja na tamathali za usemi na mbinu nyingine za lugha akionyesha jinsi zinavyosawiri sifa za mwanamke katika jamii. Too amebaini kuwa lugha iliyotumiwa na mwandishi wa tamthilia hii inamkweza na kumzusha mwanamke kwa njia ya uhalisia. Ingawa utafiti wa Too (keshatajwa) unagusia kwa ujumla baadhi ya vipengele vya kimtindo ambavyo tumevishughulikia, utafiti huu umelenga tamthilia tatu za Arege ambapo vipengele hivi vimetumika katika kubainisha mtindo. Tofauti ni kuwa yeye alitumia nadharia mseto, ya Umuundo na Semiotiki ambazo zina mtizamo tofauti ilhali wetu uliongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo.

Utafiti wa nyimbo umeshughulikiwa na Wambua (2000) na Kasau (2013) mtawalia. Wambua alitafitia mtindo katika nyimbo za Kakai Kilonzo na kuonyesha jinsi mwimbaji huyu alivyoteua maneno na mbinu alizotumia kuwasilisha maudhui yake akiongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Wambua amebaini kwamba uelewekaji na ukubalifu wa maudhui yanayowasilishwa hutegemea mtindo uliotumika. Utafiti wake unakaribiana kwa kiasi kikubwa na utafiti huu kwani ulituwekea msingi wa kuelewa nadharia na maana ya mtindo pamoja na vipengele vya mtindo. Tofauti kati ya utafiti wake na huu ni kuwa tumeshughulikia mtindo katika tamthilia za Arege ilhali Wambua alijishughulisha na nyimbo. Naye Kasau (keshatajwa) amehakiki maudhui na matumizi ya lugha katika nyimbo za injili za Rose Muhando akiongozwa na nadharia za Uhakiki wa Kimtindo na Uadilifu tofauti na huu ambao ulijikita kwenye tamthilia tukiongozwa na nadharia

Uhakiki wa Kimtindo. Hata hivyo watafiti hawa wamebainisha kuwa mtindo ndio msingi wa uelewekaji wa maudhui.

Wathome (2009) ameshughulikia mitindo katika nyimbo za tohara za jamii ya Wakamba wa Masaku, tarafa ya Kati akiongozwa na nadharia mseto za Ethnografia na ya Kimtindo. Yeye amejihusisha na mabadiliko ya kimtindo katika nyimbo za tohara. Katika utafiti wake amejadili vipengele mbalimbali vya kimtindo hasa tamathali katika nyimbo teule. Licha ya utafiti huu kuwa wa fasihi simulizi umetufaa kwa kutufafanulia maana, aina ya mitindo na vijenzi vya kimtindo kwani kuna ukuruba mkubwa kati ya fasihi simulizi na ile andishi. Tofauti ni kwamba katika utafiti wetu tumechunguza mtindo wa tamthilia ilhali wake ulijikita katika nyimbo. Pia utafiti wake uliongozwa na nadharia mbili tofauti na huu ambao uliongozwa na nadharia moja tu: Uhakiki wa Kimtindo.

Tahakiki ya tamthilia *Mstahiki Meya* imeandikwa na King'ei (2012). Kwenye tahakiki hii, Kinge'i ameelezea muhtasari wa maonyesho, uhusika, maudhui, dhamira, na mtindo wa tamthilia ya tamthilia *Mstahiki Meya*. Hata hivyo, tahakiki yake ni ya kijumla na inalenga kuwaongoza watahiniwa wa shule za upili kujiandaa kwa mitihani ya fasihi madhali tamthilia hii ni mojawapo ya vitabu teule. Katika tahakiki yake King'ei (keshatajwa) hajaonyesha jinsi mbinu za lugha zinavyochangia kubainisha mtindo wa mwandishi huyu. Licha ya hayo, mwongozo wake ulitufaa kwa kuwa *Mstahiki Meya* ni mojawapo ya kazi za Arege tulizoshughulikia katika utafiti wetu.

Okwena (2013) ametafitia matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu teule za Arege. Amechanganua aina mbalimbali za jazanda alizotumia mwandishi huyu kuwasilisha ujumbe wake. Ameeleza kuwa upo uhusiano baina ya lugha ya kijazanda anayotumia mwandishi na ujumbe unaowasilishwa kwenye tamthilia hizo huku akiainisha jazanda mbalimbali. Naye Wekesa (2008) ameshughulikia matumizi ya taswira katika ushairi huru wa Kiswahili. Ameonyesha kuwa taswira husaidia katika kuelewa maudhui ya mashairi haya kama alivyofanya Okwena (keshatajwa) katika kufafanua jazanda. Wote wana mtazamo sawa tofauti ikiwa katika kipera wanachoshughulikia. Kwa mantiki hiyo, utafiti wa Okwena (keshatajwa) umeupa huu msingi kwani umelenga kuangalia mbinu za kimtindo katika tamthilia teule na utafiti wa Wekesa (keshatajwa) umetusaidia kuelewa

maelezo ya taswira. Jazanda ni kipengele kimoja tu cha mtindo kama ilivyo taswira. Utafiti huu ni tofauti kwani umehakiki vipengele vingi vya kimtindo katika tamthilia teule za Arege ambavyo vimesaidia kuonyesha mtindo katika tamthilia teule licha ya kusaidia kuelewa maudhui yaliyokuzwa.

Naye Mwita (1994) amehakiki mbinu za sanaa zilizotumiwa kusuka maudhui ya tamthilia mbili za Ebrahim Hussein: *Arusi na Ukingo wa Tim*. Mwita amechambua mbinu hizi katika muktadha wa maudhui yanayowasilishwa katika tamthilia hizi akiongozwa na Nadharia ya Mtindo. Yeye anaonekana kuyapa maudhui uzito katika maelezo ya tasnifu yake. Hata hivyo utafiti wake uliupa msingi huu wetu kwa kuwa tulifaidi na maelezo ya Nadharia ya Mtindo na vilevile vipengele vya kimtindo. Hata hivyo tofauti iliyopo ni kuwa yeye alishughulikia tamthilia mbili za Hussein ilhali sisi tumeshughulikia tatu za Arege. Licha ya tofauti hizi, utafiti wetu umetilia mkazo mtindo kama nguzo inayoamua jinsi maudhui yanavyoeleweka.

Mwanakombo (1994) amehusisha falsafa na dhamira katika uhakiki wake wa mtindo katika tamthilia za Chacha N. C. akionyesha namna zinavyoathiri mitindo ya mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wake. Mwanakombo (keshatajwa) alitathmini athari ya falsafa na dhamira kwa mtindo ilhali utafiti huu umeshughulikia vipengele vya mtindo na athari yao kwenye maudhui katika tamthilia teule. Utafiti huu kimsingi umeshughulika mtindo kama kipengele muhimu kinachoamua uelewekaji wa maudhui.

Mtindo katika hadithi fupi umeshughulikiwa na Ongarora (2007) na Katutu (2013). Ongarora (2007) alishughulikia *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* huku Katutu (2013) akishughulikia *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Wawili hawa wameshughulikia mtindo kama matumizi ya lugha ila Katutu amezama katika kuonyesha jinsi mtindo unavyosaidia katika uwasilishaji wa ujumbe. Watafiti hawa wameongozwa na nadharia ya Kimtindo katika tafiti zao sawia na utafiti huu. Tofauti ni kuwa katika tafiti zao walishughulikia kipera cha hadithi fupi ilhali sisi tumeshughulikia tamthilia. Hata hivyo tafiti zao zimetusaidia katika maelezo ya maana ya mtindo na vipengele vyake na jinsi vinavyosaidia kukuza maudhui.

Utafiti uliochanganua matumizi ya takriri na sitiari katika *Utenzi wa Rasil' lghuli* kwa kurejelea nadharia ya Umuundo ni wa Ndumbu (2013). Katika utafiti wake, ameelezea aina mbalimbali za takriri na sitiari pamoja na umuhimu wao katika kuwasilishia ujumbe wa utenzi teule. Katika utafiti wake imebainika kuwa sitiari na takriri ni vipengele vya mtindo ambavyo hupendelewa na waandishi kwa kuwa husaidia kuelezea ujumbe kwa mnato zaidi licha ya kuufumba. Utafiti wake umeufaa huu kwa kuwa hivi ni baadhi ya vipengele ambavyo tumevishughulikia. Hata hivyo, utafiti wake Ndumbu (keshatajwa) unatofautiana na huu wetu kwa kuwa yeye ametumia nadharia ya Umuundo ilhali sisi tumetumia nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Tofauti nyingine ni kuwa utafiti wake umejihusisha na utenzi ilhali wetu umejikita katika tamthilia teule.

Nadharia ya Umitindo ilimwongoza Lugwiri (2011) kutafitia sitiari, ishara na tashbihi katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*. Lugwiri ameonyesha kuwa vipengele hivyo vitatu vilisaidia kuelezea dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*. Kinachobainika kutokana na utafiti wa Lugwiri (keshatajwa) ni kwamba mtindo ndicho kigezo muhimu zaidi katika kuyaeleza na kuyaelewa maudhui katika fasihi. Utafiti wake una manufaa kwa huu licha ya yeye kushughulikia utenzi huku mtafiti akijikita katika tamthilia. Tashbihi na sitiari ni baadhi ya vipengele ambavyo tumevishughulikia katika Lugwiri alitumia nadharia ya Umitindo ambayo pia sisi tumeitumia na hivyo basi utafiti wake umetusaidia kupata mwangaza wa mielekeo ya nadharia hii.

Murumba (2013) naye ameshughulikia mtindo katika riwaya ya *Watu wa Gehenna* akiongozwa na nadharia ya mseto za Umitindo na Uhalisiajabu. Katika utafiti wake amechunguza wahusika na uhusika, ukiushi wa kisemantiki, mandhari na usimulizi. Tumefaidi na utafiti wake kwa viwango viwili ambavyo ni; chimbuko na maana ya nadharia ya Umitindo na pia ukiushi wa kisemantiki (tamathali za usemi). Hata hivyo utafiti wake unatofautiana na huu wetu kwa njia mbili: Murumba (keshatajwa) aliongozwa na nadharia mseto za Umitindo na Uhalisiajabu ilhali huu umeongozwa na Uhakiki wa Kimtindo.

Kwa upande mwingine, Fadhili (2014) amechunguza dhima ya mtindo katika tamthilia za kihistoria. Fadhili amelinganisha tamthilia ya Morani na Kinjekitile kwa mkabala wa

vipengele vya lugha na maudhui ili kudhuihirisha suala la kihistoria katika tamthilia hizi mbili. Katika utafiti wake ameongozwa na nadharia ya Elimu-mitindo ambapo amejadili namna waandishi wa tamthilia husika walivyoelezea swali la kihistoria katika tamthilia zao huku kila mmoja akitumia vipengele mbalimbali vinavyombainisha katika upekee wake. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa kila mwandishi ana upekee unaojitokeza katika matumizi yake ya lugha na hivyo kumpambanua. Utafiti wake Fadhili (keshatajwa) una mchango mkubwa kwa huu wetu kwa njia zifuatazo: Kwanza, alishughulikia dhima ya vipengele vya kimtindo sawia na huu. Pili amejikita katika tamthilia kama utafiti huu ulivyofanya. Japo hali ni hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwani ameshughulikia tamthilia mbili za waandishi tofauti huku akiegemea misingi ya kihistoria ilhali utafiti wetu umeshughulikia tamthilia tatu za mwandishi mmoja katika karne ya ishirini na moja kwa lengo la kubainisha usanii wake.

Nadharia za Uhalisia na Umitindo zilimwongoza Muthoni (2014) kuhakiki mtindo na maudhui katika riwaya ya *Tikitimaji* ya Wamitila. Muthoni (keshatajwa) amechunguza maudhui na matumizi ya lugha katika riwaya hii na kubainisha kuwa ujumbe wa mwandishi hueleweka kwa utegemezi wa mbinu za lugha alizotumia. Utafiti wa Muthoni umefaidi huu wetu pakubwa. Yeye amehakiki vipengele vya kimtindo ambavyo vimetupa mwanga wa maelezo yanayofaa kwa utafiti huu pamoja na ufafanuzi wa dhana ya umitindo. Hata hivyo kuna tofauti za kimsingi kati ya utafiti huu na wake. Kwanza, utafiti huu ulijikita katika tamthilia tatu za mwandishi mmoja ilhali wake ulijikita katika riwaya moja tu. Pili, utafiti wa Muthoni umeshughulikia sana maudhui na mtindo ilhali huu umejikita katika mtindo pekee. Tatu, utafiti wa Muthoni (keshatajwa) umehusisha nadharia mbili ilhali huu umetumia nadharia moja.

Nyaga (2013) amehakiki mtindo katika mashairi ya Diwani ya karne mpya. Aliongozwa na nadharia ya Mtindo katika utafiti wake. Nyaga (keshatajwa) ameshughulikia vipengele vya mtindo katika mashairi teule pamoja na athari ya vipengele hivi kwa ujumbe wa waandishi wa mashairi yenyewe. Utafiti wake umetalii maumbo ya mashairi na athari ya maumbo hayo kwenye ujumbe na kubaini kuwa athari ya mitindo ya kifasihi hubainika pia katika maumbo yenyewe. Utafiti wetu ulinufaika kwa maelezo ya nadharia ya mtindo na vipengele vya mtindo. Tofauti ni kuwa Nyaga alijihusisha na mashairi kutoka diwani

moja yaliyoandikwa na waandishi tofautitofauti ilhali huu umeshughulikia tamthilia zilizoandikwa na mwandishi mmoja.

Nadharia ya Umuundo imetumiwa kuchanganua fani katika hadithi za Kiswahili na Oyoyo (2013). Amefafanua na kueleza maswala ya kifani kama muundo, wahusika, msuko na matumizi ya lugha na kuonyesha jinsi hadithi hizi tano zilivyotumia lugha kwa ufanisi wa kusafirisha ujumbe. Utafiti wake umechunguza vipengele vya fani vingi bila kuvizamia. Hata hivyo katika utafiti wake imebainika kuwa lugha ndicho kigezo cha kimsingi cha kufafanua vipengele vya fani. Utafiti wake licha ya kuwa ni wa fasihi simulizi ulifaidi wetu kwani tulipata maelezo mwafaka kuhusu vipengele vya kimtindo vilivyotumika pale kwani ndivyo utafiti huu ulikuwa umejikita katika kuvitafitia. Tofauti ni kuwa utafiti wa Oyoyo (keshatajwa) ulijikita katika kipengele cha fasihi simulizi cha hadithi ilhali huu umeshughulikia kipengele cha fasihi andishi cha tamthilia. Pia utafiti wa Oyoyo (keshatajwa) uliongozwa na nadharia ya Umuundo ilhali wetu umeongozwa na nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo.

Maoni haya yaliyotolewa na wataalamu na wahakiki mbalimbali katika tafiti zao yaliupa utafiti wetu maelezo kuhusu nadharia ya mtindo na vipengele mbalimbali vya kimtindo. Maoni yao yaliusukuma utafiti huu mbele hadi kiwango cha kukamilika kwa kuupatia maelezo kuhusu vipengele mbalimbali vya mtindo. Kwa hivyo umuhimu wao huwezi kupuuzwa. Kwa mantiki hii, utafiti huu ulitalii kwa kina matumizi ya mtindo katika uwasilishaji wa ujumbe wa mwandishi katika tamthilia ili kuziba baadhi ya mapengo katika tafiti za awali na kuweka msingi thabiti kwenye tafiti za baadaye.

1.11 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imetoa ufafanuzi kuhusu muundo wa utafiti ambao ulifuatwa katika utafiti wetu. Maelezo kuhusu eneo la utafiti, idadi lengwa, na uteuzi wa sampuli pia umetolewa. Ufafanuzi wa njia za ukusanyaji data, mbinu za uchanganuzi pamoja na uwasilishaji umeelezwa kwa kina.

1.11.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa kimaelezo ulitumika katika kushughulikia utafiti ili kuafikia malengo yake

matatu. Data tuliyochanganua ilitokana na usomaji na uhakiki wa vitabu na machapisho mbalimbali, zikiwemo tamthilia zilizoteuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Muundo huu ulituwezesha kuainisha, kuchanganua na kufasiri data iliyokusanywa ili kufikia malengo yetu.

1.11.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ni wa kifasihi na ulijihusisha na utanzu wa tamthilia. Tamthilia zilizoteuliwa ni za Kiswahili na ambazo zimechapishwa baina ya mwaka 2007 na 2009. Tamthilia teule zilisomwa na vipengele vya kimtindo kuchanganuliwa ili kuvibainisha na kutathmini mchango wao katika uwasilishaji wa maudhui. Eneo la utafiti huu ni maktabani na sababu za kuchagua eneo hili ni upatikanaji wa maandishi mengi yaliyorejelewa katika utafiti ili malengo yake yaafikiwe.

1.11.3 Idadi Lengwa

Tamthilia tatu zilizoteuliwa ni za mwandishi mmoja. Kufikia mwaka wa 2013, kazi za Arege zilizochapishwa katika utanzu wa tamthilia ni tatu nazo ni: *Chamchela* (2007), *Mstahiki Meya* (2009) na *Kijiba cha Moyo* (2009). Tamthilia hizi zilifaa kutimiza malengo yetu kwani zimesheheni vipengele vya kimtindo katika mkabala wa lugha ambavyo vilitumika katika utafiti huu na zilichaguliwa kutoka kwa kazi nyingi ambazo ametunga katika fasihi.

1.11.4 Uteuzi wa Sampuli

Bryman (2004) anaeleza uteuzi wa sampuli kuwa ni mchakato wa kuchagua kikundi cha vitu ama watu ili kutumika kama kiwakilishi cha kundi zima linalotafitiwa kwa kuwa ni vigumu kutafitia kundi zima. Hata hivyo uteuzi wa sampuli hutegemea zaidi lengo la mtafiti na habari anazohitaji kuibua (Kothari, 1990). Kwa mantiki hii, sampuli kusudio ndiyo ilitoteuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaksudi. Hii ilitokana na malengo mahususi ya utafiti. Maoni haya yanaungwa mkono na Powell na Connaway (2004) wanapoeleza kwamba katika uteuzi wa maksudi, sampuli huteuliwa kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinahusiana na maswali ya utafiti. Kwa mantiki hii, mtafiti ameshughulikia tamthilia zake tatu pekee ili kupata data ya kuchanganua kwa kigezo cha mtindo na hakuangalia kazi zingine alizozichapisha mwandishi huyu katika kitengo cha fasihi. Alifanya hivyo

kwa kuwa hizi tamthilia zilikuwa na vipengele anuwai ambavyo vilivyomsaidia kujibu maswali ya utafiti ili kufikia lengo kuu.

1.11.5 Ukusanyaji wa Data

Kuna mbinu mbalimbali ambazo mtafiti huweza kutumia ili kukusanya data ya utafiti wake (Seale, 2012). Hata hivyo anakiri kuwa hakuna mojawapo ya mbinu hizi ambayo imejitosheleza. Aidha, mbinu hizi hutegemea data anayokusanya mtafiti. Hii ina maana kwamba ukusanyaji data huongozwa lengo la mtafiti. Kwa mantiki hii, utafiti huu ulitumia mbinu ya usomaji maktabani ili kupata data ya kimsingi. Usomaji wa kimaktaba huhusu kutafuta data kwa kusoma maandishi. Ili kufikia lengo la utafiti huu, mtafiti alisoma kwa uhakiki tamthilia tatu zilizoteuliwa, vitabu, majarida na machapisho ambayo yanayohusiana na malengo ya utafiti ili kupata data za zilizokidhi mahitaji ya utafiti huu. Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo, malengo na maswali ya utafiti yaliongoza usomaji huo. Aidha, majarida na vitabu-meme vilivyohusiana na mada ya utafiti vilirejelewa katika mtandao. Nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo ilimsaidia mtafiti katika kubainisha vipengele vya lugha na kuvichanganua. Kwa kusoma maktabani tuliweza kuweka bayana vipengele vya mtindo tulivyoshughulikia ambavyo ni: Tamathali, sintaksia na uwasilishaji wa maudhui.

1.11.6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data huathiriwa na mbinu za ukusanyaji zilizotumika kupata data husika. Utafiti huu uliegemea zaidi data iliyokusanywa kutoka kwa usomaji wa maktabani. Data za utafiti huu zilichanganuliwa kwa kuegemea mbinu ya uhakiki matini. Uhakiki matini ni mbinu ya kuchanganua data ambapo mada huratibiwa na kupangwa kutegemea mfanano na uhusiano wao ili kurahisisha utafsiri wake (Tromp, 2006). Utafiti ulitumia mbinu hii kuchanganua data kwa kuzingatia vipengele vya kimtindo vya tamathali, sintaksia na uwasilishaji wa maudhui. Baada ya kukusanya data maktabani tulizigawa katika makundi ili kuziainisha kwa makundi mawili: za usimulizi na zile za kitamathali na mwishowe kuelezea namna zilivyoathiri uelewekaji wa maudhui kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Aidha tulizilinganisha tamthilia zilizoteuliwa ili kubaini vipengele vya lugha vilivyojitokeza zaidi kwa kuwa ndivyo tulivishughulikia. Data

iliyokusanywa ilihaririwa na kupangwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti huu na matokeo kuwasilishwa kwa maandishi ya nathari.

1.12 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili usuli wa utafiti ambapo tumeonyesha maelezo ya wataalamu mbalimbali na namna wanavyoielezea dhana ya mtindo na kubaini kuwa mtindo ni usanii katika utunzi. Pia tumeshughulikia suala na malengo ya utafiti wetu, sababu za kuchagua mada ya utafiti pamoja na kujadili umuhimu wake. Aidha, tumechunguza yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti ambayo yametusaidia katika kuuwekea msingi thabiti utafiti huu pamoja na kubainisha pengo tulilotarajia kuziba. Aidha, tumejadili nadharia iliyouongoza utafiti na mbinu zilizotumika kukusanya na kuchanganua data.

MTINDO WA UWASILISHAJI MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA TEULE

2.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia historia fupi ya uandishi wa Arege na ufafanuzi wa dhana ya mtindo wa uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia teule. Aidha tumechanganua jinsi maudhui yalivyowasilishwa katika tamthilia zilizoteuliwa za Arege.

2.2 Uandishi wa Arege

Timothy Arege ni mwandishi ambaye ameinukia kwa kasi mno katika safu ya uandishi wa karne hii. Mwandishi huyu ameandika kazi nyingi katika Kiswahili – fasihi na lugha. Kazi alizozindika ni pamoja na *Kielezi cha Tungo, Mwongozo wa Kifo Kisimani* (2002), *Mwongozo wa Siku Njema* (2002), *Kunga za Kiswahili na Mwongozo wa Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2005). Arege pia ameandika hadithi fupi ya *Ndimi za mauti katika Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na kuhariri mkusanyo *Gitaa na Hadithi nyingine* (2011). Mwandishi huyu ameandika baadhi ya mashairi katika diwani ya *Tamthilia ya Maisha*. Aidha, ameandika tamthilia. Tamthilia alizozindika ni pamoja na *Kijiba cha Moyo* (2009) (ambayo ilishinda Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta mwaka 2011), *Mstahiki Meya* (2009) ambayo ilitolewa kutahiniwa katika shule za upili mwaka 2013 na *Chamchela* (2007). Kwa sasa ni mhadhiri wa fasihi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

2.3 Mtindo wa Uwasilishaji wa Mawazo (maudhui)

Mtindo wa uwasilishaji wa mawazo ni mbinu za kimtindo ambazo mwandishi huzitumia kuyadokeza tu mawazo katika matini za fasihi. Kwa mujibu wa Leech na Short (2007) mtindo wa uwasilishaji wa mawazo hutupa uwezo wa kuyajua mawazo ya mwandishi na wahusika. Hii hutusaidia kufahamu mbinu ya kimsingi ya kuyaelezea hayo mawazo (maudhui). Wamitila (2002) anayaeleza maudhui kwamba ni jumla ya masuala na mambo yanayozungumziwa katika matini za kifasihi. Maudhui huhusu ujumbe ambao mwandishi anajadili katika kazi za fasihi. Mwandishi hawezi kuwa na mtindo bila ya kuwa na cha kueleza. Hii ina maana kuwa mtindo na maudhui ni vitu vinavyotegemeana na kukamilishana katika kuleta maana. Hii ina maana kuwa hatuwezi kupuuza maudhui

kila tunapochunguza mtindo. Ni kupitia kwa mtindo ambapo mtunzi wa kazi za fasihi huwasilisha maudhui yake. Mtindo ndio humwezesha mwandishi kuwa na upekee katika kushughulikia mada husika na kuifanya kuonekana mpya hata kama imekwishaandikiwa na watunzi wengine, (Leech, 2007). Arege ni mwandishi ambaye ameonekana kuegemea mbinu ya kinaya katika kuwasilisha ujumbe kwenye tamthilia zake zilizoteuliwa. Tumechunguza jinsi Arege alivyowasilisha maudhui kwa kinaya ili kuwakejeli Waafrika ambao licha ya kudai kuwa huru, hawaelekei kuelewa dhana hii na ndicho chanzo cha wao kushindwa kujisimamia katika misingi ya kisiasa, kiuchumi na kitamaduni.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2008) kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa. Kinaya huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi ambavyo mambo yanaonekana na jinsi yalivyo sasa (uhalisia wake). Kwa upande mwingine, Kuhenga (1977) anafafanua kejeli kuwa ni uneni wa kimafulimo ambao hulenga kumuudhi mtu kwa nia ya kumwonya kichinichini bila bughudha. Japo kuna tofauti katika ya kinaya na kejeli kutokana na maelezo ya Mbatiah na Kuhenga, Wamitila (2008) anaona kinaya kuwa sawa na kejeli. Mbatiah (2001) anakubali maoni ya wataalamu hawa wawili ambapo anaeleza kejeli au kijembe kuwa ni matamshi yanayolenga kumtweza mtu kwa sababu huwa ya kuchoma, kukata na kutia uchungu. Mtu anapopewa sifa ambazo hastahili, basi huwa anakejeliwa. Ingawa Mbatiah (keshatajwa) anakubali kuwa kejeli huchukuliwa kuwa kisawe cha kinaya, inafaa kuisitizwa kuwa kejeli ni aina ya kinaya yenye ukali wa kipekee. Maoni ya Mbatiah (2001) ndiyo tuliyotumia katika utafiti huu yanayoieleza kejeli kama aina ya kinaya kwa kuwa ni kupitia kwa kinaya ambapo kejeli huweza kufahamika.

Katika lengo letu la pili, utafiti ulilenga kuonyesha jinsi mbinu za usimulizi anazotumia mwandishi huathiri uwasilishaji wa maudhui. Tumechunguza jinsi Arege alivyowasilisha maudhui kwa muhtasari katika tamthilia zilizoteuliwa kwa lengo la kuchanganua mbinu alizotumia katika kuyafanikisha. Aidha, katika muhtasari wa uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia zilizoteuliwa tumechunguza jinsi maudhui yalivyowasilishwa kwa kinaya na kejeli.

2.3.1 Uwasilishaji wa Maudhui katika *Chamchela*

Mwandishi Arege anasawiri mgongano wa tamaduni pamoja na maafa yanayosababishwa

na usasa. Arege anaonyesha kuwa mgongano huu ndicho kiini cha kutoelewana katika jamii. Tamthilia ya *Chamchela* inaangazia jamii iliyovamiwa na utamaduni wa kigeni. Vijana wanaonekana kuwa katika mstari wa mbele katika kufuata mienendo na mitindo hii ya kigeni ya maisha. Kwa kuwa wana pupa, wanatekwa nyara haraka na mitindo mipya ya maisha kwa kuwa hawajaelewa wala kuzama katika tamaduni zao asili. Vijana wanavutiwa na kubadilika kwa urahisi katika imani zao kwani wanaendelea kuzijenga kwa kuwa hazijakomaa. Katika *Chamchela*, vijana wamejitahidi mno kuonyesha ukomavu wa kujitegemea wao wenyewe. Wanalowania ni kuwaonyesha wazee wao kuwa wanaweza kuyadhibiti na kuyaendesha maisha yao bila msaada wowote uwe wa kimawazo au kifedha. Kwa mfano, Mayaka anakataa kuacha mipango ya kumwoa Bisase licha ya kushauriwa na kushtumiwa na kila mhusika. Anadhihirisha ukomavu katika msimamo thabiti wa uamuzi alioufanya. Anautetea msimamo wake vikali bila kutetereka kwa vyovyote vile. Hata hivyo msimamo wake unaelekea kuchochewa na msukumo kwenye misingi ya kiuchumi. Kwa kinaya, mwandishi anawakejeli wazee ambao wanajitana kuwa wanaufahamu utamaduni wa Kiafrika ilhali hawakuwafunza vijana ambao sasa wanawalaumu kwa kufuata na kuiga ule wa Kimagharibi.

Tamthilia imetalii mabadiliko ya vijana na mapuuzo yao kwenye misingi kijamii na kiuchumi. Inaonekana kuwa chambo kinachowavuta katika utamaduni wa kimagharibi ni umaskini. Wosia anaoutoa Sure unakataliwa kwani hakuauni familia ya Mayaka wakati ilmpohitaji zaidi. Mayaka ana madai haya:

(Kwa hasira) Hivi siku zote hizi wamekuwa wapi? Eeh? Unakumbuka siku zile tulivyoishi? Sote tukikaa chumba kimoja na mama? Baadhi ya siku tukishinda bila tonge la chakula. Unakumbuka? (uk. 29)

Mwandishi anafaulu kuwakejeli wazee ambao wanaimba ujamaa kwa vinywa vipana katika misingi ya Kiafrika ambayo huwashirikisha wanajamii wote kusuluhisha majanga yao ilhali hawaonekani kwa vitendo kamwe. Walihitajika kuwepo katika maisha ya watoto wao wanapokua ili wawafunze mila na tamaduni wanazoziiimba sasa, badala yake walienda mbali huko kutafuta hela na kusahau majukumu yao.

Mwandishi pia anaonyesha kuwa kadhia nyingine inayowafanya vijana kupapia na kutamalaki kwenye utamaduni wa Kigeni ni utepetevu wa wazee katika kuwapokeza utamaduni wa Kiafrika. Wao (wazee) badala ya kuwafunza vijana walienda mbali kuchuma mali ambayo hata hivyo haikufaa familia zao bali kuziporomosha. Wanafika kuchelewa na kutaka kuwalazimishia vijana waliopata uhuru wao tayari kupokea wanayoyapendekeza. Wao walisahau kwamba ‘udongo uwahi uli maji’. Ni vigumu kuwafunza vijana itikadi za utamaduni ambao hawakutangamana nao hapo awali kwa kuwa ni vigumu kumkunja samaki aliyekauka. Teknolojia iliishawafunza mengi tayari. Kwa mantiki hii mwandishi anafaulu kuwakejeli wazee ambao wanawalaumu vijana kwa kuufuata utamaduni wa Kimagharibi kikasuku ilhali hawakuwepo ili kuwaelekeza.

Utamaduni unaotetewa na wazee una imani yake kwenye ujamaa wa kuamualiwa tofauti na ule wa kigeni unampa mtu binafsi uhuru wa kujiamulia. Vijana wanapata nafuu katika utamaduni wa kigeni ambao unawapa fursa ya kutenda wapendavyo kwani hauwafungi kwenye jamii kama ule wa Kiafrika. Wanapenda kuishi mijini ambapo wana uhuru wa kutenda wapendavyo bila viziwi vya tetesi za wazee wao. Wazee wanataka kuwafanyia vijana maamuzi bila kuwasikiza. Na hii ndiyo hatari kubwa inayoua maelewano yanayotarajiwa katika kumaliza mgogoro katika utamaduni hizi zenye mila tofauti.

Vijana wanadhihirisha kwa uwazi misukumo inayowalazimu na kupelekea wao kuchukua maamuzi yao katika jamii. Wanatumia kasoro walizoziona katika utamaduni unaotetewa na wazee ili kujihalalisha kwenye matendo yao. Mayaka katika kutetea uamuzi wake wa kutaka kumwoa Bisase anasema:

...Mimi si mtoto ulivyokuwa wewe. Wewe hukuwa umeamua mwenyewe. Mama alipokuwa akiunga mkono uolewe na yule mzee, kwa nini hakuona vibaya? Kwa nini kwangu aone vibaya? (uk. 73)

Hii inaonyesha kuwa hapatakuwa na maridhiano pasipo wazee kutathmini uwezo wao wa kuwalazimishia vijana mila zao bila kuwahusisha na kuwaelewa.

Elimu wanayopata vijana inawaandaa kujisimamia kimawazo na kifedha. Inakuwa kinaya kuwa uhuru huu wanaopigania vijana ndio chanzo cha mgongano na wazee wao. Vijana

wanataka uhuru wa kufanya watakavyo lakini wazee wanakerwa kwa kuwa wanaona ni mapuuza. Mabadiliko haya ya usasa ndiyo chanzo cha mafarakano yanayozikumba nchi nyingi za bara la Afrika. Mwandishi anataka kuonyesha kuwa mabadiliko haya ni kiini cha kukosa maendeleo yenye manufaa kwenye jamii kutokana na elimu isiyoendana na uvumbuzi unaohitajika katika jamii za Kiafrika. Inakuwa kinaya kuwa elimu waliyopata vijana inawafanya kuwa wategemezi badala ya kujisimamia na kuvumbua. Vijana wanakejeliwa kwa kung'ang'ania utamaduni usio manufaa kutokana na kasoro katika utamaduni wa Kiafrika.

Afadhali sisi dadangu. Wapo wenye kisomo
kama chetu lakini ukiwaona utawasikitikia.
Afadhali sisi mara mia. (uk. 30)

Masomo yalifaa kuwaelekeza vijana ili waishi maisha ya raha na kujisimamia kifedha. Inakuwa kinaya pale masomo hayo yanawaporomoshia na kuwafanya wategemezi katika jamii. Kwa maelezo haya, mwandishi analenga kuwakejeli vijana ili wafahamu kuwa utamaduni wa Kimagahribi wanaoukimbilia una kasoro nyingi kuliko ule wa Kiafrika walioukimbia. Anawaasa kuwa mwacha mila ni mtumwa ili wafahamu kwamba chako kibaya ni heri kuliko kizuri cha mwenzio.

Mwandishi anaonyesha ulazima katika mabadiliko kwa kuzingatia uzuri na ubaya wake mtawalia. Kwa mfano, amelalamikia jinsi uhuru wanaopata vijana ulivyowapelekea kuasi na kujishughulisha na mambo yanayowadhuru kama kujiingiza katika uuzaji na matumizi ya mihadarati, upuuzaji na ubinafsi. Vijana waliukimbilia utamaduni wa kimagharibi na kuushika mkikimkiki wakidhani utawanufaisha maradufu. Inakuwa kinaya kuwa utamaduni huu ndio chanzo cha maangamizi yao. Abaya anaeleza hivi:

Na waliposhindwa baadhi wakaingia katika
malevi; si dawa za kulevya, si tembo, si uha-
lifu... unaona? (uk. 55)

Kwa usemi huu mwandishi anawakejeli vijana ambao wanaandama unyounyo nyayo za utamaduni wa Kimagharibi unaowapotosha kinyume na walivyoona hapo awali kuwa wenye manufaa.

Hata hivyo mwandishi anaendelea kutetea kauli kuwa hakuna kinachodumu katika maisha ila mabadiliko. Mabadiliko ni lazima yawepo na mabadiliko haya hubadilisha mikondo ya maisha kadri wakati unavyosonga. Kilicho wazi ni kuwa mabadiliko kiwakati ndiyo husababisha mabadiliko kimawazo na kitabia. Mwandishi anadhamiria kuonyesha kuwa ili mataifa ya bara la Afrika kupata maendeleo yoyote yenye manufaa ni sharti jamii zote zitalii na kukubaliana katika yale yenye manufaa na kutupilia mbali yasiyofaa. Hili linawezekana katika maelewano yasiyo na ubinafsi kwani mabadiliko ni jambo lisiloepukika katika maisha ya kijamii. Hata hivyo, tamthilia ya *Chamchela* inachunguza mabadiliko yanayotokea katika jamii kwa mtindo wa kinaya ili kumsaidia msomaji kuifuatilia kwa urahisi.

2.3.2 Uwasilishaji wa Maudhui katika Tamthilia ya *Mstahiki Meya*

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni mojawapo ya kazi za Arege ambazo zinaweka wazi chimbuko la uongozi wa kiimla uliotukuka barani Afrika. Tamthilia hii inazungumzia maisha ya wanacheneo ambao wanaongozwa na Mstahiki Meya ambaye anaitwa Sosi. Mstahiki Meya ni kielelezo cha viongozi katika nchi kadha za bara la Afrika. Cheneo ni kielelezo cha nchi za bara la Afrika ambazo zilipata uhuru na hivyo nyadhifa za uongozi zikatwaliwa na viongozi wa Kiafrika wenye uwezo hafifu. Viongozi hawa licha ya kudai kuwa huru, walikosa sera mwafaka za kuwasaidia katika nyadhifa zao mpya za kuongoza. Hii iliwalazimu kuchukua na kuiga kikasuku sera za wakoloni wakongwe na kucheza midundo ya nyimbo zao katika kuziendesha nchi zao changa. Badala ya kuunda sheria zilizohusiana na matakwa ya mataifa yao, walifanyia mabadiliko sheria za kikoloni lakini kwa lengo la kujinufaisha kama ilivyoonyeshwa na Orwell katika riwaya yake ya *Shamba la Wanyama* kuwa Mkimwa ambaye anatwaa hatamu za uongozi baada ya wanyama kuungana na kufaulu kumfurusha Bw. Mtiki (binadamu aliyewanyanyasa wanyama) alisaidiwa na nguruwe wenye tamaa kama yeye katika kubadilisha sheria zilizoundwa na Bwana Mtiki kwa manufaa yao binafsi. Kwa kifupi, viongozi hawa wanaendeleza na kudumisha uongozi wa kiimla ambao ulianzishwa na ukoloni mkongwe. Lengo la Arege ni kuonyesha kuwa uwezo duni na hofu ya kung'atuliwa uongozini umewavua utu viongozi hawa na kuwavisha unyama. Ni kama anavyoeleza Orwell (keshatajwa) katika riwaya yake ya *Shamba la Wanyama* kuwa baada ya wanyama kuungana pamoja na kufanya mapinduzi yaliyomfurusha Bw. Mtiki kutoka

shamba lao, binadamu ambaye aliwadhulumu, nguruwe walipochukua hatamu za uongozi wanakuwa wakatili hata zaidi kumshinda binadamu aliyekwishafukuzwa.

Viongozi hawa wanafahamu fika kwamba hawana tajriba ya kuyaendesha mataifa yao. Hali hii huwafanya kutumia mbinu mbalimbali zinazowanyanyasa na kuwadhulumu wakazi wa mataifa yao ambazo zina misingi yake kwenye udikteta mradi wasalie uongozini. Mojawapo ya mbinu muhimu zinazodumisha uongozi wa madikteta hawa ni kupitia kwa ahadi za uongo ambazo wanatoa kwa wananchi wao. Viongozi huonekana kusomea skuli ya kuwadanganya wananchi kiasi cha kuwafanya waamini kuwa wanayashughulikia majanga yanayowakumba. Wengi wa wakazi wa mataifa haya machanga huwa na imani na wale wachache wanaonekana kujua njama hizi hupuuzwa au kukemewa vikali. Imani hii huwafanya wakazi wa mataifa machanga kuendelea kudidimia katika ulitima wao. Kwa kuwa wakazi hawa ni maskini walio na uhitaji wa hali ya juu, viongozi hupata fursa ya kuwadhalilisha kwani mhitaji kila wakati atasalia kuwa mtumwa katika jamii hii iliyojengeka kwenye misingi kibinafsi. Tunafahamu kuwa dawa zilizotumainiwa kufika hospitalini hazitawasili. Matamshi ya Meya yanadhihirisha ukweli huu anaposema:

Ahadi zetu zimetufaa hadi sasa.
Atajua nani ukweli ila wenyewe
myaseme huko nje? (uk. 21)

Matamshi ya Meya kama kiongozi yanadhihirisha uongozi ambao huna mwelekeo au tuseme ulioshindwa kutimiza lengo lake la kimsingi. Ni kinaya kwa kuwa licha ya Meya kuaminiwa kuwa anayashughulikia majanga yao anatoa matamshi kama haya. Ukweli ni kuwa uongozi wa kidikteta umesababisha viwango duni vya maendeleo katika mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa kuwa haujali wananchi wake. Hii ni mojawapo ya mbinu ambazo viongozi hutumia ili kupata kibali cha kuendelea kusalia uongozini kwani huwapa wananchi matumaini yasiyozalisha maendeleo. Matokeo yake ni kuzorota kwa maendeleo ya nchi zao kinyume na maendeleo yanayotarajiwa. Hivi ndivyo Arege anavyofaulu kuwakejeli viongozi wanaowahadaa wananchi kuwachagua katika nyadhifa mbalimbali. Kwa mtindo huu mwandishi anaashiria kuwa shabaha ya wananchi si mbaya bali ni viongozi ndio humezwa na tamaa inayokuza ubinafsi na kuishia kuzitumia nafsi zao vibaya.

Pili, viongozi hawa wanajua vipawa vyao ni hafifu mno katika kuendesha nchi zao kwa mikakati ya kusuluhisha matatizo yanayowakumba wakazi wao. Kwa kuwa wanaelewa hili, wanajua kuwa umoja wa wanyonge ambao ni wengi ni tishio katika kufikia matamano yao ambayo yamejaa ubinafsi. Viongozi hawa hutumia mbinu ya ‘tenga utawale’. Viongozi hawa wana tamaa iliyosababishwa na ubinafsi wa kujitakia makuu. Ili kufikia malengo yao, wametafuta wafuasi wengi wanaowasaidia na kuwatendea kama wanavyotaka ili kuhakikisha hakuna ushindani na pingamizi katika kuyafisidi mataifa yao machanga. Wamewaajiri watu wasiohitimu na kushikilia nyadhifa zisizokuwapo katika katiba ya mataifa yao. Kwa kujua na kufahamu kuwa hawana sifa za uongozi bora au ulio wa manufaa kwa wananchi, wao hutumia muda mwingi katika kupanga mbinu watakazozitumia ili kuendelea kuongoza na labda kusalia uongozini milele. Bili, mshauri wa kupotosha na Mhazili wamepewa kazi za ofisi kwenye misingi ya ubarakala na sio kuhitimu. Mpango huu uliwapa nguvu za kuwadhulumu wanyonge. Kwa kuwa wana uwezo wa kimamlaka wao huamrisha na kuhakikisha kuwa amri zao zinatekelezwa bila pingamizi zozote. Kinaya ni kwamba licha ya kukosa mamlaka ya kuyaendesha mataifa yao, wako radhi kukubali ushauri wa vibaraka ambao inasadifu kuwa hawana maarifa yoyote. Ni kama kipofu kumwongoza kipofu. Kwa mbinu hii mwandishi anawakejeli viongozi wa bara la Afrika ambao licha ya kukosa uwezo wa kuyendesha mataifa yao wanang’ang’ania nyadhifa hizo.

Mbali na kuyafisidi mataifa yao, viongozi hawa hawana uwezo wa kubuni njia za kizalishaji zitakazowapelekea wakazi wao kujitegemea. Wao huongozwa na kiburi cha ukengeushi. Mataifa haya machanga yanahitaji viwanda ili kujiendeleza kiuchumi. Inakuwa kinaya kwamba badala ya kufungua viwanda na kujiundia bidhaa zao, wao huagiza bidhaa za bei ghali bila kufahamu madhara yake katika chumi zao changa. Katika kufanya hivi, pesa nyingi hutumika. Fedha hizi zingetumika katika miradi ambayo ingeimarisha viwango vya maisha kwa wananchi wa mataifa yao duni. Inakuwa kinaya kwamba wanacheneo wanaishi maisha ya kubabaisha na kubahatisha kwa kuwa hawana uwezo au namna ya kujitosheleza kwa mahitaji ya kimsingi licha ya juhudi za kuwachagua viongozi ili waweze kutatua shida zao.

Wanacheneo wana njaa licha ya kuwa wagonjwa. Hawa ndio watu waliomchagua Meya. Mwandishi anakuza kinaya ili kukejeli viongozi wa mataifa machanga anapommulika Meya ambaye yuko radhi kuwapa wageni anaowaita ‘ndugu’ ambao hutoa misaada kwa Cheneo mapokezi ya kupigiwa mfano huku watu wake anaowaongoza wakiangamia. Meya anajisemea:

Hoteli ya kifahari. Vyakula kutoka kila
utamaduni. Si sembe. La hasha! Mvinyo
nitauagizia kutoka Urusi na divai kutoka
Ufaransa. Wale wa kunywa wajue Cheneo
si mji hivi hivi. Wauone ukarimu wetu na
maana ya udugu wetu. (uk. 25)

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatutarajii kumpata kiongozi anayeshuhudia matatizo mengi yanayowakumba wananchi ambao anaowaongoza kuwa na mawazo hafifu kama haya. Huu si werevu bali ni ujinga ambao huwezi kuleta maendeleo katika nchi change. Arege anaonyesha kuwa misaada hii inayotolewa mara nyingi haisadii katika kuinua maisha ya maskini walio wengi katika jamii bali huwateka nyara kiakili Waafrika ambao hukubali na kuridhia unyonyaji kikupe wa ‘kaka’ zao. Na ndio sababu Mohamed anaiita ‘paja lililooza’ katika *Amezidi* kwa kuwa hailengi kumsaidia Mwafrika kujiendeleza kiuchumi bali kumwangamiza.

Kwa kinaya, mwandishi anatalii na kukejeli dhima ya washauri na ushauri wao katika mataifa machanga. Ameonyesha na kuweka wazi ni kwa jinsi gani ushauri unaotolewa ni muhimu katika kuleta au kukosesha maendeleo katika nchi za bara la Afrika. Ushauri wa kupotosha wanaopata viongozi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu ni chanzo cha maangamizi ya kiuchumi yanayoshuhudiwa katika nchi hizi. Kupitia kwa ushauri wa Madiwani I na II na Bili, wanacheneo wanaendelea kuteseka na kudidimia katika maisha ya ulitima. Badala ya kumshauri Meya aweze kuunda sera mwafaka za kuimarisha maendeleo ya Cheneo, wanamshawishi na kumfumba macho kutokana na ukweli wa hali ya Cheneo mradi tu wanufaike. Wanamsaidia kwa kufanya mipango ya kuifisidi Cheneo kwa manufaa yao tu. Bili anapoona kuwa hamna njia itakayomwezesha kunufaika anatoa ushauri wa kuuza fimbo ya Meya jambo ambalo linakubaliwa kwa pamoja.

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011) polisi ni askari wa kulinda usalama. Katika mazingira ya Cheneo, polisi ni walinzi wa Mstahiki Meya na vibarakala wake. Badala ya kuwatumika wanacheneo, askari hawa wanawadhulumu kwa kuwapiga na kuwaumiza kila wanapoandamana kwa nia ya kulalamikia au kushtakia majanga yao. Askari kwa uhitaji wao, hawana budi kupokea na kutekeleza amri zinazowadhilisha wananchi kutoka kwa vikaragosi wa Meya mradi wahakikishe kuwa wana riziki. Askari wanajua fika dhima yao ya kuwalinda wananchi lakini kwa kuwa ni amri wao hutekeleza madhila haya kwani wanaogopa adhabu itakayozalikana kutokana na ghadhabu ya Mstahiki Meya. Askari badala ya kuwahakikishia wanacheneo usalama, wanazua rabsha kuwaumiza na hata kusababisha vifo kwa wananchi wasio na hatia. Hiki ni kinaya kwa kuwa si matarajio ya wananchi.

Mahubiri na maombi ya kidini hustahili kusifu kadhia ambazo huendeleza utu katika jamii. Umuhimu wa maombi ni kusuta vitendo viovu na visivyofaa ambavyo ni chanzo cha uozo katika jamii. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* dini inatumika kwa kinaya kuwatakasa viongozi waovu kwa umma mkubwa sawia na vyombo vya habari. Inakuwa kinaya kwamba wahubiri kama viongozi hawa wanaowatakasa, hudhihirisha tamaa na ubinafsi kwani wao pia hushiriki katika kuyafilisisha mataifa yao. Kwa kukubali kuhongwa na viongozi hawa kinyume na dhima yao ya kimsingi ya kuwakemea na kuwasuta viongozi wanaoendeleza uongozi ulioandamwa na tamaa iliyojengeka kwenye ubinafsi, inakuwa kinaya kwani hatutaraji kuwaona wakitekeleza vitendo kama hivyo. Viongozi wa kidini kwa ngozi ya kondoo, hutumia uwezo wao katika kuwahadaa viongozi kwa tamaa na ubinafsi wa kujiendeleza. Wao hawana budi kupokea hongo kwa fumbo la sadaka kwani wamejawa na tamaa na ubinafsi. Licha ya kujua kuwa uongozi wa Meya una doa linalowaumiza wanacheneo katika sekta zote za kiuchumi, mhubiri anamwomba ili uongozi wake udumu akisema hivi: Mwendolee nuksi ya maadui na kinyongo cha mahasidi (uk. 42). Hata hivyo, kinaya katika maombi haya ni kwamba maadui na mahasidi wanaorejelewa na Mhubiri katika muktadha huu ni wanacheneo na wafanyikazi wanaopinga njama za uongozi unaowafaa wachache katika jamii. Wanaopinga uongozi mbaya wa Meya ni wazalendo kama Daktari Siki na Kheri (Diwani III). Kwa mkabala huu Arege anafaulu kukejeli na hivyo kuikashifu dhima ya kimsingi

ya dini ambayo badala ya kutunza maadili inatukuza maangamizi kutokana na ubinafsi wa kujitakia makuu.

Vyombo vya habari huwa na jukumu la kusambaza habari kwa faida na maendeleo ya wananchi. Katika mazingira ya tamthilia ya *Mstahiki Meya* vyombo vya habari badala ya kutumika kueneza habari za kuhamasisha maendeleo hutumika kueneza propaganda za uongo ambazo zinawasababishia wanacheneo hali ngumu kimaisha. Badala ya vyombo hivi kumwendeleza binadamu kwa kumpasha habari za ukweli, vinamdhalilisha kwa kueneza habari za uongo zisizowafaidi chochote. Hiki ni kinyume cha matarajio. Ni kinaya kwani vyombo vya habari havitekelezi majukumu yao ya kuimarisha kimaendeleo. Aidha, mwandishi anatumia kinaya kukashifu viongozi wanaotumia vyombo vya habari kwa manufaa yao dhidi ya nchi nzima yatakayowafaa wananchi kwa jumla.

Ofisi ni mahala pa kufanyia shughuli muhimu za kuleta maendeleo katika jamii. Ofisi ni mahali ambapo tunataraji kuwaona wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali katika uongozi wakijadili hatua wanazonuia kuchukua kwa manufaa ya wananchi. Katika mazingira ya tamthilia hii, inakuwa kinaya kwani ofisi ni mahali pa kufanyia shughuli za kuifisidi serikali na kujinufaisha. Meya na madiwani wake ambao pia ni kitengo cha washauri, wanapanga njama za kulifisidi Baraza Cheneo pasina kujali maslahi ya wanacheneo wanaowawakilisha katika nyadhifa wanazozishikilia. Inakuwa ni kinaya kwamba baada ya kuyafisidi mataifa yao kwa rasilimali, viongozi hawa hujiona wenye uwezo usiotetereka na ni vigumu kuweza kuelekezwa na walio na nia njema hata familia zao kwani huwaona kama mahasidi. Wanakengeuka na kukosa imani kwa watu wa jamaa zao kwani hujiaminisha kwenye utajiri wao wa ghafla uliotokana na njia za haraka na mkato. Wanawaona kutowafaa na kuwachukia kwa kuwa wanawaambia ukweli mtupu kuhusu hali duni katika nchi zao. Haya yote wanayofanya ni kutokana na tishio la maskini ambao ni wengi na huenda wakiungana watawafurusha. Meya anamfukuza daktari Siki ambaye ni binamu yake kwa kumshauri kuhusu dharura iliyopo na umuhimu wa kuyashughulikia mahitaji ya kimsingi ya wanacheneo. Ukweli huu ndio unamfanya Meya kupandwa na hasira na kumwamrisha mpambe wake - Gedi asimruhusu kuingia kwake tena. Anasema:

Hakikisha mtu huyo halikaribii lango
kuu kuanzia sasa. Jengo langu alione
paa. Alright? (uk. 15)

Matamshi haya yanadhihirisha wazi kuwa viongozi huwaona watu wa jamaa zao kuwa maadui badala ya ndugu. Hali hii ndiyo huwafanya kuwageukia washauri ambao kila mara wako radhi kutekeleza maagizo kulingana na matakwa yao. Hata hivyo, yanaonyesha kinaya kuwa viongozi hawawataki washauri wanaowaambia ukweli wa hali halisi katika majanibu yao bali huwapendelea wanaowadanganya.

Ardhi ni jambo ambalo limekuwa likizozaniwa katika jamii mbalimbali. Kwa hivyo ni matarajio ya wananchi kuwa viongozi wanaowawakilisha katika nyadhifa mbalimbali watatafuta suluhu la kudumu katika umiliki na ugavi sawa wa ardhi. Inakuwa ni kinaya kwamba viongozi na wale wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali za kuwahudumia wanajamii ndio huhakikisha kuwa wanapata ardhi kwa mbinu zozote zile bila kuwajali walala hoi wasiomiliki chochote. Bili ana vipande vya ardhi alivyopata kutokana na ukupe wake kwa Meya. Meya vilevile ana vipande kadha vya ardhi. Vipande hivi wamevipata kwa njia zisizo halali. Bili amevipata vipande vyake kutokana na juhudi za ukupe wake kwa Meya. Hili ni dhihirisho kuwa licha ya mataifa ya ulimwengu wa tatu kupiga vita ukatili ili kuleta usawa kwa watu wa matabaka tofauti, ukaragosi uliokithiri katika jamii unakwamiza juhudi hizi na kukatiza tamaa. Vipande hivi vya ardhi vinastahili kuwafaa wananchi wote haya hivyo ni kinaya kuwa havimfai yeyote katika jamii kwa kuwa ni mali ya kibinafsi.

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* imetalii kwa kina na kuonyesha kuwa uongozi wa kiimla unapata mashiko yake kwenye ahadi za uongo, ufisadi, ukandamizaji wa wafanyikazi na uozo wa kidini. Sifa hizi zinazodhihirika katika ukoloni huu mamboleo ni sawia na za ukoloni mkongwe. Licha ya vitendo vinavyodhihirishwa na viongozi wa kiimla ambavyo vinahujumu haki za wanyonge, mwandishi anaonyesha kuwa wingi na umoja wa maskini ndiyo ngao tu ya kuwang'oa viongozi wa aina hii kutoka uongozini. Imani ya Arege ni kuwa wingi wa wanyonge ni ngao dhidi ya viongozi wachache waliojawa na ulafi na tamaa. Ukweli ni kuwa tamthilia nzima imesimuliwa kwa mtindo wa kinaya ili kukejeli viongozi wa mataifa machanga katika vitendo vyao viovu vinavyozuia maendeleo ya kiuchumi pamoja na yale ya kijamii.

2.3.3 Uwasilishaji wa maudhui katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*

Arege ametunga tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* mwaka wa 2007 wakati mmoja na ile ya *Mstahiki Meya* ili kuendeleza dhamira yake yenye misingi katika uongozi wa kiimla uliotapakaa katika nchi nyingi za bara la Afrika na kukita mizizi pale. Tamthilia hii ni miongoni mwa kazi za kifasihi zinazochunguza uhusiano uliopo baina ya ubepari wa mataifa na hali duni ya kiuchumi iliyojiri mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa mtindo wa kinaya. Mwandishi anatalii maudhui ya kiuchumi na mfumo wa kibepari ambao licha ya kuwakandamiza wakazi wa mabara ya Afrika unapunguza nafsi za wafanyikazi na kuwafanya kujihisi kuwa duni. Mahusiano haya yameendelezwa kwenye misingi ya udhalimu. Mwandishi ameelezea maonevu haya kwa kinaya akitumia sitiari pevu ili kukejeli mfumo mzima wa uelewaji wa dhana ya uhuru katika uzalishaji mali.

Katika tamthilia hii mwandishi anaonyesha kuwa uongozi uliopata mashiko yake kwenye mfumo wa kibepari, umemiliki nyenzo za kimsingi za uzalishaji mali kupitia kwa ufasidi, uongo na zaidi katika kuwakandamiza wale waliopata mwangaza wa kuona njama hii ya kunyanyaswa. Hili hutekelezwa ili kuzuia juhudi za wale waliopata mwamko mpya kisiasa dhidi ya kuwazindua wanyonge wengine katika jamii. Mwandishi kupitia kwa mhusika nguli (Sele), anasawiri uhusiano uliopo baina ya mataifa ya ulimwengu wa kwanza ambayo huyapa misaada na kuyamiliki mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa kuyafanya yakose kujitegemea. Mwandishi anasawiri kwa kina misaada inayotolewa kwa mataifa machanga na kuonyesha kuwa misaada hii haiwafai Waafrika ila tu ni chambo kinachotumiwa ili kuweza kupata fursa ya kuwanyonya Waafrika rasilimali zao. Hii ni kinaya kwa kuwa Waafrika wenyewe hawaelewi hali hii.

Arege anaendelea kuonyesha kuwa hali ya uhitaji katika mataifa mengi ya bara la Afrika imesababishwa na unyonyaji wa nguvu za wakazi wake kwa malipo duni. Anaeleza kuwa mipango ya kuyasukuma mbele kimaendeleo mataifa machanga barani Afrika ambayo inaamuliwa na kuwekwa na mataifa yanayodai kujitegemea ni chanzo cha kudorora kwa maendeleo yanayotarajiwa. Hii inatokana na ukweli kwamba walioshikilia (wakoloni) nguzo za mfumo huu wa kibepari waliwafumba macho wakazi wa nchi changa kwa kuwapa misaada isiyowafaa. Misaada hii ambayo kwa kawaida imefungamanishwa na utekaji nyara akili za Waafrika ni baadhi ya mbinu zilizowafanya waamini wao ni

wahitaji. Matokeo yake ni kuwa wahitaji katika nchi zao wakidhani wako huru. Bi. Rahma akithibitisha imani hii anasema:

Wahenga wanasema, mwenye
nguvu mpishe! Sasa utapigana nao?
Usiloliweza unaliacha. Unafungua
ukurasa mpya. (uk. 29)

Matamshi haya ni dhihirisho kwamba Mwafrika ameridhia matendo maovu atendewayo na hataki kuchukua jukumu la kupigania haki yake. Hii ndiyo sababu kuu ya uongozi wa kibepari kuendelea kumkandamiza kwa kuwa ameamini hana uwezo wowote mbele ya bepari. Mfumo wa kibepari umehakikisha kuwa wakazi wa Afrika wanabaki mazuzu kwa kuwawekea minyororo ya kisaikolojia inayowaaminisha kuwa wako huru kimawazo ilhali wanatawaliwa maradufu kinyume na wanavyojiona wao wenyewe.

Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* inasawiri kwa kina tunavyoyaona matatizo yetu hapa Afrika kijuujuu bila kuzamia na kuwazia katika kuyasuluhisha. Madaktari ambao ni wakoloni hupata fursa ya kutupendekezea tiba ambayo ni suluhu lisilotufaa. Wao hufanya hivi sio kwa kuyaauni mataifa ya bara la Afrika kutokana na majanga yanayoyasibu bali kwa manufaa yao wenyewe. Kisa cha papa na vidagaa kinachojadiliwa tamthiliani ni picha ya mwandishi ya kuchora uhusiano huu. Papa ambao ni wakoloni wanaoshikilia nyenzo za uzalishaji mali na vidagaa wakiwa ni wananchi katika nchi zinazotawaliwa na wakoloni huendelea kuumia kutokana na dhuluma za papa kwani hawana uwezo wa kujitetea. Mabepari huzozana na kupigana wao kwa wao na wakati mwingine hali hii husababisha maafa kwa wakazi wa nchi changa barani Afrika kama vile mfumko wa bei. Chanzo cha mizozo hii ni rasilimali za nchi za ulimwengu wa tatu ambapo mabepari hung'ang'ania ili wapate kuzihodhi na kuzimiliki. Mabepari hufanya hivi baada ya kuhakikisha kuwa wameshaiua imani ya wakazi wa mataifa haya kisaikolojia. Ushahidi wa hali hii ni katika matamshi ya Sele ambaye anasema:

...Mara wanashauriana kuhusu kitu fulani na kuniashiria.
Halafu kwa kauli moja wakasema “Bado amelala.” Waka-
wa wananipekuapekua kila mahali. Kwanza nguo, halafu
mwili na nywele. Waliposhindwa kupata chochote nikao-
na wamechukua vyembe vyao. Niliogopa. Wazo likanijia
la kuwatapikia moyo wangu. Pale pale nikautapika. Wote
wakaukimbia. Niliutazama nikaona unafanana na kida-

gaa cheusi. Wakakitwaa huku wakikipigania. Nikajua ha-
wakuja kuutibu mwili wangu bali kuutwa moyo wangu... (uk. 80)

Shabaha ya mwandishi ni kuonyesha kuwa mfumo wa ubepari hukuja kuleta nafuu ila tu kuzifisidi nchi za ulimwengu wa tatu rasilimali zao. Mfumo huu ulifika ‘kumlalisha usingizi wa pono’ Mwafrika ili asilalamikie madhila anayofanyiwa. Mabepari hawakuja kusuluhisha majanga ya nchi za bara la Afrika bali kujinufaisha.

Katika kuweka wazi sababu zinazoyafanya mataifa ya bara la Afrika kukosa maendeleo yoyote yenye manufaa, Arege anatoa maelezo yanayoshihi ngano ya Plato ya Pango ambapo watu walikuwa wamefungwa minyororo na kuishi pangoni penye kiza kikali ajabu. Mmoja wao alipopata fursa ya kujinasua na kutoka nje alistaajabia mwangaza wa jua pamoja na uzuri wake. Aliporejea pangoni na kuwalezea wenzake ugunduzi wake hawakumwamini bali walimwona mwendawazimu asiyejimudu wala kujielewa. Waliona mambo haya ni ndoto iliyokuwa mbali na uhalisia kwa kuwa walifurahi kuwa gizani. Mtindo huu ndio hasa aliutumia Arege katika hii tamthilia yake ya *Kijiba cha Moyo* ili kukuza maudhui yake kwa kinaya. Kwa mtindo huu Arege anafaulu kuwakejeli Waafrika wanaojitapa kuwa wako huru ilhali wanatawaliwa maradufu.

Pengine kuzinduka kwa Sele na kufahamu kuwa anapatikana katika mfumo wa ubepari, katika jamii isiyomwelewa ndiko kunamfanya kuonekana mgonjwa. Sele anaelewa fika kuwa yeye na wahusika wanaomwona kuwa mgonjwa wamo kwenye tabaka moja la wanyonywaji. Sele akiwa katika harakati zake za kujikomboa kimawazo kutokana na minyororo ya mfumo wa kibepari, anajikuta amekumbwa na changamoto kubwa kwani anakosa mhusika anayemuunga mkono kwa dhati. Inakuwa ni kinaya kuwa mhusika aliyepata mwamko mpya ndiye anayeonekana ‘mgonjwa’ na kutafutiwa daktari na wale ambao ndio haswa ndio ‘wagonjwa’ wanaohitaji matibabu hayo. Daktari anayeletwa kumtibu anafika kwa fikra zake za uongo wa kujinufaisha. Katika kusisitiza sababu na umuhimu wa mjo wake anasema:

Sele, kuja nimekuja kwa ajili yako wewe
ndugu mwenzu. Sikuja kwa sababu ya kujileta.
Na wewe unajua hivyo. Ningejjali singetoka
kwetu huko nikamwacha mke wangu mpendwa
na watoto wetu kuja hapa... (uk. 56)

Hii ndiyo minyororo ya kuimarisha imani ya wakazi wa Afrika kuwa wakoloni wa miliki zao walikuja kwa nia njema ya kuwasaidia. Mwandishi anaendelea kumulika mbinu za ukoloni za kuwapa Waafrika misaada kwa mkono mmoja na kuficha uozo wao kwa mkono mwingine. Waafrika hawaminiwi kuwa na uwezo wowote na ndiposa hawapewi fursa ya kuelezea au kushiriki katika kutatua matatizo yanayowakumba kamwe. Inakuwa ni kinaya kwa daktari (mkoloni) kudai kuwa amekuja kumsaidia Sele (Mwafrika) ilhali amekuja kwa nia ya kujinufaisha pekee.

Sele ni kielelezo cha wananchi waliozinduka na ambao wamezama katika kuchunguza manufaa ya mahusiano na mataifa haya. Mhusika huyu ametumiwa kama kizindushi kwa wakazi wa nchi za bara la Afrika kuwa uhuru wa Mwafrika katika misingi ya kiuchumi, kitamaduni na kisiasa unawezekana iwapo ataamka kimawazo na kujitathmini kwa kujihakiki katika hali yake ya sasa. Hii inakuwa kinaya kwani kila mhusika tamthiliani anamwona kuwa ‘mgonjwa’

Arege anaashiria kuwa hakuna anayeweza kumnasua na kumkomboa Mwafrika kutokana na nguvu hizi za kumilikiwa na kudhibitiwa katika nyenzo za uzalishaji mali ambazo ni kitovu cha uhai wake ila yeye mwenyewe. Analenga kuonyesha kuwa hatua ya kwanza na muhimu ni kujikomboa na kupata uhuru wa kimawazo kutokana na minyororo ya akili kwamba alizaliwa kuwa mhitaji hata katika nchi yake. Ung’amuzi huu ndio kwa maoni ya mwandishi anaona kuwa utamsaidia kujikomboa na kujiendeleza. Ushahidi huu unajitokeza Sele anaposema hivi:

Lakini nyoyo na akili zao
Shaka zinanitia.
Nyoyo zao zina ukungu
Wala hazitaki kusikia
Kilio cha moyoni mwangu
Vipi basi niamini tiba yao. (uk. 98)

Hili ni dhihirisho kuwa wanaoendesha mifumo ya kibepari hawana lolote jema katika maendeleo barani Afrika. Mwandishi anatoa onyo dhidi ya kuwaamini na ushauri wao kwani wana inda kwa nchi hizi za ulimwengu wa tatu. Wamekuja kwa lengo moja tu:

kumiliki, kudhibiti na kunyonya rasilimali za mataifa ya bara Afrika huku wakiwafanya Waafrika kukata tamaa na hivyo kuridhia madhila katika janibu zao.

Mwandishi anaonyesha kuwa ukombozi wa mataifa ya Afrika katika misingi ya elimu, itikadi na uchumi yatawezekana tu ikiwa Mwafrika mwenyewe atajirejelea, atajitafakari na kusaili nafsi yake ili apate kujikomboa kisaikolojia. Hii itamwezesha kuwazia kwa kina shida zake na kuzitafutia suluhu halisi. Sasa atakuwa daktari wa nafsi yake na hivyo kuwa na uwezo wa kutibu ugonjwa wake bila kutapatapa katika kugonga ndipo kwenye tiba. Kwa njia hii ataweza kuwa na uhuru wa kujiwazia badala ya kuwaziwa na hawa mabepari wa kikabaila. Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* imeandikwa kwa kinaya kwa lengo la kuzindua wakazi wa mataifa machanga waweze kujitahidi na kujikomboa kimawazo ili kujiendeleza kwa misingi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kinaya hii inabainika baada ya kutamatisha kusoma tamthilia hii ambapo inabainika kuwa ugonjwa wa Sele ugonjwa si ule wa kawaida kama ulivyochukuliwa na wahusika tamthiliani bali kuzinduka kutokana na mwamko mpya wa kisiasa na kijamii.

2.3.4 Wazo kuu la Mwandishi katika Tamthilia Teule

Mwandishi ametumia mtindo wa kinaya katika tamthilia tatu zilizoteuliwa ili kukejeli nafsi za Waafrika kuwa ‘msiba wa kujitakia hauna kilio’. Ametalii na kuonyesha kwa uwazi kuwa hali anamojikuta Mwafrika imetokana na kuzifuata ‘nyayo’ za mkoloni kikasuku bila kumpiga darubini kubaini njama zake za kumla akiwa hai. Kwa kufanya hivi, Arege anataka kuonyesha na kudhihirisha wazi kuwa Mwafrika mwenyewe ndiye hasa kiini cha matatizo yake bali mkoloni. Hivyo basi, Mwafrika hastahili kulalamika kwa vyovyote vile madhila anayofanyiwa na ukoloni mkongwe pamoja na ule mamboleo kwani ana uwezo wa kujinasua na kubadilisha hali yake.

Kupitia kwa kinaya, inabainika wazi kuwa Arege anaonyesha tumaini la kutia moyo kwani anatalii njia za kumwezesha mwafrika kujinasua kutokana na minyororo ya ukoloni. Suluhu analotoa ni muungano wa wanyonge. Migomo inayoshuhudiwa viwandani katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, kukataa na kusaili mahusiano ya mifumo ya kiuzalishaji kutokana na mwamko mpya wa kisiasa katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* na wazee kukubali kuwa mabadiliko ni jambo la lazima katika jamii lisiloepukika katika tamthilia ya *Chamchela* ni dhahirisho kuwa baada ya kutambua matatizo

yanayoleta migongano katika jamii, Suluhu litakalokuwepo ni kuungana na kuleta umoja. Kutokana na muhtasari wa kila tamthilia, jambo moja linabainika: shida zinazokumba nchi za bara la Afrika zaweza kusuluhishwa na Waafrika wenyewe kwani wanazielewa vyema.

2.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangalia historia fupi ya uandishi wa Arege ambapo tumebaini kuwa ameandika kazi mbalimbali katika utanzu wa fasihi. Tumechunguza tamthilia zilizoteuliwa kimuhtasari ili kutoa mwanga kwa maudhui anayoyawasilisha mwandishi. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, Mwandishi amejishughulisha na madhara yanayoletwa na uongozi wa kidikiteta ambao hujali maslahi ya wachache na kuwafaidi huku wengi wakiumia na kuteseka. Katika tamthilia ya *Chamchela*, mwandishi ameangalia jinsi migongano ya tamaduni mbili huzua mizozano isiyokadiriwa katika madhara yake. Matokeo yake ni kukosa maelewano ambayo husababisha maendeleo duni. Mwisho, ni tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ambapo mwandishi ametalii misingi ya mifumo ya kibepari iliyojikita kwenye nyenzo za uzalishaji mali barani Afrika. Ametalii mbinu kuu ya kukosesha maendeleo barani Afrika ambayo ni utekaji nyara saikolojia ya wakazi wa bara la Afrika na kuwafanya kuamini kuwa kadhia yao imeamuliwa na Mungu kwani liandikwalo ndilo liwalo. Hata hivyo tumebaini kuwa mwandishi anashughulikia masuala ya ukombozi kutokana na minyororo ya kijamii inayokwamiza maendeleo katika mataifa machanga. Imebainika kuwa Arege ametumia kinaya na kejeli kupitisha ujumbe kwenye tamthilia husika.

SURA YA TATU

MBINU ZA USIMULIZI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA AREGE

3.1 Utangulizi

Katika sura hii tumebainisha na kuchanganua mbinu za usimulizi alizotumia Arege katika tamthilia tatu zilizoteuliwa. Kusimulia ni kueleza jambo fulani kwa njia maalumu na yenye ubunifu. Mbinu kwa upande mwingine ni njia au maarifa ya kufanya kutekeleza jambo fulani. Hivyo basi mbinu za usimulizi ni maarifa ya kueleza jambo kwa ubunifu. Mwandishi wa kifasihi hutumia maarifa haya kuelezea ujumbe wake kwa njia ambayo huifanya ivutie na hatimaye kueleweka na kukubalika. Hii ina maana kuwa mbinu anazoteua na kutumia mwandishi katika kusimulia ujumbe wake huathiri namna ile kazi aliyoiandika itakavyopokelewa na hatimaye kutoa ujumbe wake kwa njia aliyokusudia. Hivyo basi uteuzi mwafaka wa mbinu za usimulizi ndio huwezesha uwasilishaji wa maudhui kwa mantiki na ufasaha. Kwa mantiki hii basi mbinu za usimulizi huwa uti wa mgongo katika kubainisha mtindo. Lengo letu ni kubainisha ubunifu wa mwandishi katika tamthilia teule na jinsi ulivyochangia katika uwasilishaji wa maudhui mbalimnali. Ili kufikia lengo letu, tumechunguza mtindo katika kiwango cha sintaksia.

3.2 Sintaksia

Sintaksia huhusiana na uundaji wa sentensi ili kukidhi mahitaji ya ujumbe unaowasilishwa. Sintaksia ni mbinu ya usimulizi ambayo hujihusisha na kuangalia miundo mbalimbali ya sentensi iliyotumika katika kueleza ujumbe. Ngara (1981) anairejelea sintaksia kama kategoria ya kisarufi ambapo aina za sentensi (pamoja na virai) na uhusiano kati ya maana na muundo huchunguzwa. Uteuzi huu umeongozwa na kiwango cha pili cha nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo ambacho huhusisha uchanganuzi wa aina za sentensi, uchangamano wa sentensi, aina za virai kama virai nomino na virai vitenzi.

Hii ndiyo sababu Wamitila (2008) anakirejelea kiwango hiki kama tamathali za sentensi. Anataja baadhi ya mbinu ambazo huchunguzwa katika kiwango hiki ikiwemo mdokezo, maswali ya balagha, usambamba n.k. Katika sura hii tumefafanua namna sentensi pamoja na virai vilivyotumiwa kiubunifu ili kumwezesha mwandishi kusimulia ujumbe wake.

3.2.1 Mdokezo

Kwa mujibu wa Senkoro (2011) mdokezo ni mtindo ambapo mwandishi hukatiza maneno au huacha kitu fulani bila kukitaja au maneno ambayo kwa kawaida ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu wa msomaji. Sentensi za mdokezo humsaidia msomaji kujua hisia za mhusika fulani na hivyo kuweza kutabiri maudhui yanayowasilishwa kwake na mwandishi. Matumizi ya mtindo huu yametawala katika tamthilia tatu teule kwa shabaha mbalimbali.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mtindo huu umetumika na watawaliwa na watawala mtawalia. Mara nyingi watawaliwa wanapotumia mdokezo huwa wamejawa na hofu kwa sababu ya kuwaogopa viongozi wao. Dida anaitikia wito wa Meya kwa utiifu lakini maswali anayoulizwa na Sosi yanasababisha hofu kiasi cha kushindwa kulitamka jina lake. Anasema ‘Mst... (uk. 9)’

Haya ndiyo matokeo ya woga wa wafanyikazi wa jiji ambao ni chanzo cha dhuluma zao. Woga huwafanya watumishi kunyenyekea ovyoovyo hata pale ambapo hawahitajiki kufanya hivyo. Woga unakuwa kiwango sawa na heshima. Dida anamwambia Meya:

(Anashangaa. Anajibu kwa upole.)
Mstahiki Meya...lipi lilioenda kombo?
Samahani sana... (uk. 9)

Dida anaomba msamaha kwa kosa asilolifanya kwa hofu aliyo nayo kwa Meya Sosi. Mwandishi anaonyesha kuwa mbinu mojawapo wanayotumia viongozi barani Afrika ili kudumisha utawala wao ni kuwakandamiza watumishi wao kwa kuwajaza woga ili waweze kuwadhulumu bila ya wao kulalamikia hali hii. Ni ubabedume wa viongozi wa nchi zinazoendelea.

Daktari Siki anagubikwa na hasira ya hali mbaya isiyotabirika kwa wanacheneo na uhitaji wao, na kila mara anapoelezea matatizo ya Cheneo hisia za hasira na masikitiko humfanya kukosa kukamilisha maelezo yake.

Diwani III anamtahadharisha Meya dhidi ya kuwanyanyasa wanacheneo ambao kwa mbali wanaonekana kuendelea kuishiwa na stahamala. Akionyesha hofu na hasira yake anasema:

... watu sasa wanataka vitendo,
si maneno. Tusi... (uk. 16)

Japo hili ni onyo kwa Meya kuwa anahitajika kuyashughulikia mahitaji ya wanacheneo kwa dharura, pia linaibua hisia za masikitiko kwa hali ya ulitima inayotawala Cheneo.

Hisia za Diwani III za hasira kwa kutowajibika kwa madiwani wenzake zinamfanya kushindwa kuelezea na kukamilisha usemi wake. Kwa kuwa anashtakia matatizo ya wanacheneo, Diwani III anaonekana kutumia mtindo huu sana anapooni haki ikinyimwa wanacheneo ambao wanateseka. Akipinga mawazo ya madiwani kuongezewa mishahara ilhali wafanyikazi wa Jiji la Baraza hawapati mishahara kwa wakati ufaao licha ya kuwa ni duni na unaocheleweshwa, anasema:

Mwezi huu Mstahiki Meya una
siku mbili tu. Tayari mishahara
imeisha kuandaliwa na... (uk. 52)

Meya anafahamu fika kuwa Diwani III hayuko tayari kutekeleza matakwa yake ya kuwaongeza vibarakala wake mishahara. Kwa kutaka kumwonyesha kwamba hayuko tayari kukabiliana naye, anamwamrisha kutekeleza agizo lake la kuwalipa mishahara pamoja na nyongeza madiwani wote. Diwani III anasikitikia hali hii kwa mdokezo huu:

Lakini... (uk. 52)

Mdokezo wa kwanza na wa pili unaonyesha kuwa Meya anaogopwa na watumishi wake katika baraza kama anavyodhihirisha Diwani III licha ya kuonyesha hisia za masikitiko kwa namna Meya Sosi alivyojawa na ubinafsi wa kifisi.

Gedi akimweleza Meya kuhusu wageni waliofika anaonekana kutwaliwa na hisia za woga. Anasema hivi:

Gedi: Mstahiki Meya *sir*, hamna ila
kuna wageni wanaotaka kukuona...
Meya: Wale wa kawaida...
Gedi: Sio hao. Bili... (uk. 58)

Mdokezo umetawala katika tamthilia zote na umetumika kumtafakarisha msomaji kuhusu ujumbe anaokuza mwandishi. Pia mdokezo humpa msomaji uwezo wa kutambua hisia za mhusika fulani na uhusiano wake na wahusika wengine katika tamthilia husika.

Katika tamthilia ya *Chamchela* matumizi ya mdokezo yanadhihirika kupitia kwa wahusika mbalimbali. Mayaka anamweleza Bisase ambaye ni mfadhili wake kuhusu habari alizopata zinazomtaka kuukata uhusiano wao kwa kusitasita. Anasema:

Kwa hivyo nawe unakubali kwamba...
kwamba... kwamba...kwamba... (uk. 40)

Mdokezo huu unaonyesha bayana kuwa Mayaka amegubikwa na hofu nyingi ambayo inamzuia kumwambia Bisase ukweli wa hali inayousibu uhusiano wao. Mwandishi ametumia mawazo haya kutufunulia mawazo ya Mayaka ana tashwishi ya uamuzi wa kumwoa Bisase. Anashindwa kumweleza kuwa yeye ndiye chanzo cha mtanziko anaoupata kwa kuwa anaogopa kumpoteza (Bisase) ambaye anayakimu mahitaji yake.

Katika kukejeli hali ya maisha ya vijana wasomi mwandishi ametumia mtindo huu wa tashbihi. Mazungumzo kati ya Rukia na Kofi yanatumiwa kusikitikia maisha ya vijana waliosoma lakini wanaoishi kwenye vibanda. Hii ni kejeli kwa nchi ambazo zimefuata utamaduni wa kigeni pamoja na elimu yao lakini haziwezi kuwapa vijana hawa kazi baada ya kuhitimu. Matamshi ya Rukia yanadhihirisha hali hii:

tunakaa kama...kama... kama nini.
vile sijui Pamoja na elimu yote hii ? (uk. 30)

Maneno yaliyodokezwa yanatokana na hali ya kusikitisha inayomfanya Rukia kushindwa kuelezea hali mbaya ya maisha wanayojipata licha ya kuwa na kisomo. Yanaonyesha jinsi wasomi hawa walivyokata tamaa. Rukia anatumia mdokezo huu ili kuchochea fikra za Kofa katika kuwazia hali duni wanayoishi licha ya kufuzu kutoka vyuoni.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, hali ni sawa ambapo pia mwandishi ametumia mtindo huu. Katika tamthilia hii, mhusika mkuu anaonekana kutumia mtindo wa kudokeza anapokuwa na woga au kutokuwa na hakika na hali fulani.

Daktari: Kama waiona kali basi acha
tukutie mkasi mkavu...
Sele: Si hivyo... (uk. 52)

Matumizi ya mdokezo yanatuashiria kuwa Sele ametawaliwa na woga na hana hakika kama anahitaji matibabu aliyopendekezewa na daktari au la. Akiendelea kuonyesha hisia za woga zinazomtawala, Sele anasema:

Nafhamu Daktari... (uk. 53)

Mwandishi anaonyesha jinsi Sele anavyoyashuku matibabu yanayopendekezwa kwake na daktari. Hofu inaonekana kuongezeka kila mara anapozungumza na daktari. Kabla ya kuraiwa na daktari kupanda kitandani baada ya kumdadisi, Sele anaendeleza mjadala ambao unamkasirisha daktari wake. Anamuuliza, ‘Tayari lakini...’(uk. 57)

Mdokezo unaotawala katika tamthilia hii mara nyingi unadhihirisha ukosefu wa hakika kwa wahusika kama Sele. Udadisi kwa madaktari ni ishara ya woga wake Sele na kutokuwa na hakika ya matibabu yao. Hii ndiyo sababu inayomfanya akose matibabu mwishowe.

Baada ya kuchunguza mtindo huu, tumebaini kuwa mdokezo umetumiwa na mwandishi ili kuhusisha nadhari ya msomaji katika kuelewa maudhui yanayokuzwa. Aidha, mtindo huu umetumiwa na wahusika ili kuchochea hisia na kuamsha ari ya msomaji katika kutoa uamuzi faafu.

3.2.2 Maswali ya balagha

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) balagha ni dhana inayoelezea sanaa ya usemaji na mbinu ya uwasilishaji wa usemi kwa njia ya kushawishi na kuathiri msikilizaji (msomaji). Huu ndio msingi wa mbinu ya balagha kwa kuwa maswali yanayoulizwa hayahitaji majibu kwani jibu lake linafahamika kwa uwazi na wahusika. Kuhenga (1977: 48) anaelezea balagha kuwa:

Ni msemu wa tashtiti ambao kwao mwandishi au mhatibu kwa madhumuni maalumu ya kuingilia mahasa ya ndani au kuchipua maoni ya wasikilizaji, hutoa hoja za kulisimua au kuuliza maswali ya kuchoma moyo, na ambayo huchochea furaha,

huzuni, chuki au mzinduko wa utendaji ili kumshawishi mtu atende jambo fulani zuri au baya.

Kutokana na maelezo ya Kuhenga, tunafahamu kuwa nia ya maswali ya balagha ni kuchochea hisia kwa anayeelekezewa swali bali sio kupata majibu kwa swali hilo. Ndiposa Holman (1976) anasema kuwa mtindo huu hulenga kumshawishi msikilizaji (msomaji) kwa kumpa changamoto ya kuyatafuta majibu ili asiwe msikilizaji (msomaji) tu bali pia mshirika katika mchakato mzima wa mawasiliano. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mtindo huu pia umetumiwa na wahusika kwa malengo tofautitofauti. Daktari Siki akihofia wazo la uhakika la Waridi wa dawa zinazosubiriwa, anamuuliza:

Wakisubiri ugonjwa nao utasubiri?
Hujui ngoja huumiza matumbo? (uk. 3)

Kinachodhihirika wazi ni kuwa Siki anataka kumwonyesha Waridi kuwa haelewi mbinu anazotumia Meya kudumu katika uongozi wake (ahadi za uongo) na pia kumchochea kuchukua hatua ya kuwashughulikia wagonjwa kwa njia yoyote itakayowaacha na matumaini ya tiba.

Diwani III akieleza ni kwa nini wanacheneo wanastahili kujilaumu wao wenyewe kwa majanga yanayowafika, anamwuliza Siki:

Usishangae. Mmetuchagua nyinyi.
Kama hujui, viongozi ni picha ya
umma uliowachagua. Ya nini kulia? (uk. 51)

Swali la balagha analouliza Diwani III linaonyesha kuwa wanacheneo hawastahili kulalamikia madhila wanayotendewa na viongozi wao. Hii ni kwa sababu wao ndio waliowatwika majukumu wanayoshikilia katika sekta mbalimbali. Ni kama Diwani III anaunga mkono methali ‘mwiba wa kujidunga hauna kilio’. Mwandishi analenga kukejeli wananchi ambao huwachagua viongozi wabaya wasio na uwezo wa kuleta maendeleo halafu nyumaye huanza kulalamika wanaposhindwa kutekeleza wajibu wao. Diwani I akithibitisha sifa yake kuu ya ubarakala kwa Meya, anamwuliza swali hili:

Upo wakati ulinituma nikashindwa
kumwinda ndege wako nikakuletea
mpaka jikoni? (uk. 60)

Diwani I ni mmojawapo wa vikaragosi anaowaamini Meya katika kuendeleza udikteta wake. Swali hili lililenga kumhakikishia Meya kuwa ukupe wa Diwani I ni imara na thabiti ili asiwe na hofu ya kutekelezewa matakwa yake ya kuendelea kuwakandamiza wanacheneo anaostahili kutetea maslahi yao.

Tatu ambaye anawakilisha wafanyikazi wa jiji la Baraza akilalamikia hali mbaya ya kiuchumi iliyoziidi kudorora kila uchao, anamweleza Meya haya:

*(Kwa Meya.) Sisi wafanyakazi tuna
matatizo mengi yaliyotuzonga kwa
muda mrefu. Kwanza mishahara yetu
ni midogo. Ni lini mara ya mwisho sisi
wafanyakazi wadogo tulipata nyongeza? (uk. 68)*

‘Ni lini mara ya mwisho sisi wafanyakazi wadogo tulipata nyongeza?’ ni swali la balagha ambalo linaelekezwa kwa Meya ili kuonyesha jinsi ubinafsi wake na wa washauri wake ulivyomzuia kutetea haki za wafanyikazi wa jiji la Baraza. Swali la balagha la Tatu linaonyesha kuwa chanzo cha matatizo ya wanacheneo ni mishahara duni tena isiyolipwa kwa wakati ufaao. Mhusika mwingine, Beka ambaye pia ni mmojawapo wa wawakilishi wa wafanyikazi anachochea hisia za Tatu akisema:

*... Sababu ya nyongeza zenu? Gharama
ya maisha inapanda kila uchao, mara
mfumko wa bei. Hiyo gharama inapanda
kwenu tu? Huo mfumko unawafumkia
nyinyi tu? (uk. 68)*

Matumizi ya ‘Sababu ya nyongeza zenu?’ Hiyo gharama inapanda kwenu tu?’ na ‘Huo mfumko unawafumkia nyinyi tu?’ ni balagha kwa sababu hakuna majibu yanayohitajika bali zinatekeleza dhima ya kumzindua mhusika (Meya) ili ashawishike kuwa hali ya wanacheneo ni mbaya na yanahitaji kushughulikiwa kwa dharura. Mtindo huu unasaidia kufafanua jinsi maudhui ya ubinafsi yalivyotawala katika tamthilia. Ubinafsi ndio chanzo cha matatizo ya jamii ya Cheneo. Maswali haya yanaweka wazi hali mbaya ya wakazi wa Cheneo ambao wanaishi katika umaskini.

Akiendelea kulalamikia hali duni inayowasibu Wanacheneo na hasa wafanyikazi, Tatu anamlalamikia Meya akisema:

... Kuna raha gani watoto wetu wana-
pofukuzwa shule kwa sababu hatuwezi
kuwalipia karo? Kuna raha gani kutazama
watoto wetu kufa taratibu mikononi mwetu
kwa sababu hatumudu gharama ya matibabu?
Tena katika hospitali ya mwajiri wetu? Hospitali
hiyo imejengwa na nani kama si sisi waajiriwa wake? (uk. 70)

Maswali haya yote ni balagha kwani hayahitaji majibu kwa kuwa ni wazi kwa wahusika na msomaji wa kazi hii. Maswali ya balagha yameelekezwa kwa Meya ili kumchoma na kumshawishi aweze kuchukua hatua zitakazosaidia kusuluhisha shida zinazowakumba wanacheneo. Kwa njia hii mwandishi anamleta msomaji karibu na kuhisi hali ya wahusika na kuhuzunika nao katika majanga yanayowakumba. Mwandishi ametumia mtindo huu kuonyesha kuwa majonzi yote ya wanacheneo yanasababishwa na uongozi duni wa Meya na washauri wake wenye tamaa na ubinafsi.

Meza akionyesha hofu yake ya kushtakiwa na mwanakandarasi aliyemfuta kabla ya muda wake kukamilika anamkabili Bili ambaye ni mshauri wake kwa swali hili:

Ajidungaye mwiba hufaidi nini Bili? (uk. 29)

Methali inayojitokeza katika swali la Meza ina maana kuwa mtu anayejitia matatani hujilaumu mwenyewe kwa maafa yanayomfika. Meza akitumia methali hii katika swali balagha analenga kuonyesha kuwa hayuko tayari kujitia kwenye shida za kujitakia kwa kuwa hatafaidi kwa lolote. Ingawa Bili anamshauri na kumwelezea atakavyoshirikiana na mwanakandarasi ili wote wafaidi, ni wazi kuwa Meza anahofia sifa yake kuharibika kwani hataki kung'atuka uongozini. Hii inaonyesha chanzo cha kudidimia kimaendeleo katika nchi maskini kwani viongozi huchukua hatua ambazo huwawezesha kunufaika wao na vibarakala wao dhidi ya wengi walio maskini kupindukia.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, mtindo huu umetumiwa na wahusika wakuu kwa wajenzi katika kukuza ujumbe wa mwandishi. Aisha katika kuhalalisha hofu yake kwa mabadiliko yaliyompata Sele, anamuuliza:

...Ni makosa kuuliza chanzo cha hali
hiyo? Si wewe uliyezipenda ngoma
mpaka ukawa wa kujisahau? Ukakesha

chee ulingoni! Hivi umekuwa kinyonga
wabadilika kila utakapo? (uk. 11)

Maswali ya Aisha yanaonyesha wazi mbanduko katika maisha aliyoyapenda na kuyazoea Sele. Maswali haya yanaonyesha kuwa wahusika hawaelewi kuwa Sele amepata mwamko mpya wa kisiasa. Katika kuwahakikishia kuwa japo yeye na wahusika wanaomwona mgonjwa wako kwenye tabaka la wanyonywaji anamuuliza Zainabu:

Tuseme mimi naumwa na nyinyi
kuhisi maumivu? (uk. 42)

Swali la Sele linalenga katika kukejeli nafsi za wahusika ambao wanamwona kuwa mgonjwa kutokana na mawazo yake. Mawazo yake yanapinga njama za mfumo wa kibepari unaonyonya wakazi wa mataifa ya Afrika katika rasilimali zao. Anakejeli nafsi hizi na kuziona kuwa zinahitaji kujidadisi kwani hazijapata mwamko wa kuona hali duni ambazo zimejiri katika maisha yao.

Aisha amechanganyikiwa na hali ya Sele. Mawazo haya yamemfunga kiasi cha kusahau kuwaamkua Zainabu na Bi. Rahma. Bi Rahma ambaye kitambo ashaona hili analalamikia hali hii ya kukosa adabu kwa Aisha:

...Aisha desturi gani hii? Mtoto utoke
kule nje sisi wazee wako tuko hapa
kisha utupuuze na kuelekea kwenye
vitabu! Ndivyo elimu yenu hii ya
Kizungu inavyowatuma kufanya?
Huo ndio ustaarabu kwenu? (uk. 18)

Maswali ya balagha anayoyauliza Bi Rahma yanaonyesha kuwa ameghadhabishwa na mwenendo wa Aisha. Kupitia kwa maswali haya tunabaini kuwa ukengeushi unawapata vijana baada ya kupata elimu iliyoambatana na mila za kimagharibi. Kwa maswali haya ya balagha, Bi Rahma alinuia kuonyesha kuwa utamaduni wa kimagharibi hauna ustaarabu kama ulivyo wa Kiafrika. Hii inaonyesha chanzo cha migongano katika jamii kwani wazee wanaiona elimu ya kimagharibi kama inayowanyima vijana adabu kwa wazee.

Bi. Rahma katika kumwonya Sele dhidi ya kupinga nguvu hizi za kibepari zilizonyonya kwa ukatili nguvu za wakazi wa nchi za ulimwengu wa tatu, anasema:

Wahenga wanasema, Mwenye
nguvu mpishe! Sasa utapigana
nao? Usiloliweza unaliacha.
Unafungua ukurasa mpya. (uk. 29)

Bi. Rahma anamtahadharisha Sele dhidi ya kupigana na wenye nguvu wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali kwani anaona hili kuwa hatari kwake. Swali hili linaonyesha kuwa wanyonge wameridhia hali yao ya unyonge kwani wana imani kuwa hawawezi kupigana na matajiri walio na uwezo. Kuchelea huku kwa wanyonge kulikojengeka ndani ya woga ndiko kukowapa nguvu mabwanyenye katika kuwatumikisha kikatili kuzalisha mali katika jamii na kujitajirisha dhidi ya wengi walio maskini.

Sele katika kuonyesha ufahamu wake wa njama ya mifumo ya kibepari katika mataifa machanga, anajiuliza:

Mimi ni nani?
Nimekuwa wapi?
Niko wapi?
Ninakwenda wapi? (uk. 96)

Haya ni maswali anayojiuliza Sele katika uzungumzi nafsia wake. Maswali haya yanalenga katika kuchochea hisia za wakazi wa nchi za ulimwengu wa tatu ili wawazie upya hali zao. Hii ni njia moja itakayowawezesha kubaini waliko kwenye misingi ya kijamii na kiuchumi na jinsi wanavyoweza kutatua vizingiti vinavyokwamiza maendeleo ya nchi zao. Anaendelea kujisaili akisema:

...Kwa nini watoke kwao kunijia?
Je, wao hawana wagonjwa kwao? (uk. 96)

Maswali haya yanaamsha ari ya kutaka kusaili upya kuwepo kwa mabepari wa kikoloni katika mataifa ya Afrika. Maswali anayojiuliza Sele yanaonyesha wazi kuwa wakoloni hawakuja Afrika na nia ya kuleta maendeleo kwenye misingi ya kiutu. Wakoloni hawa walifika katika mataifa ya Afrika kwa nia ya kuhodhi mali na kujiendeleza kiuchumi huku wakiwatumikisha wakazi wa Afrika katika kuwazalishia mali.

Tamthilia ya *Chamchela* imeendeleza matumizi ya mtindo huu kwa njia mbalimbali. Mtindo huu umetumiwa na wahusika wote mtawalia, vijana kwa wazee. Kwa mfano,

Sure akimshawishi Atisa kuwa maamuzi ya Mayaka ya kutaka kumwoa Bisase ni kinyume na utamaduni wao, anasema:

Mwanangu ushawahi kuona au
kusikia ugonjwa ukibisha? (uk. 2)

Mwandishi anaonyesha kuwa maamuzi ya Mayaka ambayo hayakubaliani na itikadi za Kiafrika kwenye misingi ya ndoa ni sawa na ugonjwa kwa kuwa kunahitajika suluhu kutokana na umoja wao wote. Anaendelea kusema:

Tangu lini ukaona watu hapa
kijijini wakimwambaa mgonjwa? (uk. 2)

Maswali ya Sure yanalenga katika kuchochea hisia za Atisa katika kusaidia kupata suluhu la mgogoro uliopo. Ingawa Mayaka amefanya maamuzi yanayopingana na kanuni za utamaduni wao, yeye anasalia kuwa mmoja wao. Lengo la mwandishi ni kuonyesha kuwa utamaduni wa Kiafrika unaenzi itikadi zake za ujamaa. Katika kuweka wazi wazo la umuhimu wa jamii, anaendelea kumweleza Atisa hivi:

...Si suala la mtu mmoja! Ndoa
haiwi bila baraka za jamii. Je,
jamii haikumfunda na kumtunza? (uk. 3)

Swali la Sure halihitaji jibu kwani ni balagha. Sure anatumia swali hili kuonyesha uchungu na hasira yake kwa uamuzi aliouchukua Mayaka wa kumwoa Bisase kinyume na matakwa ya jamii. Lengo la mwandishi ni kuonyesha kuwa utamaduni wa Mwafrika unaipa jamii kipaumbele tofauti na ule wa Kimagharibi ambao unampendelea mtu binafsi na si jamii.

Rosa akilalamikia na kuonyesha kutoridhishwa na uamuzi wa Mayaka, ananukuliwa akisema:

Itakuwa vipi mtu anayekushinda
umri kukuita ma mkwe? Eti nami
nimridhie kuwa mkaza mwana? ... (uk. 9)

Maswali haya yanaonyesha hasira za Rosa kwa Mayaka kwani ameenda kinyume na matakwa ya jamii yao. Sure akijaribu kumweleza kuwa anayoyafanya Mayaka si mageni kwani yametendeka kwingine, anatamka hivi:

... Na yule pale? tazama kucha
zake. Je, hazina mipako ya rangi? ... (uk. 10)

Maswali ya Sure yanalenga kuwafahamisha wanaokataa mabadiliko yaliyofika kuwa hawatafaulu kwani hili ni jambo ambalo limefika kudumu katika jamii. Maswali haya ni dhihirisho la ukengeushi kwa vijana. Maudhui haya yanaendelezwa na wahusika wengine ambao wanauliza maswali yenye ushahidi wa ukengeushi wa vijana. Bisase analalamikia kutowajibika kwa Sera katika kumtunza mwanawe Lema anaposema:

(Kwa hasira) Shughuli gani nyingi? Shughuli zisizoisha wala kuzalisha kitu? *(kakasirika)*
Wewe uondoke wende hizo shughuli zako na kuniachia mzigo wako! Mzazi gani asiyejua haja na mahitaji ya mtoto wake? Eeh? Niliku-
lea wewe kwa mikono hii yangu. Tena nimlee mtoto wako wewe? (uk. 18)

Maswali haya yanaonyesha kiwango kikubwa cha hasira ya Bisase kwake Sera katika utepetevu wa kutekeleza majukumu yake kama anavyostahili mzazi kwa mwanawe. Maswali haya yanaonyesha kuwa vijana waliovutwa na mila za kimagharibi kama Sera wamesahau kuwajibikia majukumu yao katika familia. Matamshi haya yanaendeleza maudhui ya ukengeushi katika jamii kwani vijana wameandama desturi na mienendo ya Kimagharibi. Lema, ili kudhihirisha ukweli wa tetesi za nyanyake, anauliza maswali yafuatayo:

Lakini mbona yasinitie? Wakati kila mtu anatoa maelezo kuhusu kazi wanazofanya wazazi wao, mimi simjui babangu na mama namwona mara moja moja. *(Kwa huzuni)*
Haya si maonevu? Yaani ni mimi tu sijielewi? (uk. 15)

Maswali ya Lema yanaonyesha kuwa utamaduni wa Kimagharibi umekuza ubinafsi miongoni mwa wanajamii kiasi cha kusahau kuwajibikia majukumu yao kama malezi ya wanao. Mayaka akitetea uamuzi wake wa kumwoa Bisase licha ya kwamba anamzidi kiumri na hata ule wa Rosa, anauliza maswali ya balagha. Anauliza maswali haya:

...Mama alipokuwa akiunga mkono uolewe na yule mzee, kwa nini hakuona vibaya? Kwa nini kwangu aone vibaya? (uk. 73)

Mwandishi anaonyesha vijana wanaona hitilafu fulani kwenye itikadi zinazolazimishwa kwao na wazee na hivyo wako tayari kuzitumia katika kuhalalisha maamuzi ambayo wamechukua. Kinachoonekana ni kuwa badala ya kuwahukumu vijana kuwa wana hatia, wazee wanahitaji kuchukua hatua ya kuelewa chanzo cha misimamo yao ili waweze kuwafunza wanayotaka na kuridhiana nao.

Kutokana na matumizi mengi ya balagha tumebaini kuwa mara nyingi zimetumika ili kuonyesha hisia za hasira kwa wahusika walengwa katika kupuuza majukumu na nafasi zao katika miktadha mbalimbali. Hata hivyo maswali ya balagha yamesaidia kuendeleza ujumbe wa mwandishi kwa njia kwani unamshirikisha msomaji katika kuufumbata ujumbe huo.

3.2.3 Kuchanganya Ndimi

Kuchanganya ndimi huhusu kutumia msamiati kutoka lugha nyingine katika maendelezo ya lugha ya jamii husika. Kulingana na Spolsky (1998), kuchanganya ndimi huhusisha matumizi ya maneno au sentensi zenye muundo ambao umevunja kaida za lugha husika. Hali hii hutegemea: uwezo wa kumudu lugha alionao mzungumzaji, mada inayojadiliwa, mazingira ya lugha tumizi, ujumbe unaokusudiwa kupitishwa na uhusiano uliopo baina ya wanaowasiliana. Arege amedhihirisha matumizi ya kuchanganya ndimi ndimi katika tamthilia zake ili kuibua na kuendeleza maudhui yake.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mbinu hii imetumika na wahusika ili kukuza maudhui mbalimbali aliyodhamiria mwandishi. Mhusika anayetumia mtindo huu kwa wingi ni Mstahiki Meya pamoja na washauri wake na wafanyakazi wa Baraza. Mara nyingi Meya huwasiliana kwa kuchanganya ndimi anapopatwa na hasira. Akionyesha hasira zake kwa chamsha kinywa alichandaliwa na Gedi, anasema:

*(Akijisemea mwenyewe huku akila na
kunywa) Viyai vidogo... (Analiangalia
yai mojawapo) Bloody hens ... Nonsense!
(Kimya) (uk. 9)*

Gedi naye anapoitwa anaitikia kwa ‘Yes sir!’. Matumizi ya mbinu hii na Gedi pamoja na Mstahiki Meya yanadhihirisha chembechembe za ukoloni mamboleo. Mpambe wake Meya anatumia mtindo huu pia kuonyesha kuwa viongozi huwakengeusha watumishi

wao wanapotagusana. Baada ya Meya kukutana na Siki ambaye amefika kushtakia hali duni ya wanacheneo, anakasirishwa na matamshi ambayo anayaona kuwa ni tishio kwa uongozi wake. Anamfukuzilia mbali Siki na kumwamrisha Gedi asimruhusu kuingia kwake tena:

Gedi: (*Anarudi mbio. Anapiga saluti.*) Sir!

Meya: Hakikisha mtu huyo halikaribii lango kuu kuanzia sasa. Jengo hili alione paa *Alright?* (uk. 15)

Matamshi haya yanaonyesha hasira alizonazo baada ya kuambiwa ukweli unaotishia uongozi wake na Siki. Haya ni maendelezo ya maudhui ya udikteta kwa viongozi wa nchi changa za bara la Afrika ambao hujihisi kuwa na uwezo usiotetereka katika kuendesha miliki zao wpendavyo pasina kujali umasikini uliogubika wananchi wao ambao wanadai kuwaongoza.

Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* imeangazia matumizi ya mbinu hii kwa njia mbalimbali. Mtindo huu unajitokeza kupitia mazungumzo ya wahusika katika tamthilia hii. Aisha akirejelea mahala pa kustarehe bila malipo, anamwambia Sele:

Sisi hatwendi *private beach*. Twenda *public beach* kama tulivyokuwa tukifanya tangu zamani. (uk. 3)

Sele akiendelea kumtahadharisha kuhusu hatari kwenye bahari, Aisha anamjibu kwa kuchanganya ndimi akisema:

Life savers si wako lakini? (uk. 4)

Mwandishi ametumia mbinu hii kwa madhumuni ya kuelezea uwezo wa kiuchumi wa Sele na Aisha kuwa ni wa kadiri na ndio sababu hawamudu kuweza kuenda katika ‘private beach’. Aidha, matumizi haya ni dhahirisho tosha la ukengeushi kwa Waafrika kutokana na ukoloni mkongwe.

Jamila akimweleza hali yake kiafya anachanganya ndimi. Anamweleza Sele:

Jamila: 144 kwa 91.

Sele: Hivyo ndio nini?

Jamila: *Pulses* zako si mbaya
wala *pressure*. *Border line*. (uk. 62)

Matumizi ya kuchanganya lugha yanadhihirisha utaalumu katika taaluma ya utabibu.

Katika tamthilia ya *Chamchela*, mtindo huu umejitokeza katika viwango mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi ipasavyo. Rukia akisikitikia hali duni wanayojipata vijana baada ya kuhitimu masomo ya shahada ambayo huwalazimu kuwa wategemezi kwani hutaraji kuajiriwa kwa kazi ambazo hazipo.

...unaona maisha yetu sisi
kilele ni kuishi katika
servant quarter?... (uk. 30)

'*Servant quarter?*' ni msamiati wa Kiingereza uliotumika katika Kiswahili. Mwandishi ametumia mbinu hii kudhihaki elimu ya uzungu ambayo huwafanya vijana kutaka kuwa na kazi za ofisi ambazo ni za kutegemea wala si kuvumbua. Na hili ndilo janga linalodhirishwa kwenye nchi za bara la Kiafrika ambazo huandama elimu isiyofaa ambapo vijana hawawezi kuvumbua kwani wana elimu ya kinadharia tu. Matokeo yake ni utegemezi usio kikomo kwenye nchi za kimagharibi. Hali kama hii huzalisha maendelao duni katika nchi za ulimwengu duni.

Pia Bisase anachanganya ndimi anapotaka kujua msimamo wa Mayaka katika uhusiano wao wa ndoa uliopingwa vikali na jamii yao:

... Mbona unapenda kunizungusha?
Nionavyo utanipandisha *pressure*
bure wewe! (uk. 44)

Bisase anatumia neno '*pressure*' kuonyesha kughadhabishwa na maelezo ya Mayaka ambayo yanadhihirisha kutokuwa na hakika katika uamuzi wake wa kumwoa. Amekasirishwa na utepepetevu wa Mayaka katika kufanya uamuzi thabiti.

Matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha ukengeushi kwa wahusika kutokana na mtagusano na utamaduni wa kigeni. Utamadunni huu una mila na desturi zilizo tofauti na zile wanazotakiwa kufuata katika jamii zao. Hii ndiyo sababu kuu ya vijana kujipata katika mtanziko wa kufanya maamuzi maalumu na yenye manufaa katika maisha yao.

3.2.4 Uzungumzi Nafsia

Wamitila (2003) anaeleza kuwa uzungumzi nafsia ni maongezi au hotuba ndefu inayotolewa na mhusika mmoja ili kukuza tendo kuu la hadithi. Wahusika mbalimbali katika kazi za fasihi huweza kujikuta katika mtanziko fulani unaowapelekea kuwa na mtindo huu wa kuwasilisha hisia zao. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, uzungumzi nafsia unajitokeza mara moja tu lakini katika onyesho zima. Japokuwa ni mara moja, unamsaidia msomaji kuelewa tamthilia hii kwa kina kwa kuwa umejitokeza kwa urefu. Uzungumzi nafsia huu unatupa picha halisi kuwa ugonjwa wa Sele si ugonjwa wa hospitali bali ni mwamko mpya wa kisiasa alioupata. Ni huu mwamko mpya wa kisiasa uliomwezesha kutalii mahusiano baina ya mataifa ya Afrika na mfumo wa kibepari unaopata nguvu zake katika ukoloni. Ugonjwa huu ndio tunaokumbana nao katika tamthilia Hussein ya *Mashetani* na *Marejeo* ya Chacha. Kitaru, mhusika mkuu wa Hussein na Muniko wa Chacha wanatafutiwa madaktari kutokana na ‘magonjwa’ ya mwamko mpya wa kukosa kukubaliana na unyonywaji wa kibepari katika janibu zao.

Kupitia kwa uzungumzi nafsia wa Sele, mwandishi anatumulikia njama za washika dau wa mfumo wa kibepari ambao huonekana kuwasaidia wakazi wa mabara fukara kwa nje. Japo hivi ndivyo wanavyojionyesha, lengo lao hasa si kuwapa nafuu wakazi wa mataifa haya bali kuwafilisisha zaidi kwa kuzinyonya kwa rasilimali zao. Mwandishi anatumia mtindo huu kama mbinu ya kutafakarisha nafsi za wakazi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu kuwazia upya hali yao ya kimaskini iliyochangiwa na mfumo huu wa kibepari. Haya ndiyo maswali anayotaka tujiulize:

...Wao ni nani?
wanatoka wapi?
Wananuia kwenda wapi?
Wananitoa wapi?
Wananipeleka wapi? ... (uk. 96)

Katika tamthilia ya *Chamchela*, kuna wahusika mbalimbali ambao wanajihusisha katika uzungumzi nafsia. Kwanza, tunakumbana na Bisase akijiongelesha. Kupitia kwa uzungumzi nafsia tunafahamu kuwa Bisase ni mjane na amempenda Mayaka ambaye ni mkembe kwani anamzidi umri. Pia uzungumzi nafsia wake unatufahamisha changamoto wanazokumbana nazo wajane katika jamii, za kutokubalika na kutothaminiwa. Wao huachwa katika upweke bila mtu wa kuwasaidia katika mahitaji yao. Anasema:

...Ujane ni adhabu.
Unakutia minyororo ya ukiwa
ilimradi mwenzio kakuacha...
...Kisha kuna hawa uliowaleta
ulimwenguni wasiokujali wala
kubali... (uk. 13)

Pili, tuna uzungumzi nafsia wa Atisa. Atisa anaeleza kiini cha mgogoro wa tamthilia hii ambacho kipo kwenye mapenzi. Anaona mapenzi ni kupenda na kuchukia kwani ndiyo chanzo cha misukosuko ambayo inawakumba wahusika takribani wote tamthiliani. Mayaka amempenda Bisase na anafurahi. Jamii yake yote inapinga uamuzi wa Mayaka kwa misingi ya kutokubalika katika mila za utamaduni wa Mwafrika. Mkinzano huu unamfanya kuyaita ‘pande mbili za sarafu moja.’ Anaonyesha kuwa mapenzi yanakuwa mgogoro mzito kutokana na ubinafsi wa wahusika ambao wamejiamini na kushikilia misimamo yao kwa kiburi kinachozuia maelewano. Tunaambiwa hivi:

... Na ubinafsi wake
Ubinafsi uliochochewa na kiburi
Kiburi cha kujiamini
Na kuamini katika nafsi yake
Moyo wake hasa... (uk. 57)

Kinachobainika katika usemi huu wa Atisa ni kuwa ubinafsi wa kujiamini ndio chanzo cha migogoro ya kijamii kwani unawafanya wahusika kutowasikiliza wengine wanapotoa maoni yao. Mgogoro mkuu wa tamthilia hii umekosa kusuluhishwa kwa msingi huu wa kutoshauriana.

Atisa ndiye aliyetwikwa jukumu la kumkabidhi Mayaka habari za maamuzi ya wazee wao ambao waliishakataa ndoa kati yake na Bisase. Atisa ana hakika kuwa Mayaka hatamsikiliza kamwe. Hali hii inamtia katika mtanziko kwa kuwa wazee wanamtumainia yeye katika kusuluhisha mgogoro huu. Anajisemea:

...Hata ukishindwa bado wanakutumainia
Na mwenyewe una hakika. Dau mbele
haliendi... (uk. 63)

Uzungumzi nafsia wa Atisa unadhihirisha kuwa anajua ugumu uliopo katika mawazo ya wazee kufanikiwa na kukubalika miongoni mwa vijana. Anafahamu kuwa hawatafaulu

kumzuilia Mayaka kumwoa Bisase licha ya kuwa anamzidi umri. Anajua hili kwa kuwa anafahamu msimamo thabiti wa Mayaka katika maamuzi wake.

Mayaka ambaye ni nguli wa tamthilia ya *Chamchela*, anajiongelesha. Kutokana na uzungumzi nafsia wa Mayaka, tunafahamu kuwa chanzo cha vijana wenye umri mdogo kuingia katika ndoa na wachumba waliowazidi umri ni utajiri. Mayaka anatoka kwenye aila maskini na Bisase anayo miliki kubwa aliyoachiwa na hayati mumewe. Mvutano unatokea kwa hili, kwani wahusika wengine wanamtazama Bisase na kumkana kwa misingi ya umri huku Mayaka akimtazama kwa misingi ya kiuchumi. Hii ndiyo sababu yake kusema hivi:

...Bisase! Mfadhili wangu wakati
kidau changu cha maisha kilitishiwa
na mawimbi...(uk. 39)

Maneno ya Mayaka yanaonyesha kuwa mvuto wake mkubwa kwa Bisase unatokana na ufadhili wake. Ufadhili huu aliupata wakati alikuwa katika hali ngumu iliyochochewa na ulitima aliuacha hayati babake.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, kuna wahusika mbalimbali ambao wanajihusisha katika uzungumzi nafsia. Meya akiwa kwake anajiandaa kupata chamsha kinywa alichandaliwa na mpambe wake, Gedi, analalamika kwa kuandaliwa viyai vidogo. Katika hali ya kujisemea hasira zinamjaa na anawaita kuku walioyataga mayai yale madogo 'bloody hens'. Hii ni ishara ya kukasirika. Hasira zake zinadhahirika wazi kutokana na kutoridhishwa kwa chamsha kinywa alichandaliwa. Analalamika akisema hivi:

...Viyai vidogo... Bloody hens
... Nonsense! (*Kimya*). Hivi huyu
ana nia gani? (uk. 8)

Matamshi haya ya Meya yanaonyesha kuwa kapandwa na hasira sana licha ya kuwa mlafi. Meya tena anakuwa na uzungumzi nafsia akiwa ofisini mwake ambapo anajisemea haya:

... shwari kabisa. Nitawapa mapokezi
ya kupigiwa mfano. Hoteli ya kifahari.

Vyakula kutoka kila utamaduni duniani.
Si sembe. La hasha! Mvinyo nitauagiza
kutoka Urusi na divai kutoka Ufaransa... (uk. 25)

Uzungumzi nafsia huu unabeba ujumbe wa mwandishi na kuupitisha kwa njia ya mnato zaidi. Kutokana na jinsi anavyoelezea Meya, tunabaini kuwa ukoloni mkongwe bado ungali katika mataifa ya Afrika licha ya kudai kuwa yako huru. Mwandishi ametumia uzungumzi nafsia huu kuwakejeli viongozi mataifa ya Afrika ambao licha ya wananchi wanaowaongoza kuishi katika ulitima na uhitaji mkubwa, wanaweza kuwapa mapokezi ya kifahari wakoloni wanaowafadhili. Ukuruba huu unajionyesha katika tamthilia ya *Amezidi* ambapo mwandishi anawakejeli wahusika wake Ame na Zidi ambao wanaishi katika pango. Licha ya kuonyesha uhitaji mkubwa katika maisha yao, katika onyesho linalofuata wanajikuta katika utajiri usiokuwepo na wa vyombo vya thamani vyote vilivyoagizwa kutoka nchi za kigeni. Huu ni ubadhirifu wa rasilimali ambazo zingeweza kuwafaa wakazi wao ambao wanadidimia katika ulitima usiokadirika.

Meya ni kiwakilishi cha viongozi ambao hutumia misaada wanayopokea kwa njia mbaya pasina kunufaisha wananchi walio masikini. Misaada inayopewa mataifa haya fukara, haitumiwi kuyaendeleza bali kuwateka nyara viongozi hawa ambao huburura mataifa yao kwa ufukara zaidi kwa kuitumia kujionyesha. Meya anatumia misaada hii kuwaandalia wafadhili wake mapokezi ambayo yamezidi uwezo wake ilmradi aonekane mkarimu. Mwandishi anasisitiza kuwa maendeleo hayatapatikana katika kutegemea misaada ambayo Mohamed anaiita ‘paja lililooza’ bali katika kuwaza na kutenda haki. Aidha, mwandishi anadhihaki uwajibikaji duni unaoonekana kwa viongozi katika mataifa machanga.

Siki akiwa ofisini anapokea simu kutoka kwa Tatu ambaye ni mwakilishi wa wafanyikazi wa Baraza. Ujumbe wa Tatu unamfanya kuwaza na kuanza kujisemea hivi:

... njaa ina nguvu
Imeangusha miamba
Wenye mengi maguvu
Matata yakawakumba... (uk. 34)

Uzungumzi nafsia wa Siki unatufanya tuhisi kuwa hali si shwari kwani anakumbukia alivyomshauri Meya kuwajibikia maslahi ya wafanyikazi ambayo hayakuafikiwa kwani

Meya alidanganywa na vibaraka waliomfanya awatendee unyama wanacheneo ambao walimwamini kuyashughulikia maslahi yao. Matatizo yasiyosuluhishwa yanaonekana kuwanyima wafanyikazi subira na huishia kufanya migomo. Mwandishi anaonekana kuisitiza kuwa ujinga wa viongozi barani Afrika ambao ndio chanzo cha wao kuyapuuza mahitaji ya kimsingi ya wananchi, ndio utakaowaunganisha wanyonge na kuwavua viongozi hawa mataji yao.

Meya anakataa kukutana na wafanyikazi wa Baraza waliogoma baada ya kusikia sauti zao. Akiwa ofisini mwake, anayakumbuka mawaidha ya Diwani III alivyomsihi kuona umuhimu wa kuwajali wanyonge na kusuluhisha matatizo waliyolalamikia. Kumbukizi hizi zinamfanya Meya Sosi kubadili nia na kukubali kukutana nao. Anawaza haya:

‘Hawa wanaotaka uwasikilize
ni mzizi wa vizazi vya kesho!
Yote yanategemea uwezo wetu...’ (uk. 56)

Uzungumzi nafsia huu ulimfanya Meya kubadili msimamo wake wa awali wa kutokutana na wafanyikazi katika kushughulikia haja zao.

Uzungumzi nafsia wa Dida unatokea mwishoni mwa tamthilia sawia na ule wa *Kijiba cha Moyo*. Kupitia kwa uzungumzi nafsia wa Dida, mwandishi anatuchorea ukatili unaodhihirishwa na viongozi dhidi ya wanyonge wanapolalamikia kuhujumiwa haki zao. Dida anazungumzia jinsi harakati za kuwafurusha na kuwatawanya wanyonge ambao waliandamana ili kutetea haki zao zilivyotekelezwa na askari ambao ni vikaragosi wa Meya:

...Bunduki inayotema risasi tatu tatu
Basi tena uwe umelala chini hivi
Mlio wake ...vitoa machozi
Magari yanayotapika maji... (uk. 65)

Mwandishi kupitia kwa uzungumzi nafsia wa Dida, anakejeli viongozi wenye tamaa na ubinafsi ambao wameshindwa kuyashughulikia mahitaji ya waliowachagua kwa kudai nchi zao kuwa changa kiuchumi ilhali wanaweza kumudu gharama ya kununulia zana za kuwaangamiza. Viongozi hawa wanapotishwa kwa migomo na wafanyikazi katika sekta mbalimbali, wao hutumia nguvu zozote kuzima ari ya watetesi hawa wanyonge. Polisi

badala ya kulinda umma na kuwapa usalama, huonekana wakiwatatiza na kuwaumiza. Ushahidi huu tunaupata katika uzungumzi nafsia wa Dida ambaye anajisemea hivi:

Wakati wa mauti kama jana
Kumbe wazee huwashinda
vijana nguvu!(uk. 65)

Hii ina maana kuwa askari hawa husababisha fujo ambayo huwalazimu wanyonge kukimbilia usalama wao. Hii ni shara tosha kuwa askari ni mali ya viongozi na sio wanajamii wa kawaida. Pia tunabaini kuwa viongozi hujali maslahi ya wanaoendeleza ukupe kwani wao ndio 'watu'. Dida anadhihirisha haya:

... Kuna roho za mtu na kiatu
na hizi mbili ni tofauti.
Meya anajua hili
Watu wake wana roho za watu. (uk. 65)

Hii inaonyesha chanzo cha migongano kati ya Meya na wanyonge walio wengi katika jamii. Mwandishi anasisitiza ujumbe wake kwa kukejeli viongozi wa mataifa machanga ambao huweza kununua vyombo vya kuwaangamiza wananchi lakini wakashindwa kuyashughulikia mahitaji ya kimsingi ambayo ni chanzo cha migogoro inayoshuhudiwa katika sekta mbalimbali katika jamii. Sitiari ya 'mtu' katika muktadha huu inarejelea viongozi na vibarakala wao na 'kiatu' inarejelea wanyonge ambao hudharauliwa kwa kukanyagiwa chini. Kiatu kwa kawaida huvaliwa na mtu aliye hai ili kumsetiri mguu wake. Huu ndio uhusiano anaojenga mwandishi kwa kuonyesha kuwa viongozi hawawathamini maskini katika jamii bali tu katika kuwatumia kujiendeleza. Huu ni ubinafsi wa kiwango cha juu zaidi ambao unaendelezwa kwa njia za kidhalimu katika nchi nyingi za Afrika ambazo zinadai kuwa 'huru'. Viongozi hawa wa nchi hizi za ulimwengu wa tatu pamoja na vibarakala wao huwakandamiza wakazi wake licha ya kuwadhalilisha katika misingi ya uzalishaji na ugavi wa mali kiasi cha kuwafanya wasijithamini.

Uzungumzi nafsia humsaidia msomaji wa kazi ya fasihi kupata mitazamo ya wahusika mbalimbali katika tamthilia husika katika kukuza dhamira za mwandishi. Licha ya wajibu huu, uzungumzi nafsia ni nguzo ambayo hutumiwa na mwandishi katika kuwasukuma

wahusika kubadili misimamo yao na kujisaili ili waweze kuondoa vikwazo vinavyozuia kujiri kwa maendeleo ya kijamii.

3.2.5 Usambamba

Ngonyani akimnukuu Jakobson (1987a: 146) anasema kuwa Mtaalamu Lowth ndiye wa kwanza kutumia neno usambamba baada ya kuchunguza aya za biblia na kubaini kuwa zilikuwa zimejirudiarudia. Lowth alieleza kuwa usambamba ni:

“Mshabaha wa aya moja na nyingine ninaita usambamba. Kauli moja inapotolewa, na ya pili ikaunganishwa, au ikawekwa chini yake, ikalingana, au ikatofautishwa nayo katika maana, au ikafanana nayo katika muundo, ninaita mistari hiyo, mistari sambamba; na maneno au virai vinyojibizana katika mistari inayoshabihiana, virai sambamba...”

Naye Wamitila (2002) katika kujalizia maelezo ya Lowth, anaelezea kuwa usambamba ni urudaji wa muundo sawa au ruwaza sawa ya kisintaksia katika virai, vishazi au sentensi. Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa ni wazi kuwa usambamba ni mlandano wa muundo na mitindo katika tanzu za fasihi ambao unapatikana katika kiwango kikubwa kuliko neno au sauti tofauti na ilivyo takriri.

Katika Tamthilia ya *Chamchela*, usambamba umedhihirika kwa viwango mbalimbali. Sure anamshauri Rosa kukubali mabadiliko yaliyofika kwake. Anataka afahamu kuwa mabadiliko ni jambo lisiloepukika katika jamii. Anasisitiza haya:

... Huenda yangekosa utamu wa kuyaishi.
Waliisha kusema vikwazo ni muhimu katika kuhamasisha kani na kutimiza malengo. Wengine *waliisha kusema* utamu na uchungu ni sehemu mbili za sarafu moja. Vinginevyo sarafu hii ya maisha isingekuwepo... (uk. 7)

‘Waliisha kusema’ ni usambamba wa virai vitenzi unaoonyesha msisitizo wa mabadiliko ambayo ni jambo la muhali kuepukika katika jamii. Kupitia kwa msisitizo tunatambua madhara yanayowakumba wanajamii wanaokataa mabadiliko ambayo tayari yamefika kudumu katika jamii zao. Sure anatumia usambamba huu katika kumsihi Rosa akubali mabadiliko ambayo yamefika kwake kwani ni ya lazima na hakuna kitu kitakachozuia

kutokea kwake. Hii ni kwa kuwa Rosa amekataa kuridhia uamuzi wa Mayaka aliyeamua kumwoa Bisase aliyemzidi umri.

Bisase anaeleza jinsi Mayaka alivyomfaa katika ukiwa wake. Anasisitiza hali hii kwa usambamba ili kuweka wazi sababu zilizompelekea yeye kumweka Mayaka licha ya tetesi za jamii kuwa anamzidi kiumri. Serah anapinga haya na Bisase katika juhudi zake za kumtetea Mayaka anamweleza alivyomsaidia:

... Mimi ninajali maisha yangu. Ninahitaji *mtu wa kunijali*. *Mtu wa kuniamsha* nishindwapo kunyanyuka kitandani. *Mtu wa kunijulia* hali na kunishughulikia. *Mtu wa kunipa* tumaini magharibi yaanzapo kuniita. *Mtu wa kunipa* tumaini la kuliona jua likichomoza mara nyingine... (uk. 22)

Hapa tunaona muundo wa virai unaofanana. Huu ni usambamba wa virai nomino. Sifa moja ya kiumbe kuitwa mtu ni kuwa na utu. Utu huu ndio anaouelezea Bisase ulioonyeshwa kwake na Mayaka. Kwa usambamba huu wa virai vitenzi mwandishi anasisitiza umuhimu wa Mayaka katika maisha ya Bisase ambaye ameachwa bila mfariji baada ya kufiwa mumewe, mwanawe pamoja na jamii kumtenga. Maelezo haya yanaonyesha matatizo ambayo huwakumba wajane katika jamii.

Utamaduni wa Kimagharibi umewavuta vijana mno kwa kujitafutia uhuru ili waepukane na maamuzi ya wazee ambayo wanayaona yasiyo na umuhimu wowote. Uhuru huu unawataka vijana kujisimamia kwenye misingi ya kifedha japo hawana kazi za kuwapa ujira na wanaishi maisha ya ulitima. Hii ni sababu tosha ambayo inawavuta kwenye mahusiano na walio navyo licha ya kwamba wanaenda kinyume na itikadi za jamii zao. Rukia anahofia kuwa ndoa ya Mayaka na Bisase iliyojengwa kwa misingi ya kiuchumi huenda isikamilishe hatua ya kukiendeleza kizazi chake kwani Bisase hataweza kumzalua watoto kwa kuwa amezeeka. Ukweli huu unapuuzwa na Kofa lakini anasisitiza akisema:

... Jangwa hasa! Tutakuwa tumekufa kabla ya kuaga ikiwa tutangoja kulishwa vilivyoandaliwa (*Kwa hadhira*). Huo ndio *ukweli* unaouma. *Ukweli ambao* mwenzangu anataka tuukwepe. *Ukweli ambao* nyinyi wazee wetu hamtaki tuuone... (uk. 38)

Mwandishi anatumia usambamba huu wa virai nomino unaotokana na usemaji kando wa Rukia katika kuwasuta wanaokimbilia mabadiliko bila kuwazia madhara yake. Pia anawasuta wazee ambao hawako tayari kujadiliana na vijana ili kupata suluhu katika mgogoro wa mabadiliko ambayo ni lazima.

Mayaka anamweleza Bisase mambo mengi yaliyosemwa kuhusiana na uhusiano wao wa ndoa. Anamweleza kwa uwazi na msisitizo yanayosemwa kwake kuwa katika ndoa ile. Anasisitiza hali hii:

Sivyo. Simaanishi hivyo. *Wanasema* nilishindwa kuona katika kukuchagua wewe kuwa mwenzi. *Wanasema* macho yangu yameingia kiwi. *Wanasema* nimepofushwa na miliki yako. *Wanasema* wewe ndo umenioa. Si mimi nilioa. *Wanasema...wanasema* kila jambo... (uk. 42)

Usambamba unaojitokeza hapa ni wa virai vitenzi. Mwandishi kupitia kwa usambamba huu anaeleza ni kwa njia gani ndoa hii kati ya Mayaka na Bisase haifai. Japokuwa hali hii inasisitiza hali ya wasiwasi kwa Mayaka, mwandishi anadhihirisha kwa uwazi kuwa umaskini ndio chanzo cha vijana kujiingiza katika ndoa za aina hii. Wao hufanya hivi ili wajiimarisha katika misingi ya kifedha. Hizi ndizo sababu zinazotolewa na wazee katika jitihada zao za kuwatahadharisha vijana dhidi ya itikadi za utamaduni wa kigeni.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mwandishi anadhihirisha matumizi ya usambamba katika viwango mbalimbali ambapo unasiadia kukuza ujumbe unaowasilishwa. Tatu, ambaye ni mmoja wa wawakilishi wa wafanyikazi wanaodunishwa na Baraza la Cheneo analalamikia hali mbaya inayowasibu wafanyikazi kutokana na kunyimwa haki zao. Anamkabili Meya kwa maswali haya:

... *Kuna raha* gani watoto wetu wanapofukuzwa shule kwa sababu hatuwezi kuwalipia karo? *Kuna raha* gani kutazama watoto wetu kufa taratibu mikononi mwetu kwa sababu hatumudu gharama ya matibabu? Tena katika hospitali ya mwajiri wetu? Hospitali hiyo imejengwa na nani kama si sisi waajiriwa wake? (uk. 70)

Usambamba wa virai vitenzi ndio unadhihirika hapa. Usambamba unaojitokeza hapa unatiwa nguvu na maswali ya balagha. Kupitia kwa usambamba huu wa vira, mwandishi anatumia uhalisia wa hali ngumu wanayokumbana nayo wafanyakazi wa Baraza la mji wa Cheneo. Haya ni matokeo ya ubinafsi wa viongozi ambao hujitakia makuu bila kuwajali wananchi wa kawaida. Mwandishi anasisitiza namna kunyimwa haki kwa wafanyakazi wa Baraza la mji kunavyowakosesha raha na badala yake kuwaingiza katika uhitaji na majonzi kwani wanashindwa hata kuzikimu familia zao.

Tatu anatumia usambamba katika kuelezea maafa yanayotokana na ukosefu wa dawa hospitalini. Anamweleza Meya hali hii ya kukatisha tamaa.

*Watu wanakufa kwa sababu ya...
...watu wangukuwa wanakufa kwa...
...kuwapa watu dawa hata kwa mkopo
Watu kujifia kama nzi! (uk. 38)*

Usambamba uliotumiwa hapa na mwandishi unasisitiza majanga ya wanacheneo ambayo yanachangiwa na mapuuza na kudhalilishwa kutoka kwa viongozi waliojawa kiburi na ufedhuli. Mwandishi anataka kuisitiza kuwa watu wanakufa kwa njia zisizofaa kutokana na ukosefu wa dawa hospitalini pamoja na mishahara duni inayowazuia kumudu gharama ya maisha inayozidi kupanda kila uchao. Mwandishi anaendelea kuonyesha ni kwa njia gani ubinafsi unavyosababisha wananchi wa kawaida kuendelea kuumia katika nchi changa barani Afrika kutokana ubinafsi wa viongozi wenye ubinafsi. Usambamba huu unasisitiza umuhimu wa kuwa na utu kwa upande wa viongozi ili wajali maslahi ya wananchi ambao wanateseka.

Usambamba wa virai nomino unaojitokeza katika wosia wa Siki kwa Meya akimsihi ili ashughulikie matatizo ya wanacheneo pia unasisitiza maudhui ya utu. Usambamba huu ni dhihirisho la kushamiri kwa ubinafsi kwa viongozi wa nchi changa za bara la Afrika. Siki anamweleza Meya hivi:

*... La! Ukweli ni kwamba watu wetu
wana tatizo. Watu wetu wana njaa.
(watu wetu) wana kiu ambayo
haikuzimwa... (uk. 12)*

Mwandishi anasisitiza ujumbe wa haki kwa wananchi akitumia usambamba wa vira nomino. Siki anamsisitizia Meya umuhimu wa kuwa na utu kwa wanacheneo kwa kuwa wao ndio waliomchagua kwa imani kwamba angeweza kutatua shida zao. Viongozi mara nyingi wanapowataka wananchi kuwapigia kura, huwarai kwa ahadi ambazo baada ya kuchaguliwa husahaulika kabisa kwani shabaha yao haikuwa kutetea wananchi bali kujipatia fursa ya kuyafisidi mataifa yao na kujilimbikizia utajiri pekee yao.

Gedi akimpasha Meya habari za kugoma kwa wafanyikazi wa Baraza la mji, anamweleza sababu wanazotoa. Baadhi ya sababu wanazotoa ni mishahara duni, ukosefu wa dawa hospitalini pamoja na mazingira duni wanamofanyia kazi. Haya ndiyo mambo ambayo daktari Siki alijaribu kumhimiza kuyatekeleza hapo awali kwani ni haki za wafanyikazi japo Meya hakuyatilia maanani. Gedi anamweleza:

Mstahiki Meya sir, wanadai mishahara
zaidi; wanadai dawa hospitalini, wanadai
kukuona; wanadai takribani kila kitu. (uk. 32)

Mwandishi kupitia kwa mhusika Gedi, anaonyesha kwa uwazi kuwa chanzo cha migomo inayoshuhudiwa katika sekta mbalimbali ni utepetevu wa viongozi ambao wamechelea katika kuwapa haki wafanyikazi. Haya yanasisitizwa na maelezo ya Tatu kwa Meya:

... La Bwana Meya! Kwa ufupi,
ni kutoshugulikiwa kwa maslahi
yetu na nyinyi mnaopaswa
kuyashughulikia. (uk. 66)

Wafanyikazi wa Baraza wanalazimika kushiriki migomo kama njia ya kuwashinikiza viongozi kuyashughulikia mahitaji yao. Kwa maoni ya Arege, migomo inayotokana na wanyonge ambao ni wengi ndiyo silaha ya kipekee katika kupata haki yao kutoka kwa hawa viongozi dhalimu. Mwandishi anaonyesha kuwa hii ndiyo njia ya pekee na mwafaka ambayo wanyonge wanaweza kutumia ili kuwang'oa manyang'au hawa na wafuasi wao kutoka uongozini.

Katika *Kijiba cha Moyo*, maelezo ya wahusika mbalimbali yanadhihirisha matumizi ya mtindo huu wa usambamba. Sele anaeleza chanzo cha hali yake ya kukosa kujithamini. Anaeleza chanzo cha hali hii kuwa ni maonevu yake yanayotokana na ngozi yake nyeusi. Anamweleza Zainabu maonevu haya ifuatavyo:

Si michezo ya shuleni hata. Hata nyumbani pia. Mlinicheka kwa mwendo wangu wa matagataga. Mlinicheka kwa midomo yangu mikubwa. Nilichekwa kwa weusi uliokoza na kukolea. (uk. 43)

Mwandishi anaonyesha chanzo cha wakazi wa bara la Afrika kukosa kujiamini na kujithamini. Hali ilianzishwa hapo awali kabla ya kujinyakulia uhuru. Hii ndiyo njia iliyotumiwa na viongozi wa mfumo wa kibepari katika uzalishaji mali ili kuhakikisha kuwa wakazi hawa hawajitegemei kwa kuwafanya wakose kujiamini licha ya kujithamini. Kwa kutekeleza hili, waliwafunga minyororo dhahania katika fikra zao iliyowafanya kuamini kuwa wao wameumbwa kuwa watumwa katika nchi zao. Mbinu hii iliwarahisishia wanyonyaji harakati zao za kuwanyonya wakazi wa mataifa machanga bila wao kulalamika.

Amri anamweleza Sele jinsi ilivyo vigumu kuelewa dhana ya uhuru hata kwa anayefikiria kuwa anao. Anamweleza jinsi maana ya uhuru ni tata. Anamtahadharisha Sele dhidi ya uhuru anaofikiria kuwa nao anaposema:

Hata mwenyewe-mwenyewe ni mtumwa wa jambo linalompa huo wenyewe-wenyewe. Bila huo utumwa hawezi kuwa mwenyewe-mwenyewe. Mwenyewe-mwenyewe ndiye hukifanya kitu kuthaminiwa hata kama kitu hicho hakina thamani vile au ukubwa. Naye anajua kuwa kitu hicho hakina thamani yeye naye Huyo wenyewe-wenyewe atakuwa hanao. (*Kimya.*) Lazima awe mtumwa wa kitu hicho ili kupata wenyewe-wenyewe wake. Unafahamu lakini kuhusu wenyewe-wenyewe? (uk. 67)

Kinachosisitizwa hapa na mwandishi ni kwamba kujithamini ndiyo hatua ya kwanza na ya kimsingi katika kupata uhuru halisia wa kiutu. Mwandishi anatalii athari za ukoloni kwa wakazi wa nchi za bara la Afrika ambao walibaki kuwa watumwa katika nchi zao baada ya viongozi weusi kunyakua hatamu za uongozi na kuendeleza ukoloni mamboleo. Dhana ya kujithamini inashughulikiwa pakubwa na mwandishi kwani anaamini kuwa udhalimu wanaofanyiwa wakazi wa nchi za bara la Afrika unatokana na kutojithamini. Lengo la mwandishi ni kuonyesha kwamba hatua muhimu itakayomwezesha mkazi huyu kujikomboa itakuwa ni kujithamini.

Usambamba wa virai vitenzi na nomino umetumika sana katika tamthilia teule na umefanya kazi ya kuvuta uzingativu wa msomaji kwenye matini ili kupokea ujumbe unaokuzwa licha ya kufanya matini kuwa na muundo na mvuto pale unapotumika. Aidha, umesisitiza maudhui ya mwandishi.

3.2.6 Nyimbo, Ushairi na Sauti

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa njia ya mkato, picha na mapigo ya silabi. Naye Kinoti (2008) anaeleza kuwa nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia kwa mahadhi ya kupendeza. Anafafanua aina mbalimbali za nyimbo kama vile za kuzaliwa kwa mtoto, kuongoa, watoto wachezapo, tohara, mapenzi, harusi, kazi, matanga na nyinginezo. Nyimbo mbalimbali zinajitokeza katika tamthilia teule kwa madhumuni tofautitofauti.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* sauti zinazosikika ni za wafanyikazi. Sauti hizi zimetumiwa ili kuleta mwamko mpya kwa wanyonge wapate hisia za kuungana katika kutetea maslahi yao. Sauti zinazosikika zina ujumbe huu:

Ndugu wafanyikazi wenzangu
Tumefika hapa tukiwa kitu kimoja
Na umoja huu ndio nguzo yetu
Tushikamane hadi mwisho
Mwisho wa madhila yanayotuzonga
(*Wafanyikazi wanashangilia*)
Ndugu zangu katika vita hivi
Msisahau kuwa kwa muda sasa
Tumeonewa vya kutosha
Tumedhalilishwa vya kutosha. (uk. 57)

Japo ni sauti, mahadhi yake yana lengo la kumfahamisha Meya umuhimu wa kuchukua hatua za kushughulikia maslahi ya wafanyikazi wa baraza ambao wanateseka kwa kukosa kuyamudu maisha yao na jamii zao. Matumizi ya 'ndugu' yanazua na kuimarisha hisia za undugu katika kupiga vita uongozi mbaya unaowanufaisha wachache wanaomzunguka Sosi. Sauti hii imebeba dhamira ya mwandishi inayoonyesha kuwa usawa katika misingi ya kiutu utapatikana tu pale ambapo wanyonge wataungana na kuwavua mataji viongozi dhalimu. Hii inakuwa muhimu kwa kuwa muungano huu unaonekana katika migomo

inayoshuhudiwa kwenye sekta zote kwa kuwa wafanyikazi wa baraza wanasema kwa ‘sauti’ moja sawa. Midundo ya sauti inawahamasisha wafanyikazi kutetea haki zao.

Nyimbo zinajitokeza kwenye *Kijiba cha Moyo* zinaendeleza dhamira ya mwandishi ya mwamko mpya katika misingi ya kiuchumi na kijamii. Sele hafurahii nyimbo zisizokuwa na mahadhi ya kimagharibi kama alivyofanya hapo awali. Anafurahia wimbo unaoimbwa na Bi. Rahma wenye midundo ya Kiafrika. Anaufurahia zaidi kuliko hapo awali. Hili ni katika kuelezea shabaha ya mtunzi kuwa mafanikio ya Mwafrika ni katika kujisaka na kujithamini ili aweze kupata urazini wa kweli wa kupigana na mfumo wa kibepari katika kuleta usawa. Wimbo wa Siti binti Saad una ujumbe huu:

Siri sifunue
Kwa wino wa rangi,
Fahamu ujue
Kuna mambo mengi,
Wajila mwenyewe
Kwa ujinga mwingi. (uk. 45)

Wimbo huu unabeba chembechembe za shabaha ya mwandishi kuwa angamio la wanyonge litazidi kuwepo barani Afrika kutokana na ujinga wao kunyanyaswa kwa hiari. Wimbo ulikuwa umesahaulika kama anavyosema Bi. Rahma. Hii ni ishara tosha kuwa Mwafrika aliharibikiwa mambo alipoanza kupapia utamaduni wa kimagharibi asiouelewa be wala te yake na kuitupilia mbali kuusahau ule wake. Alisahau kuwa wahenga waliposema ‘nguo ya kuazima haisetiri matako’ hawakutania. Madhara yake yamemfanya kugundua hili japo kwa kuchelewa mno, kwani wimbo wa kuazima haukeshi ngoma.

Wimbo katika tamthilia ya *Chamchela* unatumika kuweka wazi mkinzano unaotokana na mapenzi. Mapenzi yanaumiza kwa kuwa ndiyo yanapigwa mawimbi ya mila mbili zenye asili tofauti. Wimbo unasema hivi:

Umeniacha kipenzi, Mwenyewe jipigania,
Sasa tena hunienzi, mabaya wanitakia,
Meniacha majonzi, maisha hangaika,
Japo hapa menileta, mkononi kuingia,
Sikufika kileleta, mahaba kuniandalia,
Mashakani najikuta, kwa kukosa kunioa. (uk. 54)

Wimbo huu unaonyesha hali ya kuhuzunika baada ya kukataliwa na mchumba. Wimbo huu unaangazia mgogoro mzima wa tamthilia hii. Mgogoro wa tamthilia hii unazunguka kwenye mizizi ya mapenzi ambayo yanageuka kuwa shubiri kwani hayaafikiani na matumaini ya wahusika mbalimbali.

sauti moja mwishoni mwa tamthilia hii inayokariri mada yake ifuatavyo:

Kaka... kaka
Chamchela... chamchela
Kaka... kaka
Chamchela... chamchela
Kaka... kaka
Cham - chel - a. (uk. 78)

Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2011) inaeleza chamchela kuwa ni upepo mkali unaovuma huku ukizunguka ambao aghalabu huleta maafa. Katika tamthilia hii upepo huu ni utamaduni wa kimagharibi ambao umewazunguka wazee na kuwaburura kwani umewapeperusha vijana. Hii ina maana kuwa mabadiliko ya utamaduni huu ni maafa bali si maendeleo.

Katika tamthilia hizi tumebaini kuwa mwandishi ametumia nyimbo pamoja na sauti kama mbinu ya kuchorea mgogoro katika tamthilia. Sauti zimetumika katika kusuta nafsi za wahusika katika waliyoichukua isiyoafikiana na maono ya kuiendeleza jamii. Nyimbo zimetokeleza majukumu yaliyolengwa na kunga zingine za utunzi. Wimbo wa Siti binti Saad unafafanua sababu inayowazushia maangamizi wakazi wa Afrika ambayo ni ujinga. Wimbo wa mapenzi katika *Chamchela* unawasuta vijana wanaonaswa katika pingu za mila za kimagharibi kwani wanathamini ubinafsi wa kiuchumi kuliko jamii zao. Hata hivyo mwandishi anajenga mabadiliko haya katika sitiari ya Chamchela ili kuwezesha uelewaji wa msimamo kwamba mabadiliko lazima yawepo katika jamii kama upepo huu. Muhimu ni kukadiria na kufuata yenye umuhimu na kupuuza yasiyofaa.

3.3 Hitimisho

Tumechunguza mbinu za usimulizi zilizotumika kwa wingi na ambazo zinadhihirisha ubunifu katika tamthilia teule. Utafiti umechunguza sentensi mbalimbali zilitumiwa kusimulia ujumbe wa mwandishi. Tumechunguza mdokezo, kuchanganya ndimi, maswali ya balagha, usambamba, uzungumzi nafsia, nyimbo na ushairi katika tamthilia

tatu zilizoteuliwa. Aidha, kupitia kwa kiwango hiki cha mtindo, tumebainisha kwamba uteuzi wa mbinu za usimulizi huwezesha uwasilishaji wa ujumbe kwa njia inayoleta athari zilizonuiwa. Aidha, imebainika kuwa mbinu za usimulizi licha ya kuufafanua ujumbe wa mwandishi, humwainisha mwandishi kimtindo.

SURA YA NNE

TAMATHALI ZA USEMI KATIKA TAMTHILIA ZA AREGE

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumefafanua istilahi tamathali za usemi kama kipengele cha kuelezea mtindo wa tamthilia teule. Tumebainisha na kuchanganua tamathali za usemi ambazo zimejitokeza kwa wingi katika tamthilia zote pamoja na athari yao katika kuelezea maudhui yanayoibuliwa katika tamthilia teule za Arege.

4.2 Tamathali za Usemi

Kazi ya fasihi, haihusiani na kuwasilisha mawazo tu, bali kuyawasilisha mawazo hayo kisanaa. Habari au wazo fulani haliweza kuelezwa au kuwasilishwa kwa wasomaji bila kuzingatia hali ya kuwepo kwa usanii wowote. Mawasiliano yote ya kisanaa huhitaji kuwasilishwa kwa mbinu za kimvuto, ile njia inayompa raha au ladha tamu msomaji anapojaribu kuufuatilia ujumbe wa mwandishi wa kazi ya fasihi.

Katika sura hii utafiti umeshughulikia vipengele vya mtindo ambavyo Leech alivirejelea kama ‘tropes’. *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili* ya TUKI (2006) inatoa maelezo kuwa ‘tropes’ ni tamathali za usemi. Kwa mujibu wa Senkoro (1982) tamathali za usemi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata katika maandishi ama kusema. Wakati mwingine hutumiwa kwa njia ya kupamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha.

Mulokozi (1989) naye anafafanua kuwa tamathali za usemi ni tungo au kauli fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo ya kijamii. Tamathali huchora picha kwenye akili ya msomaji ili kumwezesha kuelewa ujumbe kwa urahisi. Inabainika kuwa tamathali za usemi licha ya kupamba kazi ya fasihi hufumba ujumbe wa mwandishi. Hii humhitaji msomaji kuufumbua ujumbe wa kazi hiyo kutegemea muktadha wake. Usanii hupatikana katika ukiushi wa kawaida wa lugha iliyozoeleka. Hiki ndicho anasisitiza Jakobson akinukuliwa na Njogu na Chimerah (1999) anapoeleza kuwa fasihi ni matumizi ya nguvu dhidi ya lugha ya kawaida kimaksudi.

Tamathali za usemi ni dhana iliyoshughulikiwa na wataalamu mbalimbali pamoja na uainishaji wake. Maarufu katika uainishaji wake ni pamoja na Holman (1960), Kuhenga (1977), Mbatiah (2001) na Senkoro (2011). Wataalamu hawa wote wanakubaliana kuwa

tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi katika lugha ya kawaida katika fasihi. Hii ina maana kuwa waandishi wa fasihi huchukua lugha ya kawaida na kuifinyanga upya ili kuzalisha maumbo mapya katika kuwasilishia ujumbe kwa jamii.

Kazi yoyote ya fasihi huwa na maana ya nje na ile ya ndani. Maana ya nje hutokana na matumizi ya lugha kwa jumla. Ili kupata maana ya ndani msomaji au msikilizaji wa matini ya fasihi anahitaji kuchunguza ubunifu wa mwandishi katika ujumi wa kazi husika. Utafiti ulilenga katika kushughulikia maana hii ya ndani kupitia uchanganuzi wa tamathali za usemi zilizotumika katika tamthilia za Arege.

Ni wajibu wa kila mhakiki wa matini za fasihi kujaribu kuonyesha namna kila neno katika utungo wowote huwa na maana na umuhimu hasa kulingana na vile lilivyotumiwa. Mwandishi wa kazi ya fasihi huteua maneno fulani akiwa na lengo fulani na wala hatumii maneno kwa njia ovyo tu. Ufundu huu wa kuteua ndio hudhahirisha upevu wake wa lugha na hujitokeza katika tamathali za usemi anazozitumia. Utafiti umechanganua tamathali za usemi katika tamthilia tatu za Arege na kubainisha kusudio lake la kuzitumia katika sehemu mbalimbali. Hii ndio sababu Phythian (1970) akinukuliwa na Wambua (2001) anasema kuwa:

Mtunzi wa kazi ya fasihi huchagua maneno fulani badala ya mengine na kuyaweka au kuyapanga mengine katika utaratibu maalum ndiposa yaweze kuoana na mengine ili kuleta maana na athari kwa wasomaji. Kusema juu ya uteuzi wa mshairi (mtunzi) humaanisha kuchunguza uteuzi wake kwa jumla na upeo wa athari za maneno hayo na vile anavyoshirikisha hayo yote ili kufikia nia yake. (uk. 26)

Kwa hivyo tamathali za usemi zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ya fasihi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa na hivyo kumhusisha msomaji wa kifasihi katika kupata ujumbe uliofumbikwa kwenye matini ya kifasihi.

Utafiti huu ulichunguza tamathali za usemi ili kuafikiana na lengo la tatu la kazi hii. Utafiti katika sura hii uliongozwa na mhimili wa nne wa nadharia ya Uihakiki wa Kimtindo unaosema kuwa, mwandishi hutumia lugha kiufundi na athari za ujumi haziwezi kutenganishwa na matumizi ya kisanaa katika kazi anayoiandika. Mhimili huu uliuongoza utafiti huu katika kutambua na kuzishughulikia tamathali za usemi

zilizojitokeza kwa wingi katika tamthilia za Arege. Tumechanganua tamathali nane katika tamthilia teule.

4.2.1 Tashbihi

Kwa mujibu wa Senkoro (2011), Msokile (1993), Khatibu (1986) na Wamitila (2003) tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo watu ama vitu viwili au zaidi hulinganishwa au hufananishwa na watu ama vitu vingine au ushabihiano fulani fulani wa hali za utendaji au maumbile, mathalani, sura, rangi na jinsi ya kujimudu kwa kutumia maneno kama vile: kama, mithili ya, sawa na, mfano wa na mengine ya aina hiyo. Ulinganishi huu unadhamiria kusesitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini. Tashbihi pia huitwa tashbiha au mshabaha (King’ei na Kemoli, 2001). Mohammed (1995) naye akichangia katika ufafanuzi wa tashbihi anaeleza kuwa msingi wa tashbihi katika fasihi ni ule wa kutafuta namna ya kuweka wazi maana, dhana, picha au hali fulani kwa mujibu wa ulinganifu wa kipicha. Hii ina maana kuwa ufafanuzi wa tashbihi umefumbikwa katika picha zinazomjia akilini msomaji wa matini fulani ili aweze kuzihusisha na kutafsiri ujumbe wa mwandishi. Kuna mifano mingi ya matumizi ya mbinu hii katika tamthilia teule za Arege.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, mbinu hii imetumiwa na wahusika mbalimbali kuwasilisha misimamo yao. Kwa mfano, Sele akielezea umahiri wake katika uogeleaji anasema:

... *Kisha nikapumzika juu ya mawimbi*
kama gogo huku chini yangu maji yakipiga
na kutoa povu. (uk. 2)

Maelezo haya yanaonyesha uzoefu wa Sele wa kuogelea baharini kinyume na anavyodai sasa. Anapoelezea ushwari katika afya yake, Sele anatumia tashbihi ifuatayo ili kumhakishia Bi. Rahma hali yake:

Mzima mimi. Mzima kama
kigongo. Buheri wa afya kabisa. (uk. 27)

Maelezo haya yanalenga katika kumhakishia na kumthibitishia Bi. Rahma kwamba hamna kasoro yoyote katika afya yake dhidi wanavyomdhanika wahusika wengine.

Zainabu akielezea harakati za unyonywaji wa wafanyikazi kutokana na nguvu za kibepari katika uzalishaji mali, anasema:

*...Wanatutikisa na kutuchezea
kama sanamu inavyovutwa kutoka
mbali na kuwawinga ndege kutoka
shamba la mawele. (uk. 24)*

Tashbihi ‘Wanatutikisa na kutuchezea kama sanamu’ imetumiwa na Zainabu kutalii misingi ya mifumo ya kibepari iliyojaa tamaa ya kujinufaisha huku ikiwadhulumu wanyonge katika jamii. Mifumo hii imetawaliwa na ukatili kwa kuwa haithamini utu. Mwandishi anaonyesha ni kwa jinsi gani nchi za bara la Afrika haziwezi kujiendeleza kwani uwezo wao wote umemilikiwa na mabepari ambao huwatumia wapendavyo. Matokeo ya kadhia hizi ni umaskini usiomithilika.

Mwamko mpya uliompata Sele unamfanya akose kueleweka kwa wahusika wengine. Hali hii inasababisha kuchanganyikiwa. Aisha anajikuta katika mtanziko huu. Mambo anayoyasema Sele yanamfanya kuchanganyikiwa hata zaidi. Anasema:

*...Kama lililotiwa hamira, linafura na
kujaa fikirani. Kichwa kinakuwa kizito
kama ninga... (uk. 20)*

Tashbihi hii inarejelea ugumu wa kuelewa mawazo ya Sele ambayo yanamchanganya Aisha. Hali hii inatokana na mawazo tofauti ya wahusika hawa licha ya kuwa katika tabaka moja la wanyonywaji. Kutomwelewa Sele ndiyo sababu kuu ya wahusika wengine kumwona kuwa mgonjwa na wanakosa kuamini maelezo ya hali yake. Majanga haya ya Sele ndiyo huwakumba wale wachache waliopata mwamko mpya na kutambua maonevu ya mifumo ya kibepari katika jamii. Wenye kugundua njama za mabepari huonekana kuwa wendawazimu wanapowaelimisha na kuwaaminisha wengi wasiofahamu chochote.

Sele anaendelea kuonyesha athari ya mifumo ya kibepari inayowatingisha na kuwaacha hoi wanyonge kwa kuyeyusha matumaini yao, Anasema hivi:

*... Na mimi nahisi kama sisi
tunayumbishwa mithili ya miti
msimu wa kipupwe... (uk. 29)*

Mifumo hii ya kiuzalishaji mali ya kibepari inawanufaisha wachache wanaozinyonya nguvu za wanyonge walio wengi katika jamii. Hali hii inamuumiza Sele. Sele anaumia kwani licha ya kupata mwamko mpya yumo katika tabaka moja na wanyonge wengine ambao hawajielewi kamwe kutokana na dhuluma na udhalilishaji wa wanyonyaji wao. Anafananisha dhuluma hizi na upepo wa kipupwe kwa kuwa zinayumbisha mawazo ya wanyonge na kuwaacha hoi. Hii ndiyo sababu yake kuu ya kuanza kutathmini umuhimu wa uhusiano uliopo kati yao.

Musa anamwonya Sele kuhusu hatua anayodhamiria kuchukua, akitalii athari zake kwa wahusika wengine katika jamii. Anamwambia:

Linaweza kuwa dogo na athari
zake ziwe kubwa, *kama tone la
mafuta ya taa kisimani*- huhangaisha
mtaa mzima... (uk. 50)

Tone la mafuta ni kidogo sana tukilinganisha na maji kwenye kisima ambayo ni mengi. Harufu ya mafuta huyafanya maji yaliyo mengi yasiweze kuwa salama kwa watumiaji. Kwa kutumia ulinganisho huo, Musa anamtahadharisha Sele kutoliona tatizo lake la kuhitaji matibabu kuwa rahisi kwani matokeo yake huenda yakazaa janga kubwa litakalowadhuru watu wengi katika jamii hii ambayo tayari ina matatizo tele. Akieleza hatari iliyopo ikiwa ugonjwa wa Sele hutashughulikiwa kwa tahadhari, Jamila anasema:

...Hatimaye hujiachilia na *kuwa
mfano wa gogo lililoliwa na
mchwa*. (uk. 91)

Kwa mujibu wa Gogo lililoliwa na mchwa kwa kawaida halina umuhimu wowote kwa mtumiaji aliyetaka kunufaika nalo. Jamila anatahadharisha kwa kutoa picha ya jinsi Sele atakavyokosa thamani yoyote hali yake isipofuatiliwa kwa karibu na kumpa matumaini ili ajirejeele.

Zainabu anaeleza maenezi ya dawa za kulevya kwa kushuku kuwa huenda ndiyo anayoyatumia Sele. Kujaa huku kwa dawa kumewafanya vijana kuyatumia ovyo na mwishowe huishia kuwa waraibu. Uraibu huu huwafanya kukosa matumaini katika maisha na hata kuishia kukosa kuwa na manufaa yoyote katika jamii zao. Vijana hawa

hukosa kujielewa kwani matumizi ya dawa hizi huathiri saikolojia yao. Zainabu anakiri kuwepo kwa dawa za kulevya anaposema:

Dawa ndiyo. Siku hizi zimejaa
kote kote. Wananyweshwa tu.
Nao wanakuwa kama magogo
yaliyokunywa maji yakashiba... (uk. 84)

Tashbihi aliyoitumia Zainabu ‘wanakuwa kama magogo yaliyokunywa maji yakashiba’ inaonyesha jinsi dawa za kulevya zinavyowadhuru vijana na kuwakosesha thamani. Hii huwafanya kuwa mzigo kwa wazazi kwa kuwategemea. Mwandishi anatalii maudhui ambayo yanaathiri vijana katika jamii zetu ambao wamegeukia dawa za kulevya kwa kukosa kujithamini.

Sele anajadili mbinu wanazozitumia washika dau wa mifumo ya kibepari ili kuwamiliki na kuwanyonya wanyonge bila ya wao kufahamu. Anasema:

Kila wanapokuja huja kwa ustadi
mkubwa. *Huja na vipulizwa laini*
mithili ya hewa hii tunayovuta
ambayo taratibu hukufanya
kunywea unaona lakini huwezi
kufurukuta. (uk. 81)

Mwandishi anaonyesha njia wanazotumia hawa washika dau wa mfumo ya kibepari ili kumiliki na kudhibiti nyenzo za uzalishaji mali. Vipulizwa laini ni misaada wanayotoa kwa wakazi wa mataifa fukara. Misaada hii katika sekta mbalimbali huwafanya wanyonge kuamini kuwa wamepata ufadhili. Hiki ndicho chambo cha kuwafisidi rasilimali wanyonge kwenye mataifa ya ulimwengu wa tatu. Misaada hii huhakikisha kuwa mawazo na fikra za wanyonge zimedhibitiwa ili kutoweza kulalamikia ukatili wanaofanyiwa. Sele anamulika hali hii katika mazungumzo yake na daktari:

Sele: *(Baada ya muda)* Naona nimebanwa na
kitu mfano wa kamba.

Daktari: Kamba?

Sele: Kama kamba vile. Kamaaa... kamaaa...
kama gundi vile? (uk. 74)

Sele anazungumzia udhibiti wa mawazo ya wanyonge ambao huwazuia kuwaza na hivyo kuendelea kudhulumiwa bila kulalama. Kunata huku kunawazuia wanyonge kuwazia kadhia zinazowapitikia maishani mwao.

Sele anaeleza pia namna viongozi wa mifumo hii hutalii na kuyafahamu mataifa ya bara la Afrika kwa kina lakini hatua za wakazi wa mataifa kuwafahamu hufichwa kwa hasira:

Kunigeuza ndani nje. *Kunichambua*
kama karanga. Mimi kabla hata
kuwachungua wanaudhika. (*Kimya*)
Na wewe vivyo hivyo. (uk. 73)

Sele anaashiria juhudi za wanyonyaji hawa kuyafahamu mataifa ya ulimwengu wa tatu kwa uwazi na kina lakini wao hawapendi kueleweka. Wanahofia hili kwani njama yao ya kuyanyonya mataifa haya itatibuka iwapo watatambulika kuwa wahitaji zaidi wa misaada wanayotoa kwa makabwela wa milki zao za kikoloni.

Katika tamthilia ya *Chamchela* hali ni sawa kwani mtindo huu vilevile umetumika na wahusika mbalimbali kutetea misimamo yao. Akirejelea tabia ya Bisase ya kujisemea, Lema anaieleza hivi:

Basi ni nini? Nasikia watu wakianza
kuzeeka huanza kujisemea wenyewe.
Eti wanaanza kuwa kama watoto
isipokuwa umbo na kimo havionyeshi
dalili ya kurudi utotoni. (uk. 14)

Tabia ya kujisemea hunasibishwa na watoto na hapa Lema anamrejelea nyanyake kwa kukosa kukumbuka kuwa amekuwa akijisemea mwenyewe.

Katika kuonyesha unyonywaji wa nguvu katika uzalishaji mali, Rukia anaeleza kuwa:

... Nifikapo nyumbani nimechoka
Na huingia tu nikajibwaga *kitandani*
kama *mzigo uliofungashwa*. (uk. 30)

Rukia anasikitikia hali ya uchovu wanayokumbana nayo baada ya kazi nyingi za kijungu jiko. Mayaka akitetea msimamo wake thabiti wa kumwoa Bisase, anatumia tashbihi ifuatayo:

Mbiki, naona kuna jambo usiloelewa
hapa. *Kisa chako na changu vimetengana*
kama ardhi na mbingu. Mimi si mtoto
ulivyokuwa wewe. (uk. 73)

Ardhi na mbingu ni vitu ambavyo vimetengana kwa masafa na ni muhali vitu hivi kutangamana. Tashbihi anayoitumia Mayaka inaonyesha ukomavu wa kimawazo wa vijana ulioletwa na utamaduni wa Kimagharibi. Vijana wanafanya maamuzi kwa ukakamavu na kuweza kuyatetea bila kutetereka. Mayaka anatumia tashibihi hii ili kuonyesha kuwa anawajibikia uamuzi wake wa kumwoa Bisase ambaye ameridhia yeye mwenyewe hata kama amemzidi umri tofauti na Mbiki ambaye alichaguliwa mume aliyemzidi umri tena akiwa mkembe.

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* inadhihirisha matumizi ya tashbihi kwa njia sawia na tamthilia za *Kijiba cha Moyo* na *Chamchela*. Tashbihi zimetumiwa na wahusika ili kukidhi haja za ujumbe wa mwandishi. Tatu, mwakilishi wa wafanyikazi wa Baraza la mji analoliongoza Meya, analalamikia hali mbaya inayowafika wanacheneo. Anasema:

...sikapata kuona hali kama
hii. (*Kimya*) *Watu kujifia*
kama nzi. (uk. 38)

Tashbihi inayojitokeza hapa ni ‘watu kujifia kama nzi.’ Tashbihi inayotumiwa hapa inalenga katika kutalii namna ubinafsi wa viongozi unavyowafanya wakazi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu kujifia bila kupata msaada. Nzi ni kiumbe duni asiyethaminiwa na binadamu. Watu kujifia kama nzi basi ni kufa kutokana na kutothaminiwa kwa misingi ya kiutu.

Siki anamweleza Diwani III hali mbaya ya uhusiano wake na Meya kuhusiana na mbinu zake za uongozi ambazo zimedhalilisha maisha ya watu wa Cheneo. Anasema:

Mimi na Meya *ni mfano wa*
mafuta na maji. Hatuonani
uso kwa uso. (uk. 45)

Tashbihi hii inaonyesha kuwa uhusiano kati ya Siki na Meya ni mbaya na huwezi kuzaa maelewano. Hii inatokana na tofauti zao za kimtazamo. Siki anaona kuwa uongozi wa

Meya umekosesha maendeleo ilhali Meya anaona kinyume. Hali ya tofauti za kimtazamo ndiyo inasababisha Meya kusema:

...Kupinga haya *ni sawa na kumkama simba mwenye watoto*... (uk. 14)

Tashbihi aliyoitumia mwandishi ni ‘sawa na kumkama simba mwenye watoto.’ inamchorea msomaji taswira ya ugumu uliopo wa kumkama simba na licha ya ugumu wenyewe, kuna ugumu wa kupata maziwa hayo hasa kwa simba anayewanyonyesha watoto. Tashbihi hii inampa msomaji picha ya mambo yasiyowezekana kamwe. Tashbihi hii inamaanisha kuwa hakuna jambo lolote atakaloweza kulifanya Siki ili kuuzuia ukweli ulioenea kwa madai ya Meya kuwa thabiti katika uongozi wake. Hii ni sifa mojawapo ya uongozi wa kiimla ambao huwafanya viongozi kujihisi kuwa na uwezo usioplingika na yeyote katika nchi zao.

Tashbihi zimetumika kwa njia mbalimbali lakini katika juhudi za kuwasilisha ujumbe maalum. Kwa ulinganisho wazi wa vitu anavyovijua msomaji katika jamii, jukumu la tashbihi ni kumwelezea msomaji wa kazi za fasihi ili aweze kujenga taswira akilini mwake. Taswira hizi anazozijenga msomaji wa tamthilia hurahisisha uelewaji wa ujumbe wa mwandishi kwa njia faafu.

4.2.2 Tashhisi

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa hii ni tamathali ya kukipa kitu kisichokuwa na uhai mkamilifu sifa za kitu chenye uhai kinachojitegemea katika mazingira yake. Naye Senkoro (2011), Mohammed (1995) na Msokile (1993) wanajalizia maelezo haya kwa kusema kuwa tamathali hii wakati mwingine huitwa fasili ya binadamu. Kwa tamathali hii, vitu visivyo na sifa walizo nazo binadamu hupewa sifa hizo. Tashhisi ni mbinu ya uhusisho na ulinganisho pia. Mbinu hii ina umuhimu wa kuvitia nguvu vitu ambavyo kwa kawaida ni vitulivu na kuvifanya vionekane katika mwendo wa taharuki na picha. Hii husaidia msomaji kupata mvuto ulioimarishwa na usanii na maana au ujumbe wa mwandishi kwa uwazi. Wataalamu hawa kwa jumla wanakubaliana kuwa tashhisi ni mtindo wa kuhamisha na kupeana sifa za binadamu kwa viumbe visivyokuwa nazo na hivyo kuvipa nguvu katika vitendo mbalimbali.

Mtindo huu umejitokeza mara kadha katika tamthilia teule ili kumwezesha msomaji kupokea ujumbe kama alivyokusudia mwandishi. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, Sele anatuchorea taswira ya starehe ya bahari na uzoefu wake katika uogeleaji. Anaeleza:

...*Nikapiga mbizi. Nikapambana na
Mawimbi chini kwa chini. Nikayapenya.*
Nikataka nitokezee huko wanakokaa papa.
Nilipoibuka nilikuwa palee! Mbali huko.
Kisha nikapumzika juu ya mawimbi kama
gogo huku chini yangu *maji yakipiga kutoa
povu*. Mimi juu, papa chini. Siku hizo nilitaka
niwe bingwa wa dunia. (uk. 2)

‘Kupambana na mawimbi na kuyapenya’ ni tashhisi inayoonyesha ni kwa jinsi gani Sele alikuwa mzoefu wa kuogelea katika bahari ambapo mawimbi yanapewa uwezo wa kibinadamu wa kupambana. Tashhisi pamoja na tashbihi ‘kupumzika juu ya mawimbi kama gogo’ vinatuchorea picha ya kutuwezesha kufikiria jinsi Waafrika walivyokosa kuelewa maana ya uhuru. Hali hii ndiyo iliyowafanya kujihisi mabingwa kupindukia katika nchi zao na kusahau kuwa ukoloni mkongwe ulikuwa radhi kuwapumbaza ili ufanikiwe kuzinyakua rasilimali za nchi bara za Afrika ili kujiendeleza. Haya ndiyo yaliyokuwa mawazo ya wakazi wa nchi changa ambao hawajapata mwamko mpya wa kisiasa.

Pia mtindo huu unajitokeza katika maelezo ya Aisha kuonyesha namna ilivyomwia vigumu katika kutambua ugonjwa anaouguwa Sele. Anaonyesha kuwa hali hii ni ngumu anaposema:

...*Kama lililotiwa hamira, linafura
na kujaa fikirani. Kichwa kinakuwa
kizito kama nanga...* (uk. 20)

Jambo limepewa uwezo wa kufura na kujaa na pia kufanya kichwa kuwa kizito. Hii ni tashhisi ambayo mwandishi ametumia ili kuonyesha namna mchanganyiko wa mawazo ulimpata Aisha kutokana na kukosa kuelewa ugonjwa wa Sele.

Musa akimtahadharisha Sele juu ya maelezo ya daktari kuhusu matibabu anayoyahitaji, anasema:

... *Nawe ukitilia maanani utakufa
moyo mzima...Mwenyewe yataka
ufanye maamuzi yako. Uganga wa
kwanza nafsi yako kuiunganisha na
moyo wako. (uk. 50)*

Tashhisi hii inasisitiza ujumbe wa mwandishi wa kukosa matumaini kwa Sele ikiwa atategemea ushauri wa daktari (mkoloni).

Jamila anamweleza Sele woga wake ambao unamtawala kuwa ulikuwepo tangu akiwa na umri mdogo. Anamwambia:

*Afadhali kunguru. Kila ukiwaona
watu ulikuwa huwezi kuwatazama.
Kichwa kimeinama macho yanauchimbua
mchanga ... (uk. 59)*

Tashhisi aliyoitumia mwandishi ililenga katika kumjengea msomaji picha ya woga uliomzidia na kumtawala Sele hadi utu uzima. Macho yamepewa uwezo wa kuchimbua mchango ambayo kimsingi ni kazi ya mikono. Hii inamsaidia msomaji kunasa picha ya jinsi Sele alivyoziwa na woga uliomzuia kutangamana na watu.

Sele amegundua njama ya wakoloni ya kunyonya nguvu na chumi za mataifa machanga. Anaonyesha hili katika mazungumzo yake na Zainabu ambaye ni mamake. Anamweleza:

... *Niliogopa. Wazo likanijia la
kuwatapikia moyo wangu. Pale
pale nikautapika. (uk. 80)*

‘Kuutapika moyo’ ni tashhisi inayoonyesha jitihada za Sele kuwaelezea madaktari (wakoloni wakongwe) njama yao bila kuficha chochote. Njama aliyozungumzia mwandishi ni ya kuwapumbaza wakazi wa mataifa machanga kuwa wakoloni walikuja kuwasaidia ilhali nia yao ilikuwa kuwafisidi rasilimali zao. Ukweli huu unatokana na mwamko mpya wa Sele ambao haupendelewi na washika dau wa mfumo wa kibepari ni chanzo cha wakoloni kutaka kumpa ‘matibabu’ (kumnyamazisha) yanayofaa ili akome kuwahangaisha katika juhudi zao za kuyafilisisha mataifa fukara rasilimali zao.

Sele anaelezea uchafu uliokuwa katika kibuyu cha mganga, anaurejelea kwa maneno haya:

Kwanza kibuyu chake kile kichafu.
Siku nyingi hakikuona sabuni wala maji. Ni kama cha kuokotwa tu.
Kama kweli nina ugonjwa, *kibuyu chake kitaniangamiza kabla ya ugonjwa wenyewe.* (uk. 81)

Kuona ni sifa inayohusishwa na viumbe. Kibuyu kimepewa sifa hii kwa kuwa mwandishi alitaka msomaji wake apate picha ya uchafu uliozidi katika kibuyu cha mganga. Kibuyu kimepewa uwezo wa kuangamiza ili kuonyesha kitakavyozidisha ugonjwa wa Sele badala ya kumpa nafuu. Hii ni ishara kuwa baada ya wakazi wa bara la Afrika kupigana na kupata uhuru walifikiri Mwafrika mwenzao atakapochukua hatamu za uongozi atathamini utu na usawa katika ugavi wa rasilimali. Haya yalitokea kuwa kinyume kwani alikuwa katili hata zaidi ya mkoloni mkongwe na hivyo kuifisha imani ya mwananchi wa kawaida.

Ukosefu wa imani kwa viongozi wa nchi za bara la Afrika unadhihirishwa na Sele ambapo Zainabu anamweleza umuhimu wa kuwa na imani. Anamweleza hivi:

Afadhali hivyo mwanangu. Lakini si vizuri. Kutilia kila jambo shaka. Imani ikikuvuka si vyema. Nafsi itabaki uchi. Binadamu ni kiumbe wa imani. Wanasema yaweza kuhamisha milima. (uk. 82)

Mwandishi ameipa imani uwezo wa kutenda kama binadamu kwa kuwa anataka kumhamasisha msomaji ili aweze kutambua kuwa binadamu anaweza kufanikiwa katika majukumu magumu akiwa na imani. Anasema bila imani nafsi itabaki uchi kwa maana ya kukosa matumaini.

Naye Jamila akishadidia maelezo ya Zainabu kuhusu umuhimu wa imani, anamweleza Aisha kuwa:

Kama hivi ilivyo kwake Sele. Mzima. Ana nguvu *lakini nafsi inateseka.* Kuna uzima wa afya na uzima wa fikra. Au niseme moyo. Fikra haitulii nao moyo uko juu. Hautulii vilevile. Nayo nafsi inahangaika. (uk. 93)

Jamila anamweleza Aisha umuhimu wa utulivu wa fikra na moyo ili kushirikiana katika mawazo ambayo hujenga imani.

Tamthilia ya *Chamchela* inadhihirisha ukweli wa matumizi ya mtindo huu kwa wahusika mbalimbali. Sure akizungumzia madhara yaliyoletwa na maenezi ya kasi ya utamaduni wa Kimagharibi anasema:

...*Uzungu unatumeza kwa pupa...* (uk. 2)

‘Uzungu unatumeza kwa pupa’ ni uhaishaji wa utamaduni wa Kimagharibi ambao kimsingi unaenziwa na vijana dhidi ya ule wa Kiafrika unaoshikiliwa na wazee. Hii ina maana kuwa utamaduni wa Kigeni umegubika ule wa Kiafrika na kuzima desturi zake. Tashhisi hii inaeleza kasi ya juu ambayo watu wanaacha utamaduni wa Kiafrika na kuukimbilia ule wa kigeni bila kuutia kwenye mizani na kuuangalia kwa jicho pevu athari zake. Tashhisi hii inatuonyesha kuwa utamaduni wa Kimagharibi umegubika ule wa Kiafrika na kuufanya usihisike kamwe kwa kuwakengeusha Waafrika na hasa vijana ambao wanaupenda.

Baada ya Sure kumweleza Atisa jukumu alilo nalo katika kumpasha Mayaka ujumbe wake, Sure anatumia tashhisi nyingine:

(*Baada ya Kimya.*) Iwapo sheria
haidhuriki hakuna anayejali!
Sifahamu kwa nini kudhurika
kwa jamii *hakutoi kilio kama cha*
kudhurika kwa hiyo sheria. Nasikia
hata hao wataalamu wanasema kuwa
hata *sheria inapenda mambo kama hayo...* (uk. 3)

‘Sheria inapenda mambo kama hayo...’ ni mbinu ya uhaishaji ambapo sheria imepewa uwezo wa kupenda kama afanyavyo binadamu. Hii inamanisha kuwa sheria inakubali mambo ambayo yanapingwa na utamaduni wa Kiafrika. Mwandishi ametumia mbinu hii ili kujaribu kutuwekea wazi masikitiko ya Sure kwa madhara ya sheria hizi ambazo ni zao la utamaduni wa Kizungu. Sure kwa mara nyingine anajaribu kuonyesha ni kwa namna gani hii sheria ina ubinafsi kwani haijali utamaduni wa jamii yake. Anasema kuwa hafahamu kwa nini kudhurika kwa jamii hakutoi kilio kama cha kudhurika kwa hiyo

sheria. Sure analaumu utamaduni wa Kimagharibi kwa kukubali kwa urahisi mambo ambayo utamaduni wa Kiafrika unayapinga vikali.

Sure anamweleza Atisa kwa masikitiko jinsi ambavyo utamaduni wao unapuuzwa kuwa hawana uwezo wa kuutetea. Anamwambia:

...Hata *mila zetu zinauliwa huku
tukiona* bila hata kuatama jambo?
Tunabaki kaka tupu! (uk. 4)

Tashhisi anayoitumia Sure inaonyesha jinsi ambavyo mila na desturi za utamaduni wa kigeni zimevamia zile za Kiafrika na kuchukua nafasi yake kamili kwa kuupuza. Kuua ni sifa ya kitu kilicho na uhai. Mwandishi anajaribu kuonyesha ni kwa njia gani utamaduni wa Kiafrika unafifia na nafasi yake kuchukuliwa na ule wa kigeni kwa kukosa juhudi za kuutetea.

Mayaka, mwanawe Rosa, ameamua kumwoa Bisase aliyemzidi umri licha ya pingamizi kutoka kwa jamii yake. Maamuzi ya Mayaka yanapingana na itikadi za jamii yake. Hali hii inamwathiri sana Rosa na kumfanya kudorora kiafya. Sure anaendelea kumwonya kwa kumtolea tahadhari ya kuathirika zaidi kutokana na kuwazia jambo hilo kuzidi kiasi. Anasema:

... Jambo kama hili mtu anaweza kulitolea
tahadhari lakini *siyo kulitia mabegani.*
*Ulimwengu wenyewe ni mkubwa na
mambo unayobeba ni mazito mno...*
Lau sivyo, *ulimwengu utamfanyia
maonevu makubwa.* (uk. 9)

Ulimwengu hapa umeelezewa kana kwamba ni binadamu ambaye ana uwezo wa kubeba mambo mazito na kumfanyia Rosa madhila. Sure anatumia mtindo huu kumwonya Rosa kujihadhari na mabadiliko yanayojiri kwake kwani kuna mengi mabaya yanayotendeka ulimwenguni. Mwandishi anafafanua maudhui ya mabadiliko huku akionyesha wazi athari zake kwa mataifa ya Afrika yanayoyapapia bila kuwazia kwa kina athari zake.

Rosa anamsihi Sure asijisumbue kumpeleka hospitalini kwa kuwa hali yake kuwa na shinikizo la damu ni jambo la kawaida kwake. Anamwambia:

Hapana haja ya kujisumbua.
Nitapata nafuu. Shinikizo la
damu si jambo geni katika afya
yangu. *Ni mgeni wa mara kwa
mara kwa mara. Huja na baadaye
kwenda.* (uk. 8)

Mgeni ni mtu ambaye si mwenyeji wa mahali fulani. Ni mtu aliyealikwa katika shughuli fulani. Katika usemi wa Rosa shinikizo la damu limepewa sifa ya mgeni wa mara kwa mara kuonyesha kuwa ni hali ya kawaida katika afya ya Rosa. Haya ndiyo madhara yanayowafika wanaopinga mabadiliko ya utamaduni uliozuka katika jamii zao bila kujali matokeo yake wala kuchukua hatua za kuyakagua mabadiliko haya kwa jicho pevu.

Atisa akirejelea maisha ya kikabwela yanayowakumba vijana maskini wanaoishi mjini, anasema:

...Au tatizo ni nauli? Unajua
tena hapa mjini watu hukoga
wakang'ara vizuri, *lakini mifuko
yao haichoki kwenda miayo.* (uk. 26)

'Mifuko yao haichoki kwenda miayo' inamaanisha hali ya ufukara inayowapata watu wanaoishi mijini kwa kukosa pesa hasa vijana ambao hawana njia murua za kujipatia riziki. Maudhui ya umaskini ambayo yanaonekana kuwa chanzo cha vijana kuukimbilia utamaduni wa Kimagharibi na kufumbata desturi na mila zake unajitokeza kwa uwazi zaidi.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, hali ni sawa ambapo pia mtindo huu umejitokeza kwa wingi. Waridi ambaye ni nesi, anasikitikia maradhi ya utapiamlo ambayo hatarajii kuwafika watu katika karne ya ishiringi na moja ambapo mataifa yanastahili kupiga hatua kimaendeleo. Hali inamshangaza na anamweleza Siki:

Daktari, si hivyo tu! Basi!
*Kitoto chenyewe kiriba
chaongoza.* (uk. 5)

Mwandishi anasisitiza ujumbe wake kwa kutalii namna yule mgonjwa alivyolemewa na maradhi ya utapiamlo. Hii ni hali ya kusikitisha zaidi kwa kinaya kwamba watu hawawezi kumudu hata kujipatia lishe bora ili kudumisha afya na jamii zao licha ya

kulifanyia Baraza la mji wa Cheneo kazi. Mwandishi anadhihirisha maudhui ya umaskini ambao ni zao la uongozi uliojaa ubinafsi wa kufaidi wachache huku wengi wakiumia.

Meya akionyesha mojawapo wa sifa zake za kuwa na kiburi na madharau kwa watumishi wake, anamwambia Dida:

*... Hizo pole haziondoi wala
kufuta chochote hata ukizitema
nyingi kiasi gani. (uk. 9)*

Tashhisi ya kufanya ‘pole’ kuwa na uhai ilitumika kuonyesha madharau ya Meya kwa Dida na watumishi wake. Hii ni sifa moja inayoonekana katika janibu zetu ambapo viongozi kwa kuiga kikasuku mienendo ya viongozi wa ukoloni mkongwe, huendelea kuwadhalilisha wafanyikazi wao. Udhalilishaji huu huonekana hata kwa wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali za kuwahudumia wananchi. Na hiki ndicho chanzo cha ubinafsi unaotawala nyoyo za viongozi. Diwani I ni mmjowapo wa vibarakala wanaoendeleza sifa hii ya kuwanyanyasa wanyonge walio wengi katika jamii. Akimhakikishia utulivu kutoka kwa wanacheneo wa kutoleta fujo, anamweleza mpango wake:

*Nitawaambia kutembeza virungu
kiasi cha kuwafanya kutulia
nyumbani. (uk. 19)*

Maelezo ya ‘kutembeza virungu’ yanaonyesha mipango ya Diwani I ya kutumia askari polisi kuwapiga na kuwaumiza wale wafanyikazi watakaofanya maandamano wakitetea haki zao. Hii ni mbinu ya kuwatawanya na kuwazuia kuzua rabsha. Mwandishi anatalii misingi ya kidikteta ambayo huogopa ghadhabu ya wanyonge walio wengi katika jamii na hivyo huwa radhi kutumia mbinu zozote ambazo huwawezesha kutekeleza matakwa yao na kusalia uongozini.

Bili anamhimiza Meya kuhusu umuhimu wa kuenda na majira ya mabadiliko. Kwa kupitisha ujumbe huu anatumia tashhisi kumweleza:

*Ndivyo unavyokwenda ulimwengu.
Lazima ujitahidi kwenda nao maana
ukikuacha nyuma hatua, huna lako.
Bahati haifungui milango yake zaidi ya
mara moja. (uk. 30)*

Bili anamhimiza Meya kuenda na mabadiliko yanayojiri. Ulimwengu umepewa sifa ya kuenda na bahati vilevile ikapewa sifa ya kufungua. Mbinu hii ilitumika ili kudhihirisha jitihada za Bili katika kumshawishi Meya kushirikiana kikamilifu na mwanakandarasi aliyemfurusha katika kulifisidi Baraza la Cheneo kwa faida yake.

Waridi anatumia tashhisi anapomweleza Siki kuhusu kudorora kwa hali ya usafi ambayo ni hatari kwa kueneza magonjwa. Anaonekana kusikitikia hali hii anaposema:

... Hakuna maji ya kutosha.
usafi umetwaliwa na nzi. Ni
hatari hata kwetu sisi. (uk. 36)

‘Usafi umetwaliwa na nzi’ ni tashhisi ambayo mwandishi ameitumia ili kutuonyesha jinsi hali ya usafi ilivyo katika viwango duni. Kwa kutumia mbinu hii mwandishi anafaulu kuelezea jinsi hali ya usafi ilivyo katika kiwango cha chini mno. Mwandishi anaonyesha madhara ya utawala wa mtu mweusi kwa mwenzake ambao umesababisha hali kuwa mbaya zaidi kwa kila hali hata kumzidi mkoloni mkongwe. Hali hii inashadidiwa na maelezo ya Meya ambaye anamweleza Diwani II kuwa:

... Taka zimejaa katika barabara zetu.
anatawala nzi na harufu. Hali hii
tutaiondoaje kabla ya kesho? (uk. 73)

Matumizi ya tashhisi ‘Wanatawala nzi na harufu’ na Meya kwa mara ya pili, yanatufanya kuchora picha na kuwazia kiwango cha usafi zaidi. Mwandishi amewapa nzi na harufu uwezo wa kutawala sawia na binadamu kwa nia ya kuelezea jinsi kulivyojiri mchafukoge katika nchi za bara la Afrika. Viongozi wa nchi hizi kwa kuiga mitindo ya wakoloni wakongwe wamefaulu sana, sio kuzinusuru nchi zao kutokana na majanga yao bali kuimarisha udhalimu uliovuja kwa kila sekta. Dida akitalii ubinafsi unaodhihirika kwa Meya na washauri wake, anaonekana akiwasilisha maudhui haya kupitia uzumgumzi nafsia ambapo anaeleza:

Dida: ... Kazi ya askari nzuri
Bunduki inayotema risasi tatu
tatu...Magari yanayotapika maji.
...Roho ya mtu hapendi mtu imponyoke.
Kwa bahati mbaya ikimponyoka
Wakubwa hueleza haikumtoka.

...Watu wake wana roho za watu
Naye hakusita mbali akazipeleka
*Hata kama mji mzima kwa uvundo
unatisha!* ...(uk. 64)

Mbinu ya tashhisi imetawala sana hapa. Tashhisi ya kwanza ni ile ya ‘Bunduki inayotema risasi tatu tatu’. Maelezo haya yanatupa picha ya kasi ya bunduki katika kufyatua risasi ili kuwaumiza na kuwatawanya wafanyakazi ambao wanatetea haki zao. Tashhisi nyingine ni ile ya ‘Magari yanayotapika maji’. Kutapika ni sifa ya binadamu. Mwandishi anatumia mbinu hii kuonyesha jinsi maji yanavyomwagwa kwa haraka na kasi kutoka kwa magari. ‘Naye hakusita mbali kuzipeleka’ ni tashhisi ambayo inamaanisha kuwa Meya alishughulikia maslahi ya wale wanaomshauri na kushirikiana naye katika kilifisidi Baraza la mji wa Cheneo pekee. Hawa ndio hurejelewa kama ‘watu wake’ na sio ‘viatu’ ambao ni wananchi. Haiwezekani mtu kuchukua roho za watu bali ni tashhisi inaonyesha juhudi za Meya katika kuyashughulikia mahitaji ya waliomuunga mkono katika uongozi wake.

Tashhisi katika uzungumzi nafsia wa Dida imetumiwa na mwandishi kukejeli viongozi wa ukoloni mamboleo ambao wanaweza kuwa na vifaa vya kuwahangaisha kwa udhalimu Wanacheneo wanapogoma kutetea haki zao lakini wakakosa kutatua majanga ya wananchi wao. Kejeli inayojengwa kupitia kwa tashhisi hii inaonyesha wazi namna woga wa kutimuliwa uongozini ndio huwafanya viongozi kuwa katili kwani wanafahamu kuwa hawana tajriba ya kuyaendesha mataifa yao.

Mifano hii kutoka tamthilia teule inaonyesha kuwa mwandishi ameutumia mtindo huu ili kuweza kuelezea ujumbe wake kwa njia ya kuvutia zaidi.

4.2.3 Methali

Kwa mujibu wa M’Ngaruthi (2008) methali ni kifungu cha maneno yanayotumiwa pamoja kisanii, kwa njia ya kufumba na kupigia mfano jambo fulani. Kitula na Ndalu (2009), Wamitila (2003) na Mauya (2008) wana maoni sawa wanapoeleza methali kama usemi mfupi wenye maana pana, na busara au hekima ulio na mizizi katika jamii fulani na unaoelimisha, kuasa au kukejeli watu au vitendo fulani katika jamii lakini kwa njia iliyofumbwa na kuwekewa tasfida. Hivyo basi methali huhifadhi na kudumisha ujumbe wa mwandishi kwa ufupisho wake. Katika kuisitiza umuhimu wa methali, Gesero

(2009) anaieleza methali kama kiungo muhimu cha lugha ambacho hutumika kuyapima maisha huku zikifichua falsafa na hekima ya jamii katika muktadha wa utamaduni maalumu. Katika tamthilia teule mwandishi ametumia methali nyingi kwa malengo tofautitofauti lakini akilenga katika kutoa ujumbe wake ili uwe na taathira fulani kwa msomaji wa matini zake.

Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* imetawaliwa na methali mbalimbali kwa nia ya mwandishi ya kukuza ujumbe wake. Bi. Rahma analalamikia mapishi ya kisasa na kushuku kuwa huenda ndiyo yanamkosesha Sele hamu ya chakula. Anamwambia Zainabu:

... Watavilaje vyakula vya kuharakishwa?
Heri huvutwa kwa subira mama. Vyakula
visivyopata kutua sufuria, vipi vitatua
moyoni? (uk. 14)

Methali anayoitumia Bi. Rahma ina maana kwamba kizazi cha kisasa hakina subira katika kutekeleza majukumu hasa kimapishi. Zainabu anajitetea dhidi ya madai ya Bi. Rahma. Bi. Rahma bado anaonyesha shaka yake anapotumia methali hii:

Au labda mkono ni ule ule mmoja wa
upishi. Usisahau kuwa *Mchele mmoja*
lakini mapishi mengi. Hili hukipa upya
na ugeni chakula... (uk. 15)

Methali ya kwanza ni ‘Subira huvuta heri’ ambayo inamaanisha kuwa mtu mvumilivu ndiye hufanikiwa maishani. Methali hii imebadilishwa kimpangilio na kuwa: ‘Heri huvuta subira’. Methali hii imepanguliwa kimaksudi ili kuonyesha kuwa katika mafanikio ya Zainabu kumpikia Sele chakula na akile yanahitaji uvumilivu na asikate tamaa kwani huenda akasalimu amri na kula chakula ambacho kwa sasa anakikataa. Bi. Rahma anasisitiza umuhimu wa kuyaandaa mapishi kwa utaratibu.

Methali nyingine ni ‘mchele mmoja mapishi mengi’ ambayo inamaanisha kuwa kuna njia mbalimbali za kulifanya jambo fulani na kufanikiwa kwani jambo lenyewe hutegemea ujuzi wa mtekelezaji. Bi. Rahma ndiye anaitumia akimwasa Zainabu ili ajitahidi kutumia ufundi na njia tofauti za kupika vyakula mbalimbali kwa kuwa anashuku kuwa huenda Sele hali chakula kwa kuwa hakiandaliwi kwa ufundi maalumu. Methali hizi zimetumika

kama ishara kuwa Bi. Rahma haelewi kwamba kinachomsibu Sele ni zaidi ya hiki chakula.

Methali nyingine katika tamthilia hii ni ‘mhitaji siku zote ni mtumwa’. Methali hii inatumiwa na Musa akimwambia Zainabu ambaye ni mkewe. Anarejelea kuwa hali ya Sele kuachishwa kazi ndiyo iliyosababisha hali ya kuugua kwake kwani alikuwa anategemea kazi yake katika kujikimu na kuikimu familia yake changa. Musa anasema:

Mhitaji! *Mhitaji* mke wangu
siku zote mtumwa. Na wao
wanajua. (uk. 25)

Hii ina maana kuwa mtu ambaye anataka au anategemea jambo fulani ili limfae basi huwa mtumwa wa jambo lenyewe analolitegemea. Sele alikuwa anategemea kazi ili kuikimu aila yake na ndiposa wahusika wengine tamthiliani wanadhani kuwa aliathirika baada ya kuachishwa kazi. Washikadau wa mfumo wa kiuzalishaji wa kibepari wanajua kwamba wakazi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu hawana uwezo wa kujitegemea kwa kuwa wamezifilisisha rasilimali za nchi zao. Hii ndiyo sababu kuu ya wao kuwadhalilisha katika sekta mbalimbali kwa kuwa hawana jingine la kutegemea katika maisha yao ila kuwategemea wao licha ya kuwanyonya nguvu zao.

Methali nyingine inajitokeza katika usemi wa Musa. Akimweleza mkewe, Zainabu, umuhimu wa kuwa na utaratibu, anasema:

Tumpe muda. Tusifanye kama
tunashinikiza. Atakubali.
Pole pole ndio mwendo. (uk. 26)

Musa anatueleza kuwa ikiwa tunataka mafanikio, ni lazima tutende mambo kwa mpango na utaratibu na sio kuyaharakisha.

Bi Rahma anatumia methali nyingine akimtahadharisha Sele dhidi ya kupigana na mabepari wanaomshinda katika uwezo wa kuzalisha mali. Anatumia methali hii:

Wahenga walisema, *mwenye nguvu*
mpishe! Sasa utapigana nao? ... (uk. 29)

Bi Rahma anamwonya Sele asijaribu kuwapiga vita wenye uwezo kiuchumi maana yeye ndiye ataathirika. Hii ni ishara kuwa woga ni chanzo cha wakazi wa nchi changa kuridhia madhila ya kibepari kwa kujiona maskini.

Aisha akimhimiza Sele asitishike na lawama na kukosolewa na watu katika vitendo vyake, anatumia methali hii:

Kwa nini uyajali sana ya watu?
Mchana watasema usiku watalala... (uk. 34)

Sele anashauriwa kutojali yanayosemwa na watu kumhusu maana hayana manufaa kwake. Aisha alikuwa na nia na kumhimiza Sele katika kujithamini na kutofuatilia yaliyokuwa yakisemwa na watu kwa kuwa hayana umuhimu sana. Na ndiposa anasema kuwa ‘Mchana watasema usiku watalala’ ambayo katika uhalisia huwa: wasemao mchana usiku watalala.

‘Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo’. Methali hii inamaanisha mtoto hufuata tabia na anayofunzwa na wazazi wake na haifai kumlaumu mtu kwa tabia ya huyu mtu hasa inapobadilika na kuwa mbaya. Amri anatumia methali hii akimrejelea Musa kwa maana hiyo. Anasema:

Si nyinyi mlionza kumwonyesha
hao madaktari? Sasa anafahamu wako.
Hata ahisi kuwa lipo jambo dogo
linalomsumbua atakimbia pale pale
mlivyomwonesha nyinyi. *Umleavyo*
atakuwa hivyo. (uk. 63)

Methali ‘umleavyo atakuwa hivyo’ haijakamilishwa kama ilivyozoeleka. Hata hivyo maelezo ya kimuktadha yanaifafanua. Amri anataka kumshauri Musa kwa uwazi kuwa wao ndo chanzo cha hali ya Sele na asilalamike kwani wao ndio waliomwelekeza anavyofanya.

Katika hatua za kutafuta chanzo cha ugonjwa wa sele, Bi Rahma anamweleza mbinu za kuweza kumsaidia kufahamu hali hii. Anatumia methali hii ‘maneno matamu humtoa nyoka pangoni’. Methali hii hutumiwa kuwaonya watu kuwa matatizo sugu hayawezi kusuluhishwa kwa ugomvi bali kwa upole na maelewano. Maana hii ndiyo hasa

inayokusudiwa katika maelezo ya Bi. Rahma anapomwusia Aisha atafute njia mwafaka ili apate ukweli wa maradhi ya Sele. Anamwambia:

... Utie ulimi asali na atakwambia
kila kitu. *Utamtoa nyoka pangoni
mama.* (uk. 21)

Bi Rahma anatumia methali hii kumshajiisha Aisha katika kutumia maarifa na upole ili kuwe na maelewano kati yake na Sele. Maelewano haya yatamsaidia kuelewa ugonjwa wa Sele kwani kupitia kwa maneno mazuri Sele atalainika na kuweza kumfichulia siri ya ugonjwa wake.

Tamthilia ya *Chamchela* pia ina methali nyingi zilizotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wake. Moja kati ya hizo methali ni ‘mtu hujikuna ajipatapo’. Methali hii inamaanisha kuwa mtu hujikuna mkono wake unakofikia, yaani hutenda mambo yaliyo katika uwezo wake. Hii methali huwatahadharisha watu dhidi ya kutenda mambo yanayozidi uwezo wao ambayo mara nyingi huishia kuwashinda. Maana hii ndiyo aliyokusudia Sure anaposema:

Wewe unaona ndio nini hivi?
Ikiwa hatuwezi *kujikuna pale
tunapojipata* hii ina maana gani? ... (uk. 4)

Sure anaonyesha kukata tamaa katika kushindwa kutatua shida wanazozuweza. Mbinu ya balagha katika methali hii ilinuiwa kumhamasisha Atisa kufanya jitihada za kutafuta suluhu kwa mgogoro wa ndoa ya Mayaka. Methali hii inayakinishwa tena na mhusika yuyu huyu anaposema:

... Hivyo huwezi kuukabidhi
ulimwengu mzima na kuukabili.
Mtu hujikuna ajipatapo. Nadhani
muhimu ni kujaribu kujikuna. (uk. 9)

Sure anatambua kuwa hata akikata tamaa ya mapigano na mila za kimagharibi zilizowaparamia vijana, atakayepoteza ni yeye na jamii nzima. Katika muktadha huu anaona ni vyema kujaribu kadri ya uwezo wake kuliko kutupa jongoo na mti wake. Anagundua kuwa kujaribu kumtafuta Mayaka na kumshauri kunaweza kuleta afueni ikiwa hataghairi ushauri wao.

‘Hasikii la mwadhini wala mteka maji msikitini’ ni methali inayaoshiria watu ambao mara nyingi hawasemezeki kwa baya au zuri. Ni watu ambao hawashauriki. Sure anaona kuwa Rosa anaumia kwa kukataa kufuata ushauri wake. Ndipo anasema hivi:

...nimemshauri kutojiweka katika
hali hii ila haelekei kusikia. *Si la
mwadhini wala mteka maji msikitini...* (uk. 7)

Rosa anaendelea kuumia kwa kuwa hashauriki. Mwishowe analemewa kwa hali hii na kuwa mahututi kutokana na kukosa busara ya kukubali mabadiliko ambayo yalifika mapema. Sure tena anaitumia methali hii kwa maana ileile akiwa na wazee wenzake ambapo wanajadili ugumu uliopo katika kutatua hali inayowasibu. Anawaambia:

Naam wazee wenzangu! Jambo
hili hata hivyo ni gumu. *Ila halisikii
la mwadhini wala la mteka maji msikitini...* (uk. 46)

Anaonyesha hali ngumu inayowakumba katika kusuluhisha mgogoro wa ndoa inayoenda kinyume na mila za Kiafrika. Atisa akiwa ameona ugumu wa kusuluhisha mgogoro huu anasema:

Ami, mimi nina *macho* na hivyo
sitangoja *kuambiwa tazama...* (uk. 47)

Methali hii inastahili kuwa ‘mwenye macho haambiwi tazama’. Katika muktadha huu, methali hii imeparaguliwa. Atisa alitaka kusisitiza ujumbe wake wa kuona mambo yalivyoenda mrama na kwamba yasingeweza kutatuliwa. Anaonyesha kuwa hamna tumaini la kubadili uamuzi wa ndugu yake Mayaka. Sure anaonyesha ufahamu kuwa mabadiliko yaliyozuka na kushamiri yanahitaji kukubalika kwani ni ya kudumu.

Sure anawapa Abaya na Kobia matumaini ya kuwashajiisha. Anatumia methali hii ‘penye wazee hapaharibiki neno’. Methali hii ina maana ya kuwa umuhimu wa wazee au watu wazima katika mashauriano ili kusuluhisha majanga hauwezi kupuuzwa. Sure anafahamu maana ya methali hii na ndio sababu anajadiliana na wazee wengine. Anasema:

...Bila shaka hali hii ni ngumu
lakini wahenga wetu wanatuhakikishia
kuwa *penye wazee hapaharibiki neno...* (uk.46)

Imani katika methali hii inawafanya kuamini kuwa wao wanastahili kuwaelekeza vijana kwa kuwa wao ndio wenye busara. Methali hii inaonyesha chimbuko la mgogoro mzima wa kukosa maelewano kati ya wazee na vijana mtawalia. Inaelekea kuwa msemu huu ndio unaowafanya wazee kukataa kukubali kuheshimu misimamo ya vijana. Methali hii imetumiwa kama kejeli na mwandishi kwani wazee ndio walioshindwa kutekeleza wajibu wao na sasa wanawalaumu vijana ambao kwa ukakamavu wako radhi kusimama imara na kujitetea vikali.

Bisase anaonyesha kwa uwazi kuwa chanzo cha kumchukua Mayaka ni upweke uliomkosesha mtu wa kumwauni. Mwanawe Sera ambaye badala ya kumfariji amejipa shughuli na hata kumtwika jukumu la kumlea Lema. Aliamua kumchukua Mayaka kwa kuzidiwa na upweke. Sera anapolalamikia hili, Bisase anamkabili kwa methali hii:

*... Kamba ya mbali haifungi kuni.
Nyinyi mmejitanibu na kukubali
kutekwa nyara na mahangaiko ya
dunia. (uk. 22)*

Methali hii ina maana ya kuwa vitu vilivyo karibu na mtu ndivyo humsaidia anapokuwa na janga. Mayaka ndiye aliyemsaidia Bisase kwa kuwa karibu naye alipohitaji usaidizi.

‘Mavi ya kale hayanuki’ ni methali yenye maana kuwa mambo ambayo yalitendeka hapo awali hayana umuhimu kwa yale ya wakati huu. Methali hii imetumiwa na Mayaka akiielekeza kwa Atisa ambaye anamkumbusha kuhusu Sabina, mpenzi wake wa awali. Kwa kuwa hataki habari hizi, anamwambia:

*Huo ni wakati ule Atisa.
Ni kipindi kirefu. Ni kale.
Hayanuki tena. (uk. 27)*

Mayaka anamkabili Atisa kwa methali hii kuonyesha kuwa hayuko tayari kukumbushwa habari za Sabina ambaye alikuwa mchumba wake wa awali kwani hamhitaji tena. Methali hii imekatwa kwani ililenga tu kuisisitiza wazo la Mayaka la kusahau yaliyopita. Hakutaka kukumbushwa yaliyopita kwani hayakuwa na umuhimu wowote kwa maisha yake ya sasa.

Kofa akimweleza Rukia kuhusu uamuzi wa Mayaka wa kumwoa Bisase licha ya kumzidi kiumri, anasema:

... Suala la ndoa ni suala la
mtu binafsi. *Kipenda roho hula
nyama mbichi...* (uk. 36)

Methali ‘Kipenda roho hula nyama mbichi’ ina maana ya mapenzi ya dhiti huweza kumfanya mtu aamue na kutenda jambo lolote kwa yule anayempenda. Hakuna dawa ya mapenzi. Licha ya malalamiko kuwa Mayaka ameenda kinyume na desturi na mbeko za jamii, Kofa anamtetea kwa hili.

Mazungumzo kati ya Bisase na Mayaka yanadokezewa na methali hii: akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. Methali hii inamaanisha kuwa mtu anayekuauni wakati wa shida ndiye rafiki wa kweli. Maana hii ndiyo aliyokuwa akirejelea Bisase alipomwambia Mayaka:

... *Akufaaye kwa dhiki
ndiye rafiki.* (uk. 41)

Bisase anaitumia methali hii kumshawishi kuupuzilia mbali ushauri wa watu kwa kuwa hawamfai ila yeye. Methali hii inaonyesha ukakamavu wa Bisase pamoja na milki yake ambayo ndiyo chambo kilichomnasa Mayaka kwake.

‘Wengi wape’ ni methali nyingine ambayo imetumika katika tamthilia hii ya *Chamchela* ili kukuza ujumbe wa mwandishi. Methali hii hututahadharisha kuwa tusishindane na wengi maana huenda tukahasirika. Maana hii ndiyo aliyokusudia Mbiki alipomwambia Mayaka:

Wengi wape ni moja katika vito
ambavyo vinavyoonyesha wingi
wa hekima katika lugha yetu.
Mimi naona ufikirie tena ... (uk. 76)

Methali hii ilitumiwa ili kumwonya Mayaka dhidi ya kung’ang’ania kutaka kuwoa Bisase kinyume na makubaliano ya jamii yake. Hii inamfanya kusemwasemwa na kutengwa.

Methali nyingine ni ‘haraka haraka haina baraka’. Methali hii hutumika kuwaonya watu kuwa mambo yanayofanywa kwa pupa mwishowe huharibika. Methali hii inapokea jibu

la kinyume ambalo linaonekana kuikanusha kupitia kwa methali ‘Ngoja ngoja huumiza matumbo’ yenye maana kuwa kuchelewesha kwa mambo fulani huleta hasara.

Methali hizi zinakinzana kimaana. Hili analifanya mwandishi kimaksudi kuelezea kuwa mambo hayatakiwi kufanywa kwa pupa na kwa wakati huo huo yasicheleweshwe kiasi kwamba hayatawafaa wahasiriwa. Hii inadhihirika katika majibizano kati ya Sera na Bisase.

Sera: (*Kwa upole sana.*) Lakini mama, si ni wewe umesema sasa hivi kwamba *haraka haraka haileti Baraka?*

Bisase: *Ngoja ngoja* nayo ya kipindi kirefu ni mchezo unaosubiri kutumbua usaha. (uk. 19)

Methali hizi japo zinakinzana kimaana zinaimarishana kuwa mambo fulani huhitaji dharura katika kutekelezwa. Hapa Bisase anajaribu kumfafanulia Sera umuhimu wake kumfahamisha Lema kwa babake kwa kuwa amengoja hadi akafikia umri wa kutaka kumjua yeye mwenyewe. Methali hizi mbili tena zimetumika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Kinachodhihirika ni kuwa methali zote hufasiriwa kutegemea miktadha husika.

Mazungumzo katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* yanaonyesha matumizi ya methali. Siki akitaka kumjuvya Waridi umuhimu wa kuwashughulikia wagonjwa licha ya kutokuwepo kwa dawa, anamkabili kwa methali hii:

Wakisubiri na ugonjwa nao utasubiri?
Hujui ngoja ngoja huumiza matumbo? (uk. 2)

Waridi naye katika kumjibu anamkabili kwa methali hii:

Haraka haraka haina baraka.
Usisahau kuwa Mstahiki Meya
mwenyewe amesema. (uk. 2)

Methali ya ‘ngoja ngoja huumiza matumbo’ huwa na maana kuwa tabia ya kuchelewachelewa kufanya mambo husababisha hasara. Methali hii imetumiwa na Siki ikifungamana na mbinu balagha ili kuonyesha hali ya dharura iliyopo katika kuwatibu wagonjwa. Methali hii inapokea jibu kutoka kwa Waridi kuwa ‘haraka haraka haina baraka’. Methali ina maana kuwa ili tufanikiwe lazima tuwe wavumilivu na makini katika kutenda lolote. Mkinzano unaokuzwa na methali hizi unadhihirisha kuwa japo

mambo huhitaji subira kuna hali zingine ambazo hutaka kushughulikiwa kwa dharura kama magonjwa.

Methali nyingine inajitokeza katika mazungumzo kati ya Meya na Diwani III ambapo Meya anamwambia Diwani III kuwa ‘wengi wape’ kumaanisha kwamba mtu mmoja hawezi kufaulu kushindana na makubaliano ya wengi. Hii inakuwa kama tahadhari kwa Diwani III kuacha kushindana na wanaomzidi kwa nguvu serikalini.

Ni uamuzi wa Baraza.
Ni demokrasia hii.
Wengi wape. (uk. 22)

Bili anamsaidia Meya kuelewa manufaa ya kumwacha mwanakandarasi aliyefutwa aende kumshtaki kortini. Katika kumhakikishia faida itakayopatikana, Bili anatumia methali hii:

Wahenga wanasema *dawa ya adui ni kummegea unachokula.*
Ukisha kula naye hataku dhuru. (uk. 29)

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011) adui ni mtu aliye dhidi yako au kitu kibaya unachopambana nacho. Katika muktadha huu adui ni mwanakandarasi aliyemfurusha Meya. Methali hii ina maana kuwa njia pekee ya kumzuia adui kukutendea mabaya ni kumwonyesha ukarimu kwa kumfaidi. Meya anashauriwa kufanya maelewano ya manufaa kwa mwanakandarasi ili naye afaidi asije akahukumiwa. Licha ya ushauri wa Bili, Meya anaonekana kuwa mwenye wasiwasi kwa kuwa anaogopa kesi zinazoendeshwa kortini. Anamuuliza Bili:

Ajidungaye mwiba hufaidi nini Bili? (uk. 29)

Methali hii ‘ajidungaye mwiba hufaidi nini?’ japo imetumika kibalagha ni sawa na ‘mwiba wa kujichoma hauambiwi pole’. Methali hii inamaanisha kuwa mtu anayefanya jambo baya lenye kumdhuru hana wa kumwambia pole. Meya anapoitumia methali anaonyesha kuwa hayuko tayari kufika mahakamani kwa kushtakiwa kwa vitendo vyake vya kutofuata sheria kama ile ya kumfurusha mwanakandarasi kabla ya wakati wake wa kandarasi kutimu. Matamshi haya yanaendeleza maudhui ya ubinafsi

Woga wa kung'olewa uongozini unamfanya Meya kukataa ushauri wa kweli. Badala yake Meya amewapa vikaragosi wake milungura kwa kumtumikia. Diwani III amemshauri mara kadha bila mafanikio na anaonekana kukata tamaa katika maelezo yake kwa Siki:

Sikio la kufa halisikii dawa daktari.
Huyu ndugu yako nimesema naye. (uk. 46)

Methali 'Sikio la kufa halisikii dawa' hutumiwa kuelezea jambo ambalo linaharibika huharibika tu hata tukifanya juhudi gani kuzuia. Methali hii inarejelea ugumu wa Meya kusikiliza ushauri wa ukweli wa kuiendesha Cheneo kwa manufaa ya wote. Methali hii inadhihirisha kuwa Meya hasemzeki. Ni mtu mgumu katika kushauriwa. Na hiki ndicho chanzo cha kutokuwa na maendeleo yanayowanufaisha wakazi wa mataifa machanga ya ulimwengu wa tatu kwani viongozi hujiona bora kwa hatua wachukuazo katika maongozi yao.

Methali alizozitumia mwandishi huyu ni nyingi na amezitumia kwa ufundi wa hali ya juu. Ametumia methali hizi kufupisha masafa ya kuelezea ujumbe wake na wakati mwingine kutilia mkazo na mvuto wa yale ambayo anazungumzia. Hii humtafakarisha msomaji katika kufumbua maudhui anayowasilisha mwandishi. Mtindo huu wa kutumia methali umetamalaki sana katika tamthilia teule na kutekeleza wajibu ule ule wa kudumisha na kuleta mvuto katika ujumbe wa mwandishi kwa njia maalumu. Kinachobainika hapa ni kuwa mara nyingi mwandishi anapangua mpangilio ambao umezoeleka wa methali na kudokeza baadhi ya methali katika kujalizia ujumbe wake. Aidha, methali zote zinapata ufasiri wake kutegemea miktadha ya matumizi kwenye kazi ya fasihi ambayo inahusika na lengo la mwandishi. Pia ni wazi kuwa methali huchukua nafasi mbalimbali katika tamthilia husika kutegemea ujumbe unaojengwa na mwandishi.

4.2.4 Tabaini

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) tabaini ni mtindo wa kiusemi wa kulisisitiza jambo kwa kutumia maneno yanayoelekea kutoonyesha msisitizo huo waziwazi. Kamusi ya TUKI (2004) inatoa ufafanuzi unaokaribiana na huu inapoieleza tabaini kuwa ni mbinu yenye dhana ya kukinzana lakini maana ya msingi haitenguki. Kwa hivyo tabaini ni mbinu ya kulisitiza kwa kutumia maneno ambayo kwa maana ya juujuu yanaonekana kukanusha.

Tabaini hutambulishwa kwa kikanushi ‘si’. Mtindo huu unajitokeza katika tamthilia teule ili kusesitiza ujumbe kwa njia mbalimbali.

Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* inaonyesha tabaini alizotumia mwandishi katika kuelezea hali mbalimbali kwa msisitizo wa kitabaini. Aisha anaelezea jinsi muziki unavyoweza kutuliza na kuburudisha watu wa umri wowote. Katika kuelezea athari hii anasema hivi:

Sina shaka. Viumbe wote hufurahia
muziki; *si binadamu, si wanyama,*
si miti; ndoo maana hata kizee utakiona
kikitingisha kichwa kwa mlio wa uzi dhaifu
wa gitaa... (uk. 6)

Mwandishi anatuchorea picha ya athari ya muziki kwa kila kiumbe ulimwenguni katika kuliwaza na kutuliza.

Bi Rahma anashuku kuwa huenda Sele hali kwa sababu ya maandalizi duni, anamhimiza Zainabu kumpikia vyakula mbalimbali na kwa ustadi mkubwa ili vipate kuwa na ladha. Zainabu naye anamwonyesha namna mapishi yake yalivyo na ladha. Anajitetea kwa maelezo haya:

Hata kitoweo chabadilishwa.
Kama *si pojo ni nyama, si ya*
kuku, si ya ng’ombe au samaki
... mara wa kupaka, mara wa
kukaanga. (uk. 15)

Maneno ‘Kama si pojo ni nyama, si ya kuku, si ya ng’ombe’ yanadhihirisha mbinu ya tabaini. Mwandishi anatumia maelezo haya kuonyesha kuwa Sele amepikiwa kila aina ya chakula bila mafanikio ya kumvutia. Hii ni katika kumhakikishia Bi. Rahma kuwa hali ya Sele haihusiani na mapishi kwa vyovyote vile.

Sele anakumbuka nyimbo za Siti binti Saad zilivyokuwa na umaarufu katika ujumbe pamoja na mahadhi yake. Sifa hizi zinamfanya amwombe Bi Rahma kumwimbia wimbo mmoja wa mwanamuziki huyo. Anasema:

Waukumbuka ule wa siku ilee
... Nasikia alikuwa mwimbaji
hodari; *si maneno si sauti.* (uk. 45)

Hii inaonyesha Siti binti Saad alivyokuwa mwimbaji hodari katika sauti nzuri na maneno pia. Hili ni fumbo linaloonyesha jinsi Waafrika walivyoukimbia utamaduni wao na kufuata ule wa kigeni ambao sasa unawahangaisha.

Hulka ya Sele imewashinda wahusika wengine wote. Hamsikii yeyote katika ushauri wake. Musa analamikia hali hii anaposema:

... Hajali anavyowahasiri
wengine. *Si mke wake, si
mama yake au bibi yake.*
Ameshika lake na ndo basi.
Ni kama sikio la kufa... (uk. 64)

Maelezo haya yanaonyesha kuwa hakuna ambaye anaweza kumshauri Sele kwa kuwa hampi fursa. Musa anaonyesha hali ya kukata tamaa katika kumshauri Sele kwa kuwa haambiliki wala hasemezeki. Haya yote yanachangiwa na wahusika wengine kutoelewa mwamko mpya wa kisiasa alioupata Sele.

Katika *Chamchela* hali ni sawa ambapo matumizi ya tabaini yanaendelea kutumika katika kuusisitiza ujumbe wa wahusika. Kwa mfano, Abaya akielezea ni kwa vipi wazee walizembea katika kuwafunza vijana utamaduni wao, anasema:

... wakaingia katika malevi;
si dawa za kulevya, si tembo,
si uhalifu... (uk. 54)

Mwandishi akitumia mbinu hii ‘si dawa za kulevya, si tembo, si uhalifu...’ kwa masikitiko anaeleza kwa kusisitiza kwamba baada ya wazee kutepetea katika kuwafunza vijana utamaduni wa Kiafrika na badala yake wakawafunza kuchuma hela ambazo ni hulka ya utamaduni wa Kimagharibi, vijana sasa wamegeukia kila aina ya uovu ambao unapatikana katika jamii. Hii ndiyo hali inayofanya vijana kuinukia kufuata utamaduni wa Kigeni kwa haraka mno. Hali hii ilitokana na mapuza kwa upande wa wazee

Atisa akimweleza Mbiki kuwa ubinafsi ndio unaokosesha matumaini ya kupata suluhu la ndoa ya Mayaka kwani kila mmoja anataka maoni yake yakubalike huku akipuza ya wengine au kutotaka kuyasikiliza kamwe. Anaeleza haya:

... Kila mmoja anataka kuvutia kwake.
Si Mayaka, si mama, si wewe. Paa la
nyumba halijengwi bila miti kuchongwa
vizuri ili ipate kuingiliana... (uk. 71)

Kwa maneno ‘si Mayaka, si mama, si wewe.’ tunajua kuwa ni tabaini. Mwandishi ametumia mtindo huu ili kuelezea hisia za Atisa kuhusu kukosa suluhu kwa mgogoro mzima wa ndoa ya Mayaka na Bisase. Hii inatokana na hali ya kila mmoja wa wahusika hawa kutaka fikra na ushauri wake kukubalika na kusahau kwamba wengine pia wana mchango wao.

Mbiki anatumia mtindo huu akimwelezea Mayaka hali mbaya ya mamake ambaye alikuwa anaugua hospitalini. Anasema:

Si mzima si mahututi. (uk. 72)

Mwandishi anatumia mbinu hii kuweka wazi hali ya Rosa ambayo ni mbaya kiasi kwamba haiwezi kutabirika. Kwa maneno ‘Si mzima si mahututi’ tunafahamu kuwa Rosa hayumo katika ufu wala uzima. Yu taabani kwa kuwa amedhoofika kiafya. Tunabaini athari ya mabadiliko kwa wale wasiokuwa tayari kuyakubali na kuyakabili yazukavyo katika jamii. Matokeo ya kufumbia mabadiliko macho ni maafa ya kujitakia.

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* imedhihirisha matumizi ya mtindo huu wa tabaini kwa njia mbalimbali. Waridi akimwelezea Siki kuhusu habari za umaskini wa nchi yao, anasema:

Nasikia tu! *Si vyombo vya habari,*
si wanasiasa, si wasomi. (uk. 3)

Katika mfano huu, mwandishi anaeleza kuwa ‘Si vyombo vya habari, si wanasiasa, si wasomi.’ Hapa mbinu hii imetumika kuonyesha kwamba habari hizi za nchi kuwa maskini zimeenea na kujulikana kila mahali. Msisitizo unapatikana katika mbinu hii kwa maana kimsingi vyombo vya habari, wanasiasa na wasomi ndio hupitisha ujumbe wa hali ya uchumi ya nchi zote kwa kuwa wanaaminiwa kutangamana na wengi ulimwenguni.

Siki anaeleza ilivyo vigumu kwa Meya kusikiliza kilio cha wanacheneo na kuchukua hatua ya kuwasaidia kwani amegubikwa na ubinafsi. Ni kama Siki anaonyesha kukata tamaa kutokana na maelezo ya Diwani wa III. Anasema:

Yaonekana basi hali si hali. (uk. 51)

Analojiuliza hapa msomaji ni vipi hali ikose kuwa hali. Kwa maelezo haya msomaji anaelewa kuwa ujumbe alionuia kuelezea mwandishi ni ule ugumu unaojitokeza katika maslahi ya wanacheneo kushughulikiwa katika jamii iliyojengeka kwenye misingi ya ubinafsi na ufiada. Hivyo basi inadhihirika kuwa kuna ukweli uliofichika katika kauli hii.

4.2.5 Kwelikinzi

Hii ni mbinu ambayo huonekana ikijipinga kijuujuu ingawa inapochunguzwa kwa makini inadhihirisha ukweli fulani (Corbett, 1971). Akijalizia maelezo ya Corbett, Wamitila (2008) anaeleza kuwa katika kuchunguza kwelikinzi, mambo mawili ya kimsingi yanahitajika. Kwanza, kutambua maana ya kijuujuu ambayo inaonyesha huu ukinzi na pili, maana ya ndani na ambayo ndiyo haswa aliyoikusudia mwandishi kumpokeza msomaji wake. Hii maana ya pili ndiyo inahitajika msomaji aitambue licha ya kusaidia katika kukuza ukinzi huo uliopo.

Tukiangalia tamthilia ya *Mstahiki Meya* tunaweza kudhihirisha ukweli wa mtindo huu. Katika kuelezea mateso ya wanacheneo kwa Meya, Siki anatumia mbinu hii ili kutilia mkazo ambao anataka umguse Meya ambaye ameridhika licha ya mambo kuzidi kuwa mabaya kwa wananchi kiasi kwamba hawawezi kujikimu na kukimu maisha ya familia zao. Anasema:

*... Tunatembea lakini hatuendi mbele.
Kwenda twaenda lakini kinyumenyume...
Kama huku si kuwatusi wananchi basi ndio
kutembea nyuma ya punda aliyeudhika. (uk. 14)*

‘Tunatembea lakini hatuendi mbele. Kwenda twaenda lakini kinyumenyume.’ ni maelezo yanayoonyesha mkinzano kwani tunajiuliza ni vipi mtu anaweza kutembea bila kupiga hatua ya kusonga mbele; yuko pale pale? Ni vipi mtu anaweza kutembea kinyumenyume? ‘kuzorota kwa maendeleo.’ Mwandishi kwa kutumia mbinu hii anaonyesha ni kwa njia gani ubinafsi wa Meya na vibarakala wake ambao wanamzunguka umekwamiza na kuzorotesha maendeleo katika Cheneo kwa vile hali imekuwa mabaya zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali labda kabla ya yeye kuwa Meya.

Madai haya yanatokana na maelezo ya Cheneo kuendelea lakini ‘kinyumenyume’, yaani inaendelea kuzorota kimaendeleo.

Mtindo huu pia unajitokeza katika matamshi ya Diwani III wakizungumza na Siki ambapo Diwani III anataka kuchora picha ya kinyume kuhusu uchafu uliojaa tele na kuenea kwenye mji wote. Anasema:

Huo ndio ukweli... *Hii harufu mbaya ya taka inayoupamba mji wetu ni kiwakilishi tu cha uozo ulio ndani.* (uk. 51)

Kwa mujibu wa TUKI (2004) neno ‘kupamba’ lina maana ya kunadhifisha na kufanya kitu, mahali au mtu kupendeza kwa nguo nzuri, maua au manukato. Diwani III amelitumia neno pamba kwa njia ambayo inaleta mkinzano kwani taka huchafua mji na si kuufanya upendeze kwa kuupamba. Kwa maneno ‘Hii harufu mbaya ya taka inayoupamba mji wetu’ mwandishi alitaka tupate picha kamili kuhusu hali ya usafi ilivyokosekana katika mji kwa kuwa uchafu ulienea kila pahali. Hii ni ishara ya uozo uliotawala uongozi wa Meya.

Diwani III akimshauri Meya kuhusu umuhimu wa kuangalia maslahi ya wafanyakazi waliogoma kwani ni wao waliomchagua, anatumia mtindo huu kumwonyesha Meya umuhimu wa kushughulikia mahitaji ya waliogoma kwani kazi wanazolifanyia Baraza la mji ndizo haswa zinazomwezesha Meya kutekeleza wajibu wake wa umeya. Diwani anamwambia Meya hivi:

Ndiyo sababu ya kusema kuwa
Baraza linawahitaji wao jinsi wanavyolihitaji Baraza. Hakuna bwana hakuna mtumwa. Nafasi tulizo nazo ni za kutuwezesha kuhudumiana. (uk. 55)

‘Hakuna bwana, hakuna mtumwa.’ ni maelezo yanayokinzana. Hapa msomaji anajiuliza kama hakuna bwana wala mtumwa basi kuna nini? Mkinzano huu anaoukuza mwandishi ulinuia kumkumbusha Meya umuhimu wa kuwaheshimu wafanyakazi wa Baraza na kutowapuuza kwani yale wanayolitendea Baraza yanamfaa hata yeye Mstahiki Meya katika kutekeleza wajibu wake. Kupitia kwa matamshi ya Diwani III tunafahamu kuwa

Meya anawadharau wafanyikazi wake. Meya anafaa kuwahudumia wafanyikazi kama wanavyomhudumia yeye ili Cheneo iweze kufanikiwa kimaendeleo. Maelezo haya ni ya kusesitiza shabaha ya mwandishi kwamba maendeleo yanaweza kupatikana katika jamii iliyojengeka kwenye misingi ya usawa na utu. Jamii ambapo heshima inatawala katika misingi ya uzalishaji mali kwa manufaa ya wote.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, mtindo huu unajitokeza kwa njia mbalimbali kupitia kwa wahusika wake. Sele, nguli wa tamthilia hii analalamikia maonevu yake tangu utotoni. Anayaeleza maonevu haya ifuatavyo:

... *Siku zile machozi yalinitoka
kabla nianze kulia. Sasa ninalia
bila machozi kutoka. Hulia ndani
kwa ndani yasionekane. Na... (uk. 43)*

Maneno ‘Siku zile machozi yalinitoka kabla nianze kulia. Sasa ninalia bila machozi kutoka’ ni maelezo yanayokinzana kwani ni vigumu machozi kutoka mtu bila ya kulia na kwa wakati huo huo ni vigumu mtu kulia bila machozi kutokea. Mwandishi ametumia mtindo huu katika kuelezea kuwa taabu za Sele zilianza mapema mno katika maisha yake. Hili ni dhihirisho la hali mbaya inayowakumba wakazi wa mataifa machanga kwa kuwa matatizo na maonevu yao yana historia ndefu na yalianza zamani. Maonevu haya kwenye misingi ya kiuchumi ndiyo chanzo chao katika kukata tamaa. Hii inaashiria hali mbaya na ya kusononesha ambayo huwapata wale ambao wamekwishatambua maonevu yanayotendewa wanajamii wao na tena katika jamii zao kwenye misingi ya uzalishaji na ugavi wa rasilimali.

Aisha anataabikia hali ya Sele na anashindwa kuieleza kwani haikadiriki. Anaeleza:

Ni kama *dogo si dogo; kubwa
si kubwa. Mara nahisi ni dogo
mara kubwa. (uk. 20)*

Mwandishi kwa kutumia maneno haya ‘Ni kama dogo si dogo; kubwa si kubwa. ‘Mara nahisi ni dogo mara kubwa.’ Inaonyesha chanzo cha utata uliofanya ugonjwa uliomsibu Sele kutoeleweka na kumtinga hata Aisha na wahusika wengine tamthiliani. Mwandishi anachunguza utata huu uliopo kati ya Sele na wahusika wengine. Utata huu unatokana na ukweli kuwa Sele amepata mwamko mpya wa kisiasa ilhali wahusika wengine bado

wako katika giza. Hali hii ni chanzo cha Sele kukosa kueleweka na wahusika wengine tamthiliani.

Sele anamweleza Zainabu ambaye ni mamake, wasifu wa mganga. Anamweleza kuwa woga wake ulimfanya akose kumwamini pamoja na uchafu uliokoleza katika kibuyu chake cha dawa ya kienyeji:

Kama kweli nina ugonjwa, *kibuyu*
chake kitaniangamiza kabla ya
ugonjwa wenyewe. (uk. 81)

Kwelikinanzi inayodhihirisha inaonyesha kuwa hana matumaini kwa mganga huyu katika kuuponya ugonjwa wake. Mwandishi anaonyesha kuwa wakazi wa nchi za ulimwengu wa tatu hawana imani na viongozi wao ambao baada ya kuchukua hatamu za uongozi waliendeleza udhalimu uliohujumu haki zao zaidi ya alivyofanya mkoloni mkongwe.

Katika *Chamchela*, kuna mifano inayodhihirisha matumizi ya mtindo huu. Rukia na Kofa wakilijadili suala la ndoa ambalo limebadilishwa na kufuata mkondo wa mila za Uzungu anatoa maelezo yanayokinzana kuhusu maoni yake.

Siungi wala kupinga. (uk. 36)

Kijuujuu ni kwamba Kofa haungi wala kupinga mjadala. Kwa kutumia mkinzano huu mwandishi anamaanisha kuwa mhusika huyu hana msimamo katika mjadala huu. Hali hii ndiyo iliyogubika wahusika wengi tamthiliani kwa kuwa wameshindwa ama wakubali au wakatae mabadiliko haya yaliyozuka majanibuni mwao.

Sure akijaribu kuelezea hali ilivyo ngumu kutokana na mgongano wa tamaduni mbili, ukale na usasa, anatumia mtindo huu kuonyesha ugumu uliopo katika kuzikabili tamaduni hizi. Anasema:

(*Anamaka.*) Dunia hii nayo! Kweli
si tofauti na njia wala si tofauti na
msafiri. *Mbele hakutabiriki na nyuma*
hakurudiki. Njia... (uk. 7)

Kwelikinanzi ‘Mbele hakutabiriki na nyuma hakurudiki’ inarejelea hali ya mtanziko katika tamaduni hizi mbili ule wa kale na wa sasa kwani kuna ugumu wa kuamua ni kipi

cha kufuata. Sure anaeleza hivi akionyesha umuhimu uliopo wa kukabiliana na hali ilivyo kwani imejiri. Sure anajaribu kumhimiza Rosa kutohuzunikia sana kwa mabadiliko yaliyomfika kwani maisha huwa magumu na hivi humhitaji mtu kuyakabili na kuyatafutia suluhu mwafaka na wala si kulalama na kusononeka.

Rukia analaumu vijana kwa kufanya papara za kuukimbilia utamaduni mpya bila kukadiria maafa yake. Anaona changamoto moja na ambayo itaangamiza kizazi kichajo ikiwa vijana wa kiume watawaoa akina mama wazee ambao hawana uwezo wa kuzaa. Anasema:

...Jangwa hasa! *Tutakuwa tumekufa
kabla ya kuaga* ikiwa tutangoja kulishwa
vilivyoandaliwa... (uk. 38)

‘Tutakuwa tumekufa kabla ya kuaga’ ni kwelikinzani ambayo mwandishi ametumia kuonyesha kukosa matumaini ya kizazi hiki cha vijana ambao wanapapia mila za Kimagharibi na kudharau zao za Kiafrika. Rukia anamaanisha kuwa hakutakuwa na kuendelea kwa utamaduni wa Mwafrika ikiwa ndoa hazitaweza kuzaa watoto watakaokiendelea kizazi hiki na vivyo hivyo utamaduni.

4.2.6 Taswira

Ndung’u na Wafula (1993), wanaeleza kuwa taswira ni lugha ambayo huchora picha ya watu, vitu au mahali kwa kutumia ishara. Mdee na wenzake (2009) nao wanasema taswira ni picha ya mtu au kitu inayotokea katika fikra au akili za mtu anaposoma maelezo fulani. Madai hayo yanakaribiana na yale ya Njogu na Chimerah (1999) wanaosema kuwa, taswira hutumika kuleta picha au hali fulani akilini mwa msomaji. Msomaji anaweza kuona, kusikia, kuonja, kunusa, kupenda, au kuchukizwa, au kudharau kilichosawiriwa kutegemea nguvu za taswira zilizotumika.

Wamitila (2003) ametambua aina mbili kuu za taswira: taswira za kimaelezo na zile za kiishara. Taswira za kimaelezo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi na hazina maana fiche au ya ziada. Kwa upande mwingine, taswira za kiishara huunda picha iliyo na ujumbe uliofichika. Hivyo basi, ishara hizi huhitaji kufumbuliwa ili kupata maana iliyokusudiwa na mtunzi wa matini ya fasihi. Tutashughulikia taswira za ishara kwani ndizo humsaidia mwandishi katika kuufumba ujumbe wake. Pia tumefanya hivi kwa

kutegemea maelezo yetu ya maana ya tamathali kuwa tunajishughulisha na maana nasibishi na sio halisi. Chembilecho Wafula (1999) lugha ya kisanaa huwa nasibishi.

Mwandishi wa tamthilia teule ametumia taswira mbalimbali katika kujadili maudhui anuwai. Tukiangalia tamthilia ya *Mstahiki Meya*, taswira mbalimbali zinajitokeza katika kukuza maudhui ya mwandishi. Taswira iliyosukwa vizuri ili kuonyesha kiwango cha umaskini wa wanacheneo katika tamthilia hii inajitokeza Waridi anapomwelezea Siki hali ya kitoto kilicholetwa hospitalini kwa matibabu. Anaeleza hali yake hivi:

Daktari, si hivyo! Basi! Kitoto
chenyewe kiriba chaongoza. (uk. 5)

Binadamu aliyeugua maradhi ya utapia mlo hakui kama inavyostahili bali hudumaa. Hali hii humnyima nguvu na hivyo kumfanya kuwa mtegemezi kwa msaada unaotokana na wenzake. Mwandishi akitumia taswira hii anaonyesha ni kwa vipi mataifa machanga yalivyokosa kutatua matatizo yao ambayo yamekuwa tishio la uhai wao. Hali hii imeyafanya kutegemea misaada kutoka mataifa yaliyoendelea na hivyo kutumikishwa kikatili pamoja na kunyanganywa uhuru wao. Maana ya taswira hii inakuzwa zaidi na uzungumzi nafsia wa Meya akiwa ofisini mwake (uk. 25). Hata hivyo ugonjwa wa utapia mlo si wa kutibiwa hospitalini bali unahusu lishe bora kwa anayeugua. Hii inasisitiza ujumbe wa mwandishi kuwa matatizo ya mataifa ya Afrika hayatasuluhishwa na mataifa yaliyoendelea bali Waafrika wenyewe.

Katika mazungumzo baina ya Meya na Siki inabainika kuwa Meya hana ari ya kuwatendea wanacheneo haki. Siki anaona hali hii kuwa tishio la kumwangusha kutoka uongozi wa Cheneo. Anamwambia haya:

... Kama huku si kuwatusi wananchi
basi ndio kutembea nyuma ya punda
aliyeudhika. (uk. 14)

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Karne ya Ishirini na moja* (2011) punda ni mnyama anayetumiwa na binadamu kubeba mizigo mizito. Mnyama huyu hapendi kulalamika lakini anapokasirika huweza kusababisha madhara makubwa yasiyokadirika. Mwandishi anachora taswira inayopata uhai katika sitiari ya punda ili kuelezea hali ya ghadhabu

iliyowazidi wanyonge wanaotumikishwa kikatili na viongozi wenye tamaa bila kufaidi kwa vyovyote vile.

Uzungumzi nafsia wa Dida unatuchorea taswira ya uhusiano uliopo kati ya viongozi manyang'au (wabinafsi) walioshikilia nyadhifa mbalimbali za uongozi na wananchi wanyonge wanaotumikishwa kikatili katika uzalishaji bila kufaidi kwa vyovyote vile.

Dida anasema:

Duniani kuna watu na viatu
na Cheneo ina watu na viatu
... Paka na panya
Panya na paka! (uk. 64)

Taswira inayokuzwa katika sitiari hizi inasawiri hali halisi ya maisha na uhusiano wa viongozi na wanyonge katika jamii. Viatu huvaliwa na mtu ambaye ni kiumbe mwenye utu. Hivyo basi kiutu humtumikia mtu katika kumsetiri. Katika muktadha huu, viongozi na washauri wao ndio watu kwa kuwa wanatumikiwa na wanyonge ambao ni viatu katika kujinufaisha. Paka hutawala katika mazingira aliyomo na panya hawezi kuthubutu kukaribia mazingira haya kwani paka hataki kunyanganywa nguvu za kutawala. Sitiari hizi zinashadidia mahusiano haya katika jamii zenye viongozi ambao ni katili na huwadhulumu wanyonge kila wanapopigania haki zao. Meya anatumia mbinu hizi katika kutenga na kuwatawala wanacheneo.

Taswira nyingine inajengeka katika kuelezea juhudi za wanyonge katika kujiokoa wakati askari wanatibua mgomo wao wa kulalamikia madhila wanayotendewa na Meya. Askari wanatumia nguvu kuwatawanya wafanyikazi wanaolalamikia kunyimwa haki zao. Dida anajisemea hivi:

... Wakati wa mauti kama jana
Kumbe wazee huwashinda mbio
vijana ... (uk. 65)

Wazee kwa kawaida hawana nguvu walizonazo vijana. Taswira inayochorwa hapa ni ya kinaya ambapo mwandishi anataka kuonyesha jinsi ambavyo waandamanaji walivyokimbilia usalama wao baada ya hali kuwa mbaya. Hizi ndizo sifa za uongozi wa kiimla ambao hautaki kutatua majanga ya wakazi wake bali kuwahangaisha katika juhudi zao za kutetea haki.

Siki anamsihi Diwani III kufanya juhudi za kuzungumza na Meya ili apate kuyatatua matatizo yanayowakumba Wanacheneo. Anamwambia:

(*Kwa dhiti*). Lakini bwana himizeni hiyo
miamba kuangalia maslahi ya watu. (uk. 50)

Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2004) mwamba ni boriti ya katikati inayozuia mapaa ya. Boriti huishikilia nyumba na kuifanya kuwa imara na hivyo basi haiwezi kutingika. Taswira hii imejengwa katika sitiari ‘miamba’ ambayo inaipa uwezo wa kupitisha ujumbe kuwa viongozi walivyo na misimamo mikali ambayo haiwaruhusu kuwahurumia na kuwashughulikia wanyonge katika jamii. Taswira hii aliyotumia mwandishi inasisitiza ujumbe wa kutokata tamaa licha ya kuwa Meya na vibarakala wake kuwa wagumu kuchukua ushauri.

Katika tamthilia ya *Chamchela* hali ni sawa ambapo mtindo huu umetumiwa kupitia kwa mbinu mbalimbali katika kuelezea jinsi ujumbe wa mwandishi ulivyokuzwa. Mayaka akielezea tofauti kati ya uhusiano wake na wa Mbiki, anatumia tashbihi kujengea taswira ya tofauti hiyo.

... Kisa changu na chako vimetengana
kama ardhi na mbingu. (uk. 73)

Kwa kawaida ardhi na mbingu ni vitu viwili vilivyoachana kwa masafa na haviwezi kuhusiana. Taswira inayotokana na tashbihi hii inaonyesha tofauti kubwa kati ya mila za Kiafrika na zile za Kimagahribi. Mwandishi anaonyesha kuwa vijana waliamini katika mila za Kiafrika walifanyiwa maamuzi bila kupinga ilhali katika uzungu mila ziliwapa vijana uhuru wa kujiamulia na kutenda kwa hiari yao. Aidha, taswira hii inaonyesha mkinzano unaoshughulikiwa katika tamthilia nzima ambao ni mabadiliko.

Aidha, ugonjwa wa Rosa unakosa tiba hospitalini kama ilivyo katika *Mstahiki Meya* ambapo Dadavuo Kaole anakosa matibabu ya kumnusuru katika hali yake. Ugonjwa wa Rosa unatokana na kutokubaliana na mabadiliko yanayojiri kwa kasi katika jamii. Ugonjwa huu unahitaji tiba inayotokana na nafsi ya Rosa kukubali haya mabadiliko. Hata hivyo ugonjwa huu unatupa taswira ya jinsi mwandishi anavyoshughulikia usuluhishaji na utatuzi wa majanga barani Afrika. Utatuzi unaofanywa na washika dau katika majanga ya nchi za ulimwengu wa tatu si wa kihalisia bali ni kubabaisha tu wakazi wake.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, mwandishi ametuchorea taswira nzuri zaidi inayoonyesha uhusiano wa mabepari na wanyonge katika jamii. Sele anamweleza Aisha:

Yapo mengi mengine. Ni kweli papa
ana kiburi kikubwa maana yu mfalme
wa bahari. Mwili wake una uwezo wa
kuzuia mawimbi ya bahari navyo
vidagaa hujificha nyuma yake kujisitiri.
Vidagaa vinajua ni hatari lakini afadhali
hatari ya papa kuvila badala ya kuangami-
zwa na mawimbi makali. Wajua ni kama
kuku ambaye anakiona kisu cha mchinjaji
afadhali kuliko maisha vichakani... (uk. 37)

Taswira inayokuzwa katika usemi wa Sele inaonyesha ni kwa nini matabaka yatakuwepo katika jamii na kuendelea kudumu daima na milele. Sitiari ya papa inarejelea viongozi walioshikilia na kuhodhi nyenzo kuu za uzalishaji na ugavi mali katika jamii na kuwatumikisha vidagaa ambao ni wanyonge na walio wengi kwa ukatili mkubwa. Umiliki huu huwapa uwezo wa kuamua hali za kiuchumi katika mataifa yao. Ukosefu wa kuamua huu huwalazimu wanyonge kuwategemea ili kuishi kwa kuwa hawana uwezo. Hili ndilo chimbuko la matabaka mawili makuu katika jamii ya walalaheri na walala hoi. Papa huwa wachache lakini wakubwa kwa kimo katika bahari ikilinganishwa na vidagaa ambao ni wengi na wadogo kwa kimo. Hii ni sawa na jamii ambapo tabaka la matajiri ni la wachache na la makabwela ambao ni maskini ni wengi. Taswira hii inamulika mfumo wa kibepari kama anavyoelezea Thomson (2000) kuwa jamii imegawika katika makundi mawili katika misingi ya kitabaka: mabwanyenye na makabwela. Mabwanyenye ndio viongozi na humiliki nyenzo kuu za uzalishaji mali na huwatumikisha makabwela ili kuendeleza utajiri wao.

Ugonjwa wa Sele unaendelea kukuza juhudi za mwandishi za kumulika jinsi mataifa ya Afrika yanavyopigana vita na ukandamizaji wa kijamii na kiuchumi. Taswira ya ugonjwa uliomkumba Sele ambao unashindwa kupata tiba licha ya kuwa na madaktari watatu, ni dhahirisho la kutosha kuwa mwandishi hashughulikii suluhu la matatizo barani Afrika tu bali pia chanzo. Taswira ya ukosefu wa dawa mwafaka katika kutibu magonjwa tunayoyashuhudia katika tamthilia zote tatu ni ishara kuwa mwandishi anataka kuonyesha kuwa kadhia ngumu anazozipitia Mwafrika hazina suluhu popote pale ila tu zitapata

suluhu halisi baada ya kujikomboa kimawazo. Ukombozi huu utamwezesha kukabiliana na matatizo yake na hivyo kuleta usawa uliojikita kwenye misingi ya utu.

Taswira alizozitumia mwandishi zinamfikirisha na kumtafakarisha msomaji katika kupata maudhui anayoyakuza mwandishi. Tumebaini kuwa taswira huweza kujengwa kutokana na tamathali zingine.

4.2.7 Takriri

Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja (2011) inafafanua takriri kama mbinu ambayo neno hurudiwarudiwa ili kupata umbo moja. Masinde (1992) na Kuhenga (1977) wana maoni sawa wanapoeleza takriri kuwa ni mtindo wa uneni wa ufasaha ambao msanii hutumia kwa maksudi au nia mahususi, hurudia neno, sauti au maneno yale yale ili kutilia mkazo au msisitizo zaidi juu ya jambo asemalo. Hii ina maana kuwa takriri licha ya kurudia neno huwa na dhima ya kuisisitiza ujumbe wa mwandishi. Mbinu ya takriri mara nyingi hutumiwa na waandishi kwa nia ya kumvuta msomaji wa kazi zao ili atambue umuhimu uliopo katika ujumbe unaokaririwa. Wamitila (2008) anasema mbinu hii pia huitwa ‘takriri’ kwa maana ya kurudia maneno yale tena na tena.

Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*, mtindo huu umejitokeza katika maongezi ya wahusika mbalimbali. Amri anamtahadharisha Sele jinsi uhuru ambao anaung’ang’ania ulivyo muhali kupatikana. Amri anamwelezea kwamba hamna uhuru halisi katika dunia hii, anasema uhuru ni utumwa.

... Alosema kuna *uhuru* nani? Unajidanganya.
Hata katika *uhuru* wako huo mna utumwa.
Kiungo kimojawapo cha *uhuru* ni utumwa. (uk. 66)

Amri anakariri neno ‘uhuru’ kwa Sele akitaka kumweleza kuwa hamna uhuru kamili katika dunia hii. Amri anataka kuisisitiza kuwa kuna ugumu wa kuelewa na kuzitenga dhana ya uhuru na utumwa kwani zina ukuruba.

Mfano mwingine ambao unaonyesha matumizi ya mtindo huu ni kutoka tamthilia ya *Chamchela* ambapo Bisase, mamake Sera analalamikia shughuli zinazotekelezwa na Sera na hivyo kumzuia kuwajibikia malezi ya mwanawe Lema. Bisase analalamikia hali hii:

Mara nina miadi, *mara* nenda
shughuli za kibiashara, *mara*...
(*Kaudhika*) si utachosha na hizo
haraka zako zisizo tuo? (uk. 18)

Mwandishi anasisitiza vile shughuli za vijana za mara kwa mara huwazuia kuwajibikia majukumu yao ya kimsingi. Shughuli hizi ndizo chanzo cha Sera kusahau wajibu wake kama mzazi kwa Lema. Mwandishi anaendelea kufafanua athari za utamaduni wa kigeni uliowagubika vijana kiasi cha kuzembea katika majukumu yao ya kijamii.

Sure amehofia mawimbi ya utamaduni wa kimagharibi uliogubika vijana na kuwateka nyara kimawazo. Anatambua athari za utamaduni huu akiwa amechelewa sana. Katika kuisisitiza haja ya wao kushauriana na Mayaka anamwambia Atisa:

... *lazima* Atisa... *lazima*
tushauriane naye! (uk. 1)

Sure anataka kuonyesha Atisa umuhimu na dharura ya mkinzano uliopo. Atisa anapotaka kupingana naye, Sure anaendelea kuisisitiza ujumbe wake kwa maneno haya:

Hamna cha lakini mwanangu...
Ulimwengu! ... Ulimwengu
mwanangu ... (uk. 1)

Uradidi wa Sure unaendelea kuisisitiza umuhimu wa Atisa katika kusuluhisha mgogoro wa ndoa ya Mayaka na Bisase ambao umesababisha mahangaiko kwa jamii yake nzima.

Mbiki anamrai mamake ambaye amelemewa na ugonjwa kutembea kwa maneno ‘tena’ ili kumtia moyo wa kupiga hatua.

Taratibu mama. Haya twende
... *tena...tena*. (uk. 8)

Mtindo huu wa takriri unasaidia katika kufafanua hali ya Rosa ambaye amaelemewa na ugonjwa ambao umesababishwa na hatua aliyoichukua Mayaka kufadhiliwa na Bisase katika ndoa. Kwa matamshi haya, Mbiki anataka kumhimiza mamake ajaribu kutembea japo kalemewa.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mbinu hii imetumika kuisisitiza ujumbe wa mwandishi kwa njia mbalimbali. Diwani I na II wanasaidiana kupanga njama za kuwafumba macho

wanacheneo ili wajihisi kuwa serikali yao inawajali. Mbinu inayopangwa kutumiwa na madiwani hawa ambao ni vibarakala wa Meya ni kuandaa tamasha za michezo ili vijana watuzwe kwa kuonyesha uzalendo. Diwani III analiona jambo hili kama kudunisha haki za wanacheneo, anasema:

Uzalendo... uzalendo hauji kwa
watu kuimbiwa nyimbo bali kwa
kujibu vilio vyao. (uk. 20)

Matamshi haya yanaonyesha kuwa vibarakala wa Meya hawaelewi maana ya uzalendo. Mwandishi anasisitiza kuwa ili misingi ya kiutu ipatikane katika jamii ni sharti viongozi washughulikie mahitaji ya wananchi wao.

Baada ya Bili kumshauri Meya amruhusu mwanakandarasi kwenda kortini kumshtaki ili wafaidi wote, Meya anaonekana kuwa na wasiwasi hasa kuhusu kuharibiwa jina lake kwa kuwa anahofia kuwa likiharibika huenda akakosa kuchaguliwa tena. Bili ana ushauri huu:

Jina si kitu. Tumbo ndilo muhimu.
Tumbo lako na jamaa *zako*. Watoto
wako. Wajukuu *wako*. (uk. 29)

Kupitia kwa ushauri wa Bili ambaye ni kibarakala wa Meya, tunajengewa maudhui ya ubinafsi ambayo yamegubika viongozi kiasi cha kutoona umuhimu wa maslahi ya umma uliowachagua. Hiki ni kizuizi katika kufanikisha maendeleo yanayotarajiwa katika nchi za ulimwengu wa tatu.

Meza baada ya kupitia mafaili ofisini mwake anafurahia hatua anayopanga kuichukua ya kumfurusha mwanakandarasi anayelihuliudumia baraza la mji wa Cheneo kwa manufaa ya kipekee. Katika kuonyesha kuridhishwa na hatua hii anajisemea hivi:

Safi! ... Safi! ... (uk. 25)

Matamshi haya yanaonyesha kuwa Meza ameridhishwa na hatua anayodhamiria kuichukua. Aidha, hii ni mojawapo wa njia ambazo mwandishi ametumia kuonyesha kuwa Meza analiendesha Baraza la Mji kwa njia zisizo za haki na usawa. Anaendeleza maudhui ya ubinafsi ambapo viongozi hujali maslahi yao pekee pasina kuwatendea wananchi waliowachagua haki.

Siki anamrai Diwani III kumkumbusha Meya kama mtoto ili aweze kujali na kutilia maanani haja ya kutatua majanga yanayowasibu wanacheneo. Siki anaelewa fika kuwa Meya hapendi kuambiwa ukweli, hata hivyo, anamwomba Diwani III kusema naye mara nyingi kwa kutumaini kuwa huenda akasalimu amri na kubadili nia. Anamwambia:

(*Anamrai.*) Basi kama mtoto
mkumbushe *tena* na *tena* mpaka
apate mwanga wa kile unachokisema. (uk. 47)

Diwani III anamwahidi Siki kufanya juhudi za kumweleza Meya ili aweze kushughulikia matatizo ya wanacheneo. Matamshi ya Siki yanadhihirisha wazi mapuuzwa kwa mahitaji ya wananchi wa kawaida yanayosababishwa na ubinafsi na tamaa ya kujitakia makuu kwa upande wa viongozi. Anasema:

Tunahimiza sana. Bado *hatujakata*
tamaa kama nilivyoisha kukutajia.
Mimi binafsi nitasema naye Meya
tena na *tena* hadi atakapoona
umuhimu wa ninayomwambia. (uk. 50)

Maneno 'tena na tena' yanaonyesha vile ambavyo atakavyomkumbusha Meya kuhusu hali mbaya ya maisha ya Wanacheneo hadi aone umuhimu wa kuishughulikia. Ni hakikisho kutoka kwa Diwani kwa Siki kuwa atatekeleza jukumu la kumkumbusha Meya ukweli huo kwani wanacheneo bado wangali na tumaini kwa huenda akabadilika na kuwatendea haki na ndio maana anasema: 'hatujakata tamaa'. Mtindo huu unatumika katika kutilia mkazo na kusisitiza umuhimu wa ujumbe unaokuzwa na mwandishi. Mtindo huu umetumiwa mara nyingi katika kutilia mkazo hali inayoelezewa na wahusika katika tamthilia teule.

4.2.8 Nahau

Kwa mujibu wa TUKI (2004) nahau ni fungu la maneno ambayo yakipangwa pamoja huleta maana isiyo ya kawaida ya kuonekana wazi. Mdee n.w. (2009) nao wanasema kuwa nahau ni fungu la maneno lenye maana maalumu ambayo haitokani na jumla ya maana ya maneno yanayojenga fungu hilo. Hii inamaanisha kuwa maana inayorejelewa na fungu fulani si wazi bali imefichama katika kauli hizo na humhitaji msomaji

kuifichua. Mtindo huu umejitokeza katika tamthilia zote. Katika tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* (uk.1)

Sele ameshika tama.

Mwandishi anatumia nahau, ‘kushika tama’ ambayo inamaanisha kuhuzunika. Tamathali hii inatufungulia onyesho la kwanza la tamthilia hii na kutupa maudhui ya majonzi na tabu anazokumbana nazo Sele ambaye ni mhusika mkuu. Nahau hii ni ishara ya magumu wanayokumbana nayo wahusika wote katika kutambua chanzo cha ugonjwa wa Sele katika tamthilia nzima.

Sele anaeleza kutoridhika moyoni licha ya kujitahidi kwake. Anamweleza Aisha:

... Ni kama *unanikodolea macho*.
Ni kama unanisaili kimyakimya. (uk. 9)

Kwa mujibu wa TUKI (2011) nahau kodoa macho ina maana ya kutazama kwa macho yaliyokazwa; tumbua au toa macho. Sele kwa nahau hii anaashiria ni kuzinduka kwake kunamzuia kutenda mambo kwa kuiga tu kwani unamlazimu kujisaili katika maamuzi yake.

Zainabu akilalamikia hatua zinazochukuliwa na washika dau katika kuwaachisha kazi, anasema:

Inavunja moyo. Wao ndio watu
na sisi sanamu tu. (uk. 24)

Kulingana na TUKI (2011) nahau ‘kuvunjika moyo’ ina maana ya kukosa nguvu ya kutenda jambo; ni kukata tamaa. Nahau hii inaonyesha jinsi wakazi wa mataifa ya mataifa machanga hukosa matumaini kwa kuwa wanadhalilishwa. Hawahusishwi kwenye maamuzi kwa kuwa hawathaminiwi kwani wao ‘si watu bali sanamu’.

Bi. Rahma anamweleza Sele kama mtu asiye na matumaini. Anamwambia hivi:

...*umekata tamaa* kwa kufutwa kazi... (uk. 28)

Nahau ‘umekata tamaa’ imetumika kwa maana ya kukosesha matumaini au hamu ya kuishi.

Tamthila ya *Chamchela* imedhihirisha matumizi ya nahau kwa mazungumzo ya wahusika wake kwa sababu tofautitofauti. Kwa mfano, Sure anasema:

Basi sisi tumekutana jana na *kukata*
kauli kuwa pana haja kumwita aje... (uk. 1)

Nahau ya ‘kukata kauli’ imetumika ili kuleta maana ya kuamua. Licha ya dhima hii ya kuamua, tamathali hii inaleta uzito wa kutilia mkazo umuhimu uliopo kwa Atisa kuwasiliana na Mayaka ambaye ni nduguye na kumjuvya kuhusu uamuzi uliofanywa na wazee wa kukutana naye. Kupitia kwa usemi wa Sure tunafahamu kuwa suluhu la mabadiliko yanayokusudiwa ni muhali kupatikana. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wazee hataki kuwasikiliza vijana bali wanataka wawamulie tu.

Mbinu hii inajitokeza tena Sure anapomweleza Mbiki kuhusu chanzo cha kuugua kwa Rosa. Nahau ya ‘kulitia mabegani’ ambayo inamaanisha kuwa Rosa amelichukua tatizo la Mayaka la kumwoa Bisase bila kulitolea tahadhari kana kwamba limetokea kwake pekee. Sure anasema hivi:

(*Kashangaa.*) Labda ni mgongano mkubwa
wa mawazo uliomzonga...Jambo kama hili
mtu anaweza *kulitolea tahadhari* lakini siyo
kulitia mabegani. (uk. 9)

Nahau hii inaonyesha hali mbaya iliyompata Rosa kutokana na uamuzi wa Mayaka wa kumwoa Bisase. Sure anasikitikia hali hii kwa kuhofia madhara ya kuliwazia jambo hili sana bila kutahadhari. Mwandishi anaonyesha kuwa madhara ya wazee ni ya kujitakia kwani wameshikilia mkiki misimamo yao na hawako tayari kuona mambo kwa mtazamo tofauti. Hili ndilo angamizo lao japo wanawanyoshea lawama vijana.

Atisa amekata tamaa katika kumshauri Mayaka kubadilisha msimamo wake. Sure akimsisitizia umuhimu wa kuwa na matumaini, anasema:

...Ukoo wetu si wa *kukata tama*... (uk. 4)

Alitumia nahau hii ili kumtia moyo Atisa ambaye alionekana kukosa matumaini ya kumrai Mayaka ili akubali kubadilisha nia ya kumwoa Bisase.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mtindo huu unajitokeza kwa wingi. Siki analalamikia maisha magumu na ya umaskini wanayoishi wakazi wa Cheneo. Anamwelezea hali ya ugumu huu kwa kutumia nahau hii:

Hata sembe na sukuma *vinawatoa jasho*
kuvitia mezani... (uk. 11)

Nahau ‘vinawatoa jasho’ ni tamathali inayojumlisha uhaishaji ili kuleta picha ya ugumu uliopo kwa wanacheneo kujipatia riziki zao. Siki anamweleza Meya kuhusu hali ya wanacheneo ya umaskini uliokithiri chini ya uongozi usiowajali. Tamathali hii inaashiria hali ngumu wanayoipatia wanacheneo kwani hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi kama chakula. Inadhihirisha maudhui ya umaskini. Licha ya maelezo haya kuwa ishara ya hali mbaya iliyopo kwa sababu ya uongozi mbaya, yanaonyesha uzalendo wa Siki kama mhusika anayewajali wanacheneo.

Siki anamkabili Meya kwa akitumia nahau kwa njia ya balagha ili kumwonyesha kuwa njama yake ya kuwambia watu nyimbo huenda isimfae katika uongozi wake. Hii ndiyo sababu yake kumwuliza:

Lakini ndugu, unadhani nyimbo
zitawashibisha na *kukata kiu* ya
uhitaji wao? (uk. 13)

‘Kukata kiu’ ni tamathali ambayo inamaanisha kumaliza hamu. Nahau hii imetumiwa na Siki ili kumtafakarisha Meya kuhusu mahitaji ya wanacheneo ambayo hayajatimizwa. Mwandishi anaonyesha kuwa chanzo cha kukosa kwa maendeleo barani Afrika ni njama za uongo zinazotokana na ubinafsi wa viongozi. Baada ya mkutano kati ya Meya na Siki, Meya anapata kiwewe kutokana na maelezo ya Siki. Hofu ya kung’atuliwa uongozini inamfanya kuwaita washauri wake ambao pia ni vibarakala ili wazuie michafuko ambayo yaweza kutokea katika Cheneo. Diwani II wa pili anaelezea hasira za Meya akitumia nahau. Anasema:

Mzee si mtu wa kutishwa ovyo ovyo
lakini ukiona anatuita kukutana naye
kama hivi, basi *yamemfika shingoni*. (uk. 16)

Nahau ‘yamemfika shingoni’ imetumika kuonyesha ghadhabu ya Meya inavyomsikitisha. Hali hii imemtia hofu na anataka wa kumweleza. Hii ina maana kuwa viongozi wa nchi za ulimwengu wa tatu hughadhabishwa sana hasa wanapokumbana na ukweli unaouma kuhusu uongozi wao wa kiimla.

Naye Diwani III anamweleza kwa uwazi Meya sababu itakayomzuia kufaulu katika njama yake ya kutoa ahadi za uongo. Anatumia nahau ifuatayo:

...Watu sasa wanafahamu *mbivu na mbichi*. Utawaambia lipi geni la kuwatuliza? (uk. 16)

Nahau ‘mbivu na mbichi’ imetumika kueleza kuwa sasa mambo yote katika Baraza ni wazi na kwamba wanacheneo wanafahamu ukweli wa kila jambo na hivyo hawawezi kudanganywa kwa lolote. Hii inaonyesha uongozi wa kidikteta wa Meya na vibarakala wake unajulikana na hasa katika njama zake.

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu ni kweli kwamba nahau ni mojawapo ya sifa za lugha aliyoitumia mwandishi kwa wingi katika kupitishia maudhui yake. Mtindo huu humsaidia mwandishi kufafanua hali halisi ya tendo kwa kutumia maneno machache. Hali hii humsaidia msomaji si tu kwa kuupata mvuto wa kipekee bali pia kufikiri na kuhusishwa katika kupata ujumbe. Aidha Arege ametumia nahau ya ‘kukata tamaa’ sana ili kumshirikisha msomaji kuwa licha ya changamoto nyingi katika ukombozi hamna haja ya kupoteza tumaini.

4.3 Hitimisho

Katika sura hii tumechunguza tamathali za usemi alizotumia Arege kwa wingi katika tamthilia teule. Imedhihirika wazi kuwa Arege ametumia tamathali za usemi mbalimbali katika kuwasilisha maudhui yenye mashiko katika jamii ya kisasa. Tamathali za usemi zimesaidia kuufinyanga ujumbe katika tamthilia teule na kuueleza kwa ufaafu bila kuhujumu mahusiano ya watu katika matabaka ya watawala na watawaliwa. Baada ya kupitia tamathali za usemi mbalimbali ambazo alitumia mwandishi huyu tumebaini kuwa, kadri mwandishi anavyokuwa na uzoefu wa kuandika katika fasihi ndivyo kunga za kupitisha ujumbe wake zinavyoendelea kukua na kuimarika na hivyo kuwasilisha maudhui mbalimbali yanayoiathiri jamii ya leo akilinganisha na ya juzi. Kupitia kwa

utafiti huu imebainika kuwa mbinu alizotumia Arege zimesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuwasilisha ujumbe wa tamthilia teule. Hili ni dhihirisho kuwa tamathali ndizo huelekeza mkondo wa ujumbe katika kueleweka namna unavyoeleweka. Aidha, mbinu alizotumia Arege zimedhihirisha ufundi wake katika fasihi na hasa katika kipera cha tamthilia.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia muhtasari wa sura zote za utafiti huu. Sura hii imejadili matokeo ya utafiti huu, mahitimisho na mapendekezo kwa tafiti za baadaye.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni ya kubaini mtindo katika tamthilia teule za mwandishi Arege. Kwa minajili ya kufikia lengo kuu, mtafiti aliugawa utafiti katika sura tano ambapo alishughulikia vipengele vitatu vya kimtindo katika tamthilia tatu zilizoteuliwa za Arege. Viwango hivi ni: uwasilishaji wa mawazo, sintaksia na semantiki.

Sura ya kwanza ya utafiti ilishughulikia mambo ya kimsingi ya utafiti ambapo tuliangalia usuli wa mada, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, mipaka na upeo wa utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyaoandikwa kuhusu mada na mwishowe mbinu za utafiti. Sura hii ilikuwa na umuhimu katika utafiti mzima kwa kuwa ndiyo iliuwekea utafiti msingi kwa kufafanua na kuweka wazi lengo letu.

Katika sura ya pili, tulichunguza kazi mbalimbali alizoziandika Arege katika fasihi ambapo tulibaini kuwa ameandika katika vipera vyote vya fasihi- iwe simulizi au andishi. Tulitoa muhtasari wa tamthilia teule hasa kwa kuangazia mbinu ya kimsingi ilyotumiwa katika kuwasilisha maudhui. Tulibaini kuwa japo tamthilia hizi ni tofauti kwa mada zina misingi yake katika uhalisia wa ukombozi kwa wakazi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu. Aidha tulibaini kuwa Arege ni mwandishi aliyekoleza maudhui yake katika mbinu ya kinaya na kejeli.

Katika sura ya tatu, utafiti ulishughulikia mbinu za usimulizi. Tulifanya hivi kwa kutaka kubaini mitindo mbalimbali aliyoitumia katika kuiunda kazi yake kisanaa kiasi cha kuifanya ivute msomaji ili apate ujumbe wake kama ulivyokusudiwa na mwandishi. Hapa tuliangalia mbinu mbalimbali za usimulizi alizotumia mwandishi ili kuiboresha kazi yake. Mojawapo wa mbinu tulizochunguza ni sentensi na virai katika mkabala wa kifasihi. Kutokana na maelezo ya wataalamu ilibainika mbinu za usimulizi ni pamoja na mdokezo, maswali ya balagha, usambamba, kuchanganya ndimi n.k. Ilibainika kuwa mbinu za usimulizi ni muhimu kwa kuwa zina uwezo wa kubadilisha maana katika kazi

ya fasihi na hata kuzua utata. Aidha, utafiti umebainisha kuwa mbinu za usimulizi ndizo husaidia kudumisha ujumbe wa mwandishi na kuleta taathira ya kibunifu licha ya kumtambulisha.

Sura ya nne imeshughulikia tamathali za usemi zilizotumika katika tamthilia teule za Arege. Hizi ni mbinu za kimtindo alizozitumia mwandishi huyu katika kuwasilisha ujumbe wake. Utafiti ulichunguza tamathali mbalimbali zilizojitokeza katika tamthilia teule. Tamathali zilizochunguzwa ni pamoja na: tashbihi, tashhisi, methali, tabaini, kwelinzani, taswira, takriri na nahau. Mbinu hizi zilitumika kuelezea ujumbe wa mwandishi kwa njia ya fumbo kwa nia ya kuvuta makini ya msomaji na kumtafakarisha kwa kina ili kuufumbua. Sura hii imetuwezesha kubaini kuwa kazi ya fasihi hueleweka vyema pale tu tunapochunguza tamathali za usemi zilizozitumika katika kuwasilisha ujumbe kwa msomaji (msikilizaji). Utafiti umebaini kuwa tamathali za usemi zilizotumika na mwandishi huyu zina ukuruba mkubwa katika tamthilia zote ingawa zingine huonekana kujitokeza kwa wingi zaidi na kwa miundo tofauti katika tamthilia moja kuliko nyingine. Hali hii ilichangiwa na jinsi mwandishi alivyotaka kujenga maudhui mbalimbali kwenye tamthilia husika na vile vile kuyatilia mkazo. Pia ilibainika kuwa tamathali hizi huingiliana katika kuibua maudhui mbalimbali. Mwingiliano huu ndio hukoleza ujumbe unaoelezwa na mwandishi.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga katika kuhakiki na kubainisha mtindo katika tamthilia za Arege. Katika kufikia lengo letu kuu tulitathmini tamthilia tatu za mwandishi Arege. Tulikuwa na malengo matatu yaliyotwezesha kufikia lengo letu kuu. Ili kufikia lengo letu, tulichambua tamthilia tatu za Arege (ambazo ni jumla ya kazi katika kipera hiki) zenye vipengele mbalimbali vya kimtindo. Utafiti ulidhamiria kubainisha mitindo anuwai aliyoitumia Arege katika kuwasilisha jumbe za tamthilia zilizoteuliwa kwa nia ya kuonyesha kutolea kauli ya jumla kuhusu uandishi wake na mtindo wake.

Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha mitindo iliyotumika kuwasilisha ujumbe katika tamthilia teule. Lengo hili lilifikwa katika sura zote ambapo mitindo mbalimbali ilijadiliwa kwa kina kwa kuangazia vigezo vya uainishaji.

Lengo la pili ambalo lilihusu kutathmini athari ya mitindo hiyo katika kuwasilisha ujumbe lilifikiwa katika sura ya pili na tatu. Lengo hili lilifikiwa katika sura pili na ya tatu ambapo tulishughulikia mtindo wa uwasilishaji wa maudhui pamoja na mbinu za usimulizi katika tamthilia zilizoteuliwa. Utafiti ulijihusisha na kuangalia maudhui aliyoyashughulikia Arege katika tamthilia zake tatu ili tuweze kufafanua athari ya mitindo aliyotumia katika kuyawasilisha. Katika uchanganuzi wetu, tulibaini kuwa mwandishi huyu ili kupitisha ujumbe wake, ametumia mitindo mbalimbali. Katika sura hii, tulibaini kuwa mwandishi ametumia mbinu za usimulizi mbalimbali kutegemea ujumbe aliodyhamiria kukuza huku mbinu za mdokezo na balagha zikitamalaki katika tamthilia zilizoteuliwa. Imebainika kwamba mbinu za usimulizi ni kipengele mojawapo ambacho huainisha mtindo wa mwandishi.

Aidha, lengo la pili lilijitokeza katika sura ya nne pia. Lengo la pili lilitawala na kutamba katika sura zote za tasnifu kwa sababu ni vigumu kutenga mtindo na ujumbe, yaani kinachosemwa na namna kinavyosemwa (Leech na Short, 2007). Vitu hivi vinaonekana kama pande mbili za sarafu moja kwa kuwa vinajengana na kukamilishana katika dhima zao.

Lengo la tatu lilikuwa kuchunguza tamathali za usemi katika tamthilia teule na lilifikiwa katika sura ya nne. Ilibaimika wazi kuwa mwandishi Arege ametumia tamathali mbalimbali za usemi katika kuwasilisha ujumbe wake kwa ufaafu. Mbinu hizi ni pamoja na tashbihi, tashhisi, methali na nyinginezo. Matumizi ya tamathali hizi yalidhihirisha kuwa licha ya mwandishi huyu kuwa chipukizi ana uwezo mkubwa wa kushughulikia maudhui yanayoyakabili mataifa machanga barani Afrika kwa mitindo ya kuvutia. Aidha, utafiti huu umedhihirisha kuwa kadri mwandishi anavyoendelea kutunga ndivyo anavyoendelea kuonyesha ukomavu wa kunga mbalimbali za lugha ambazo huufumbata ujumbe wake zaidi. Katika tamthilia teule za Arege, tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* imefumba ujumbe zaidi kutokana na kunga alizotumia Arege tofauti na ilivyo katika *Chamchela* na *Mstahiki meya* alizoandika hapo awali.

Kinachobainika wazi ni kuwa japo tulikuwa na malengo matatu, utafiti ulikuwa na nia moja tu. Nia yetu ilikuwa kuonyesha kuwa mtindo ni taji ya maudhui. Hii ndio sababu ya malengo haya ya utafiti huu kuingiliana na kuumana katika sura husika.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo kama ilivyofafanuliwa na Leech (1969). Mihimili ya nadharia hii iliyoorodheshwa katika sura ya kwanza iliupa utafiti huu msingi wa kufikia lengo lake. Kazi ya fasihi hujengwa na vipengele mbalimbali mathalani msuko wa vitushi, dhamira, maudhui na wahusika. Hata hivyo, vipengele hivyo haviwezi kuwasilishwa bila lugha. Mtindo basi ni namna ya kujieleza kwa kutumia lugha (Ngara, 1981; 1985). Hii ina maana kuwa msomaji wa kazi ya fasihi hawezi kupuuza umuhimu uliopo katika umbuji wa lugha ya kazi ya kifasihi. Kwa hivyo, ikiwa msomaji anataka kuuelewa na kupokea ujumbe katika kazi za fasihi basi itamlazimu kuvichunguza vipengele vya mtindo kwa makini zaidi.

Katika sura hii, nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo ilituwezesha kuonyesha kuwa lugha ndicho chombo cha kipekee anachoweza kutumia mwandishi katika kuelezea ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Utafiti huu umedhihirisha haya katika sura ya pili, tatu na nne mtawalia ambapo tumechanganua tamathali zilizotumika katika tamthilia tatu zilizoteuliwa. Kupitia kwa uchanganuzi wa tamathali za usemi katika tamthilia teule tumebaini kuwa mbinu mbalimbali za lugha itumiwayo katika uandishi huwezesha uwasilishaji wa maudhui kwa njia mwafaka inayoleta mvuto wa kipekee. Aidha, imejitokeza wazi kutokana na uchanganuzi huu kuwa mitindo mbalimbali ya lugha iliyotumika katika matini za kifasihi huathiri namna ujumbe wake unavyopokelewa na kueleweka. Hii pia huathiri namna msomaji wa matini yake anavyoelewa na kupokea ujumbe wenyewe. Utafiti wetu umedhihirisha kwa uwazi kuwa mtindo ni uti wa mgongo katika kufafanua ujumbe wa mwandishi. Mtindo huonyesha ni kwa jinsi sifa za lugha iliyotumika katika kujenga ujumbe pamoja na kuuwasilisha huleta mvuto katika usomaji ili kuupokea ujumbe huo kama ulivyokusudiwa na mwandishi. Kupitia kwa utafiti huu, tumefaulu kuonyesha kuwa njia inayomsaidia mwandishi kupitisha ujumbe ndiyo maarufu zaidi. Utafiti huu ni muhimu kwani umehakiki mtindo katika utanzu huu wa tamthilia na hivyo kutoa mwanga katika kuzielewa tamthilia za Arege kwa kuwa kazi yoyote ya fasihi huandikwa ili isomwe na kupokeza ujumbe kama ulivyokusudiwa na mwandishi. Pia utafiti huu umechangia katika kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwani utarejelewa na watafiti wa baadaye. Muhimu zaidi katika utafiti huu ni kwamba, lugha kama kipengele cha kufafanua mtindo ina mawanda mapana ya kutumika na hivyo

huweza kuzua maana mbalimbali. Ni jukumu la mwandishi kuifinyanga lugha kwa ubunifu fulani ili iweze kuwasilisha ujumbe kama alivyokusudia.

Aidha, nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo ilirahisisha shughuli ya kuzilinganisha tamthilia teule hivi kwamba tulibaini kwamba mtindo wa Arege unaendelea kubadilika kadri anavyotunga na hivyo kuonyesha ukwasi katika matumizi ya kunga mbalimbali za utunzi. Aidha, Utafiti huu umebaini kuwa Arege ni mwandishi anayependelea kutumia mtindo wa kinaya na kejeli katika kueleza ujumbe wake.

5.4 Mahitimisho

Utafiti huu umehakiki mtindo katika tamthilia tatu za Timothy Arege ambazo ni: *Kijiba cha Moyo* (2009), *Mstahiki Meya* (2009) na *Chamchela* (2007). Utafiti huu umebaini kuwa mtindo unaotumika katika kazi fasihi una athari kubwa sana katika uamuzi wa njia ujumbe utakavyopokelewa. Hii ina maana kuwa ujumbe huwezi kueleweka bila kuwepo kwa njia maalum ya kuulezea kwa hadhira husika. Kwa hivyo mtindo ni nguzo kuu katika kazi yoyote ya kisanaa kwani hufanya kazi ya kuifafanua kazi hiyo ili ieleweke ipasavyo. Aidha, mtindo ni taji ya maudhui katika kazi ya fasihi.

5.5 Mapendekezo

Dhana ya mtindo ni pana na tena tata. Mtindo huweza kufafanuliwa kwa njia tofauti kutegemea mtazamo wa mhakiki. Hata hivyo, utafiti huu umeshughulikia baadhi ya kategoria ambazo ni: uwasilishaji wa mawazo, sarufi na tamathali. Utafiti zaidi unaweza kushughulikia mambo yafuatayo:

- i) Kategoria ya uteuzi wa msamiati ambapo aina za maneno hushughulikiwa haikushughulikiwa katika utafiti huu. Utafiti unahitajika katika kategoria hii ili kuweka wazi mtindo katika tamthilia zilizoteuliwa.
- ii) Utafiti wa kina unahitajika ili kufafanua maudhui na uhalisia wake katika tamthilia zilizoteuliwa. Hii ni kwa sababu utafiti huu uligusia maudhui tu kwa lengo la kufafanua athari ya mtindo katika kuyakuza.

iii) Pia mkabala wa kiisimu unaweza kutumiwa kwa utafiti zaidi kwenye tamthilia zilizoteuliwa kwa kuwa utafiti huu umeegemea mkabala wa kifasihi katika kufafanua mtindo.

MAREJELEO

Arege, T. M. (2007). *Chamchela*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Arege, T. M. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

- Arege, T. M. (2009b). *Kijiba cha Moyo*. Nairobi: Longhorn.
- Bryman, A. (2004). *Social Research Methods* (Toleo la 2). Oxford: Oxford University Press
- Buffon, G. (1930). *Buffon's Discourse on Style*. Paris Librairie: Hatier Publishers.
- Chacha, N. C. (1980). *Ushairi wa Abdilatif: Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawaa* (1971) na *Sauti ya Dhiki* (1973) Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Chacha, N. C. (1986). *Marejeo*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Chapman, N. (1982). *The Language of English Literature*. London: Edward Arnold.
- Chimera, R. na Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman Group.
- Fadhili, E.F. (2014). Kuchunguza Dhima ya Mtindo katika tamthilia za Kihistoria: Utafiti Linganishi wa Tamthilia za Morani na Kinjekitile. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Isiyochapishwa).
- Holman, C.H. (1960). *A Handbook to Literature*. New York: Odyssey.
- Hussein, E. N. (1971). *Wakati Ukuta*. Nairobi: East Africa Publishing House.
- Hussein, E. N. (1971). *Mashetani*. Dar es Salaam: Oxford Universty Press.
- Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Ileri, J. (2011). Tamthilia kama Utendi: Uchanganuzi linganishi wa Tamthilia za *Kinjeketile* na *Mzalendo Kimathi*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Indangasi, H. (1988). *Stylistics*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Kairu, W. M. (2011). Uhalisia wa mtindo wa Ken Walibora katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja* (2011). Toleo la pili. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Kasau, M. E. (2013). Maudhui na Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Injili za Rose Muhando. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

- Katutu, R. (2013). Mtindo katika Diwani ya *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Kilanga, B. S. (2014). Ishara katika *Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Kitula, K. na Ahmed, N. (2008). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Kitula, K. n.w. (2012). *Mwongozo wa Mstahiki Meya*. Nairobi: Target Publications Ltd.
- Kitula, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Khatibu, M. S. (1986). 'Tamathali za Usemi za Kiswahili,' Katika Mulika namba 18, Uki. 1-15. Dar es Salaam: TUKI.
- Kothari, C. K. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.
- Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Usemi za Kiswahili*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.
- Leech, G. (1969). *A linguistic Guide to Modern English Poetry*. Essex: Longman Group Ltd.
- Leech, G. & Short, M. (2007) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to Fictional Prose*: New York: Longman Limited.
- Lugwiri, P. O. (2011). Sitiari, taashira na tashbihi katika Uwasilishaji wa Dhamira katika *Utenzi wa Tambuka*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Masinde, E. (1992). Mashairi huru: Uchambuzi wa dhamira na mtindo. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Mauya, A. B. (2008). *Semi: Maana na Umuhimu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing Ltd.
- Michael, T. (1998). *Language in Literature: An Introduction to Stylistics*. New York: Longman.
- Michael, T. (1992). *Language, Text and Content: Essays in Stylistics*. New York: Longman.

- M'Ngaruthi, T. K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohammed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East Africa Publishing House.
- Mohamed, S.A. (1995). *Amezidi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Muhamed, B. (2011). Usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-Adamu* (2002) na Mkusanyiko wa Hadithi Fupi wa *Sadiki ukipenda* (2002). Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Murry, J. M. (1922). *Essays in Literary Criticism*. London: Collins.
- Murry, P. (1978). *Literary Criticism. A Glossary of major terms*. New York: Longman.
- Murumba, J. B. (2013). Mtindo Katika Riwaya ya watu wa *Gehenna*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Muthubi, F. M. (2012). Mikakati na Mbinu za Usimilishwaji katika Fasihi ya Watoto. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Muthoni, M. (2014). Uhakiki wa Maudhui na Mtindo katika *Tikitimaji*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Mwanakombo, M. M. (1994). Uchambuzi wa dhamira, falsafa na mitindo katika tamthilia mbili za Chacha N. Chacha. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi (Isiyochapishwa).
- Mwita, S. M. (1994). Tamthilia mbili za Ebrahim Hussein: *Arusi na Kwenye Ukingo wa Thim*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi (Isiyochapishwa).
- Ndumbu, M. J. (2013). Matumizi ya Takriri na Sitiari katika *Utenzi wa Rasi'lghuli*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Ngara, E. (1982). *Stylistic Criticism and the African Novel*. London: Heinmann.
- Ngolo, E. K. (2011). Mabadiliko ya Kimtindo katika Ushairi wa Said A. Mohamed. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

- Ngonyani, D. (2005). 'Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake katika Jamii.' Katika Swahili Forum nambari 12, Uk.122-123. Chama cha Masomo ya Kiafrika.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyaga, P. N. (2013). Mtindo katika Mashairi ya *Diwani ya Karne Mpya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Onchangu, R. (2013). Mtindo katika Hadithi fupi na riwaya za Clara Momanyi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Okwena, S. (2013). Matumizi ya Jazanda katika Tamthilia Tatu za Timothy Arege. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Onesmus, G. (2011). Taathira ya Dhamira kwa Mtindo katika Hadithi Fupi teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Ongarora, S. O. (2007). Mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Orwell, G. (1988). *Shamba la Wanyama*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- O.U.P. (2008). *The Oxford Advanced Learners English Dictionary*. (Toleo la 8). Oxford University Press.
- Oyoyo, J. O. (2013). Uhakiki wa Fani katika Ngano tano za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- Powell, R. R. & Connaway, S. L. (2004). *Basic Research Methods for Librarians*. (Toleo la 5). London: Sage Publications Inc.
- Sally, W. & Michael A. (2005). *Oxford Advanced Learners Dictionary*. Oxford: OUP.
- Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Seale, C. (2012). *Researching Society and Culture*. London: Sage Publications Ltd.
- Simpson, P. (2004). *Stylistics: A Resource Book for Students*. London: Routledge.

- Silverman, D. (2005). *Doing Qualitative Research: A Practical Handbook*. (Toleo la 2). London: Sage Publications Inc.
- Syambo, B. K. na Mazrui, A. M. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Spolsky, B. (1988). *Sociolinguistics*. Oxford: Oxford University Press.
- Thomson, A. (2000). *An Introduction to African Politics*. London: Routledge.
- Too, M. (2011). Fani katika Tamthilia ya *Nguzo Mama*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).
- TUKI (2006). *Kamusi ya Kiingereza- Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Tunmer, G. (1973). *Stylistics*. New York: Hazell Watson & Viney Ltd.
- Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wakesho, P. M. (2010). Masimulizi na Malumbano Katika Tamthilia ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.
- Wambua, S. M. (2001). Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Wathome, R. (2003). Mitindo katika nyimbo za tohara. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).
- Wekesa, A. (2008). Matumizi ya Taswira katika Mashairi Huru ya Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

